**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 29 Mei, 2015**

*Kikao Kilianza saa 3:00 Asubuhi*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 43**

**Uwanja wa Ndege wa Pemba Kutiwa Taa**

**Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub)** - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla serikali haijajibu swali lake Nam. 43 napenda kwanza nitumie fursa hii kuipongeza serikali kwa kuweza kuanza kule Mradi wa Kubandika na Kuweka Taa katika Uwanja wa Pemba *Airport*, na kwa mnasaba huu ilikuwa hili kwa niaba ya Mhe. Mwakilishi niliondoshe hili swali lakini *for the fact of National Interest* naomba swali Nam. 43 lijibiwe kusudi watu waweze kujua ule mradi unaendeleaje na utamalizika lini.

Tarehe 13/2/2015 vyombo vya habari vimetangaza kuwa SMZ inao mpango wa kuweka taa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

(a) Je, hili suala ni kweli na nani aliyetoa ahadi hiyo.

(b) Kama kweli ujenzi huo lini utaanza na ni kampuni gani itakayojenga.

(c) Uzoefu unaonesha serikali imekuwa na wepesi kuamua kuliko utekelezaji, kwa mfano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja unakaribia mwaka mpaka leo ujenzi wa kibanda cha wagonjwa wanashindwa kujenga wakati hatua zote zimekamilika. Serikali inatoa kauli gani ambayo itakuwa ya ukweli kwa wananchi wa Pemba ili matarajio waliyonayo yatimie.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imetoa kauli ya kujenga uwekaji wa taa mpya katika Kiwanja cha Pemba, na serikali ina mpango wa kuweka taa katika kiwanja hicho cha Pemba.

(b) Mhe. Spika, kazi ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Pemba imeshaanza ambapo Kampuni ya *Safe gate* kutoka Ujerumani imechaguliwa kufanya kazi ya uletaji wa vifaa na usimamizi wa uwekaji wa taa katika kiwanja hicho. Aidha, kazi ndogo ndogo zinatarajiwa kufanywa na kampuni za ndani.

(c) Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba mradi wa uwekaji wa taa umeshaanza na kazi ya uchimbaji mitaro pamoja na ulazaji wa waya inaendelea chini ya usimamizi wa Mhandisi makini kutoka Kampuni ya *Safe gate* ya Ujerumani. Kwa mujibu wa ratiba mradi huu tunatarajia utakamilika mwishoni mwa mwezi wa sita.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri mtoto wangu hapa naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mheshimiwa serikali kwa nia safi sana imeshaamua kuanza ule mradi kwa kuanza kuchimba mitaro na hatimaye baadae kuanza kubandika taa pale. Na kwa kuwa kuna kauli ya kwamba ule uwanja unataka kupanuliwa kusudi badala ya kutua videge hivi, vichata vichata na vyengine vidogo vidogo, madege makubwa nayo yaweze kuanza kutua katika Uwanja wa Pemba *Airport* kusudi tuweze kuruka moja kwa moja kutoka Pemba mpaka nje badala ya ku-*transit* hapa Unguja au Dar es Salaam.

Je, kwa kuanza kubandika taa hivi sasa ambapo itagharimu pesa nyingi za serikali, na hatimaye mkaja mkatanua uwanja ule mkaanza kutoa miundombinu hii mnayoibandika hivi sasa ya hii mitaro ya hizo taa, haitaathiri fedha za walipa kodi wa nchi hii, jambo ambalo fedha zenyewe nchini mwetu ni masikini sana na haitakuwa ni kuharibu fedha za walipa kodi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa muda mrefu Baraza hili na wananchi wa Kisiwa cha Pemba tumekuwa tukihitaji taa kwa ajili ya huduma ya utumiaji wa ndege kwa nyakati zote usiku na mchana. Serikali imeona umuhimu wa kuweka taa, tunatambua *concern* ya Mhe. Mwakilishi kwamba uwekaji wa taa unaweza ukawa unapelekea gharama, lakini naomba nimthibitishie kwamba aina ya taa zinazowekwa ni *semi permanent light* ambazo tunapohitaji kutanua uwanja tunayo nafasi ya kubandua kuweka kwengine. Kwa

hiyo, hakuna athari yoyote ya gharama ambazo watazipata wananchi ama serikali kwa uwekaji wa taa unaowekwa hivi sasa pindi serikali tukifikia maamuzi ya kutaka kutanua na uwezo wa kufanya hivyo ukitokezea.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali hivi, tarehe 8/05/2015 kulitokea hitilafu ya ndege ya *Assalam* wakati wa kutua na sababu ya tatizo hilo ni kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha za Masika na kusababisha kiza na kutuama kwa maji mengi katika kiwanja hicho.
Je, Mhe. Naibu Waziri nilitaka kujua ni lini uwanja huo nao utafanyiwa matengenezo ili kunusuru matatizo yanayoweza kuepukika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, naomba tu nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba asifikie *conclusion* kama kumetokea athari au ajali akasema kuwa imesababishwa na kitu fulani. Utaratibu wa *aviation* uko wazi, linapotokea tatizo lolote la athari za ndege cha kwanza wanachokifanya ni uchunguzi, baada ya uchunguzi taarifa ndio inayoeleza chanzo hiki kimesababishwa na nini.

Sisi kwa upande wetu tunajua kuna baadhi ya matatizo ya uwanja lakini serikali tumeona tunaanza na hatua ya uwekaji wa taa, kuna mipango ya serikali ya kutaka kuongeza barabara ya kurukia maeneo ya maegesho pamoja na jengo.

Nimuombe tu asifikie *conclusion* ya kusema kwamba ajali hiyo imesababishwa na kitu kadhaa, tusubiri ripoti ya wataalamu watu wa *aviation* taarifa yao ndio itayoeleza chanzo na sababu ya ajali hiyo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri pia niipongeze Serikali ya SMZ kwa kuweza kuanza mradi huo wa kuweka taa katika uwanja wa Pemba.

a) Je, ni gharama gani ambazo zitachukua kuweka taa katika uwanja ule.
b) Mradi huo wa kuweka taa utachukua muda gani hadi kumalizika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, tumeeleza kwamba mradi huu utachukua kipindi cha miezi miwili kwa maana ya kwamba tulipoanza mpaka mwishoni mwa mwezi wa sita tutakuwa tumeshakamilisha mradi huu.

Gharama zilizotumika ni dola za Kimarekani 808,219 kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi wa *Safe gate* Kampuni ya Ujerumani kwa ajili ya usambazaji na usimamizi wa ujenzi pamoja na vifaa. Lakini Kampuni ya ndani ya *Skaz* tumeilipa takriban shilingi milioni 348,000,000 kwa ajili ya wakaazi na *civil works* pamoja na maeneo mengine ya kuwekea *light tubes, light holes* eneo la kuwekea *generator*, eneo la kujengea kibanda cha umeme pamoja na marekebisho madogo madogo ya kazi katika maeneo yanayojengwa, maeneo ya Uwanja wa Ndege.

**Nam. 38**

**Kitengo cha Wagonjwa wa Sukari**

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub)** - Aliuliza:-

Kitengo cha wagonjwa wa sukari kilichopo Mnazi Mmoja kuna matatizo mengi ya kufanyia kazi ikiwemo *gloves, dettol* na paa kuvuja na feni moja tu ndio linalofanya kazi.

(a) Je, *gloves, dettol* na feni inahitaji bajeti kiasi gani.

(b) Je, kweli tutafika kuwa Hospitali ya Rufaa kwa hali hiyo.

(c) Je, ni lini vitendea kazi hivyo vitapatikana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa sote katika Baraza hili Tukufu kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Pili Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na Kitengo cha Sukari kinaendelea kutoa huduma bora za matibabu ya afya kama ilivyopangiwa ikiwa ni pamoja na kuzipatia idara zake za ndani vitendea kazi muhimu kwa mujibu wa mahitaji husika ya kila kitengo. Haya yanafanyika kwa kadri ya uwezo wa fedha unapopatikana na mimi naomba kuendelea kutoa shukurani zetu za dhati na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kuendelea kutupa mashirikiano yao kila pale ambapo matatizo hutokea.

Kwa bahati mbaya wakati mwengine Wawakilishi huwa hawatuelezi mambo mengine kabla na husubiri moja kwa moja kuyaleta Barazani wakati kuna miundombinu ama vitengo vilivyopangwa maalum vya kutatua matatizo kama hayo. Kwa hiyo, naendelea kuwashukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, Kitengo cha Wagonjwa wa Sukari kwa sasa hakina matatizo ya kuvuja kwa paa, kwa vile tayari paa hilo limeshafanyiwa matengenezo, na kwa upande wa feni, feni zote sasa hivi zinafanya kazi na ile moja iliyokuwa haifanyi kazi mafundi wetu wa ndani tayari wanalifuatilia tatizo hilo ili iweze kufanya kazi kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, mbali na hayo Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inaendelea kutoa vifaa mbali mbali vya kutendea kazi kwa mujibu wa mahitaji ya kitengo husika na kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha katika idara hiyo. Hivyo kwa sasa Kitengo cha Sukari hakina matatizo ya *gloves* wala *dettol* na kazi za utoaji matibabu zinaendelea kama zilivyopangwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kulifanyia ukarabati hilo paa pamoja na kupeleka *dettol* na *glove* na mambo mengine katika kitengo hiki cha wagonjwa wa sukari.

Kwa kuwa kisukari ni miongoni mwa *Non-Communicable Diseases (NCD),* na kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa sukari katika miaka hii ya karibuni, nadhani ni kutokana na utaratibu wa maisha yetu kwa sasa. Na kwa kuwa pamoja na kuziba hilo paa lakini hii hata kwenye wodi ya wagonjwa wa sukari sasa hivi ukienda ni tatizo, vitanda viko karibu na ugonjwa wenyewe huu una matatizo mengi na wanahitaji wapate *intensive nursing care* katika *well sanitary facilities.*

Sasa Mheshimiwa ni lini serikali itafikiria kujenga wodi nzuri na kuwahamisha katika ile wodi ndogo ambapo wagonjwa wanabanana banana huku harufu pamoja na mambo mengine yakiwachagiza wagonjwa wenyewe pamoja na wale *nurse* waliomo mle ndani pamoja na madaktari. Ni lini mutatutafutia pahala pazuri wagonjwa wa sukari ili waweze kupata sehemu iliyokuwa ni *aerated*, iliyokuwa na usafi na yenye hewa ya kutosha, ni lini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, ni kweli magonjwa ya sukari yanaingia katika *Non-Communicable Diseases;* yaani maradhi yale ambayo hayaambukizi na kuna kitengo maalum ambacho kimetengwa.

Pia ni kweli kwamba tuna uhaba mkubwa sana wa nafasi ndani ya kijiji chetu cha Mnazi Mmoja, tunakiita kijiji cha Mnazi Mmoja kwa sababu Mhe. Spika tulipoweza kukamilisha lile tatizo la maji ambalo nililitolea taarifa hapa, hata mimi mwenyewe sikuwa najua kama tunatumia lita 300,000 kwa siku hakuna chochote Unguja kinachotumia lita 300,000 kwa siku. Kwa hiyo, kile ni kijiji kikubwa sana.

Mhe. Spika, kwa takwimu za haraka Mnazi Mmoja ina uwezo wa kulaza wagonjwa 450, lakini kutokana na uhaba tuliokuwa nao Mnazi Mmoja huchukua mpaka wagonjwa 660 naomba sana mtuvumilie wale madaktari wa wauguzi wanafanya kazi katika *difficult circumstances*, kwa sababu Mnazi Mmoja kama nilivyosema hapo awali ilijengwa kwa takwimu ya wananchi wachache zaidi wakati huo na sasa inatumika na wananchi wengi sana.

Mhe. Spika, hiki ni kitengo kimoja tu lakini miongoni mwa mambo tunayoendelea kuyafanya *bad capacity* yetu kama nilivyosema ni 440 na tunachukua wagonjwa mpaka 600 wakati mwengine magodoro yanawekwa chini inabidi tuwahudumie, huwezi kuwarudisha wale wagonjwa. Na tuna *under staffing* ambayo tayari tumeomba Utumishi. Tumeomba Wizara ya Fedha ili tupate *allocation* ya bajeti ya kutosha ili tuwe na *staff* wengi zaidi hususan katika zile wodi ambazo zinahudumia wagonjwa moja kwa moja ikiwemo pamoja na *maternity*.

Mhe. Spika, ninachotaka kueleza ni kwamba jitihada zinaendelea tunafanya jitihada za aina tatu hivi sasa hivi. Tunafanya jitihada ya kujenga hospitali za Wilaya ambazo zitapunguza mzigo Mnazi Mmoja inabeba mzigo kuliko uwezo wake wa kubeba mzigo, inabeba mzigo mzito sana, na unajua hata binadamu akibeba mzigo mzito aidha atavunjika mabega au anavunjika mgongo. Kwa hiyo, tunafanya mpango wa hospitali tatu za Wilaya, hilo la kwanza (*District Hospital*) mazungumzo yanaendelea kwa ajili ya makubaliano ya kujenga hizo *District Hospital* ikiwemo pamoja na Binguni.

La pili, tunaamini sana tutakapomaliza Abdalla Mzee wagonjwa kutoka Pemba watakuwa hawaletwi tena hapa Unguja, kwa sababu kuna baadhi ya wagonjwa wanakuwa *referred* kutoka Pemba huongeza *load* ya Mnazi Mmoja. Kwa hiyo, tunaamini sana Abdalla Mzee ikishakamilika wale wagonjwa wataendelea kubakia Pemba, na pengine *load* ya Mnazi Mmoja tutaweza kuipunguzia katika *facility* za Abdalla Mzee.

La tatu, kuna Mradi ule wa *ORIO* ambao pale pamezungushwa mabati pale pembeni ya Mnazi Mmoja na tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametwambia tuliangalie eneo lilokuwa limebakia la mbele kwa ajili ya kupata *extension* nyengine ya hospitali hiyo hiyo ya Mnazi Mmoja.

Kwa hiyo, hapo pia majadiliano yanaendelea, lakini Mradi wa *ORIO* ushaanza na unadhaminiwa na Serikali ya Uholanzi kwa asilimia 50 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 50, kwa hiyo, ni *fifty fifty partnership.* Kwa hiyo, nafasi hizo zikishakamilika Mhe. Mwakilishi ndipo tutakapoweza kupata *dedicated ward* ya wagonjwa wa sukari, wagonjwa wa *renal* na mambo ya *urology* na mambo ya *kidney,* haya tunaweza kupata *dedicated ward* ya wagonjwa wa moyo tukaweza kupata *dedicated ward* ya wagonjwa wa *cancer*.

Ni kweli sasa hivi tunawachanganya katika wodi kwa sababu ya uhaba wa nafasi, lakini tukishapata hizi *facilities* kwa kuanzia na *orio* tumeangalia pia eneo la Kidogo Chekundu kuna eneo kubwa sana ndani ya Hospitali ya Kidogo Chekundu ambalo sasa watu wanalima mihogo na mazao mengine kama ya migomba.

Pia eneo lile tumeliangalia kwa ajili ya kufanya *extension* ya *wards* hizi maalum *specialized wards* kama vile ***diabetes,*** yaani ugonjwa wa kisukari na maradhi mengine. Kwa hiyo, jitihada zinaendelea na tunaendelea kuzungumza na wafadhili mbali mbali mara tu *orio* itakapokamilika itapunguza hilo tatizo ulilolieleza la wagonjwa wa sukari kulazwa wote kwa pamoja katika wodi moja, na kuwa na uhaba wa nafasi na mambo ya harufu na mambo mengine. Kwa hiyo, naamini Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaweza kulifanikisha hilo *inshaallah*. Ahsante.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa kuwa ugonjwa wa sukari sasa hivi umekuwa ni ugonjwa mkubwa sana hapa Zanzibar, na kwa sababu utaratibu mzima wa kujua mwenendo wa sukari wa mgonjwa anatakiwa apimwe angalau mara mbili kwa wiki. Je, na kwa sababu vile vile wagonjwa wengi wa sukari ni watu ambao hawana uwezo mkubwa wa kulipa vipimo hivyo. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba sasa hivi kunatakiwa kupima sukari kuwe bure?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya**: Mhe. Spika, naomba nikubaliane naye kwamba tatizo la sukari linaendelea kukuwa na hii kutokana na tabia zetu za kimaisha. Watu kupunguza kufanya mazoezi, kula bila ya mpangilio, kula baada ya saa mbili usiku wanasema wataalamu pia nayo inasababisha, kwa sababu *digestion system* inachelewa kuyayusha chakula, kwa hiyo unalala nacho kile mpaka asubuhi ndani ya tumbo na mengi mengine ziko sababu nyingi sana.

Naomba pia niseme kwamba tunaendelea kupata misaada mbali mbali katika Idara hii ya Kisukari, wanachoombwa sasa hivi wagonjwa kuchangia zile *sticks* zinapokwisha za kupimia damu ama mkojo. Kwa hiyo zinapokwisha ndipo wanapoomba, na hii yote inatokana na kwamba kuna uhaba wa bajeti. Lakini bajeti itakapopatikana na Bohari Kuu ikatapoweza kununua zile *sticks* za kutosha na sio rahisi ni ghali. Siku hizi mashine ya sukari unaweza kuuziwa bei nafuu kabisa au

rahisi kabisa lakini wanajua watakupata kwenye *sticks* za kupimia, wanajua wenyewe wale wanaotengeneza kwamba watakuja kukupata kule.

Kwa hiyo, bei yake pia si rahisi, kwa sababu kile kiboksi kinauzwa shilingi elfu arubaini na tano na zimo kama 50 au sitini. Kwa hiyo, mara nyingi wagonjwa wanachangia kwa ajili ya zile *sticks*, lakini uwezo utakaporuhusu nia yetu ni kutoa zile *sticks* na tutaendelea kuomba misaada sehemu mbali mbali ili tuweze kupata zile *sticks* ambazo zitakwenda sambamba na zile mashine za kupimia sukari. Nashukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:**Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Naibu Waziri katika jibu lako mama ulisema kuwa tayari sasa hivi vifaa vya aina ya *gloves* na vitu vyengine na *dettol* kuwa tayari vimekamilika katika wodi hiyo.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini wewe umekwenda katika wodi hiyo ukahakikisha kwamba vitu viko tayari.

(b) Mhe. Spika, utakubaliana na mimi mpaka jana wenyewe Madokta wanaendelea kununua *gloves* hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa sababu ni miongoni mwa Wawakilishi wote ingechukuliwa takwimu anayetembelea sana Hospitali ya Mnazi Mmoja nafikiri yeye angeongoza maana takriban kila siku yuko pale Mnazi Mmoja na namshukuru kwa njia ya pili miongoni wa Mwakilishi ambaye anakuja kunidokezea kila anapoona kuna mapungufu au kuna tatizo huwa anakuja ananinong'oneza ananidokezea.

Sasa naomba leo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ukiangalia *TV* leo saa mbili na robo taarifa ya habari utaona ziara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo wafanyakazi wa Mnazi Mmoja wanazungumzia kupata hizi *gloves* na *dettol* na walipata juzi katika *stock* mpya iliyoingia.

Kwa hiyo, naweza kusema hizi taarifa *latest* ni jana kwa ziara ambayo mimi mwenyewe nilifanya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, na nilifanya Mapinduzi Kongwe nilifanya *Maternity* pamoja na lile tatizo la maji, na jana wakati nipo pale kwenye ziara maboksi mengine ya *gloves* yakawa yanatoka Bohari kule Maruhubi yanaletwa pale kwa ajili ya kuongezewa, na yule mfanyakazi ambaye nimezungumza naye kwenye *TV* leo utamsikia anazungumza yeye alikiri kuwa huwa kunatokezea *shortage* wakati mwengine hususan zile *gloves* zinapokwisha kule Bohari ama *dettol*.

Kipindi cha *shortage* kinakuwa baina ya kumalizika kule na kuletwa mzigo mpya hicho kinakuwa kipindi cha *shortage* na wakati mwengine wagonjwa hulazimika kuchangia. Lakini kwa upande wetu sisi sasa hivi tunajitahidi sana kwa hii *system* mpya, *Electronic logistics Information System* ambayo imefungwa huwa inaonesha mapema kabla vifaa kumalizika ili wale Bohari waweze kuagizia mapema.

Kwa hiyo, taarifa hizi Mhe. Spika, naomba kumjuilisha Mhe. Makame Mshimba kwamba ni jana mwisho imefanyika ziara, *dettol* ipo, *gloves* zipo pamoja na dawa zile zote za kumsaidia mzazi kupata uchungu na nyenginezo zote zipo na zipo za kutosha. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

**Nam. 64**

**Ukosefu wa Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji**

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza**:**

Kwa muda mrefu Wawekezaji wamekuwa wakilalamika kutopatiwa maeneo ya ardhi kwa ajili ya Uwekezaji, hali ambayo hupelekea kwa baadhi ya Wawekezaji kushindwa kuanzisha baadhi ya miradi hiyo hususan katika maeneo ya Kiwengwa, Pwani Mchangani na Nungwi.

(a) Kutokana na kadhia hii ningependa kujua ni hatua gani ambazo Serikali imezichukukua katika maeneo hayo ya Uwekezaji.

(b) Na kwa kuwa baadhi ya maeneo hayo yamechukuliwa na baadhi ya watendaji kwa ajili ya manufaa yao binafsi, Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakiki ardhi yote iliyochukuliwa na baadhi ya watu binafsi ili kuweza kuwasaidia Wawekezaji hao kutokaa kwa muda mrefu kwa kusubiria maeneo hayo kwa ajili ya kuanzisha miradi hiyo.

(c) Je, ni maeneo mangapi mpaka sasa ya ardhi ambayo hati zake zimefutwa kutokana na kushindwa kuendelezwa, na pia ni maeneo mangapi ambayo yamezungushwa ukuta bila ya kuendelezwa na wamiliki wake ni nani katika maeneo hayo hususan katika eneo la Kiwengwa.

**Mhe. Spika:**Waheshimiwa Wajumbe hili ndilo swali la jana ambalo lilileta utata kidogo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Wizara haijapokea lalamiko kutoka kwa Wawekezaji juu ya kupatiwa eneo la Uwekezaji tukiwa kama taasisi husika, hata hivyo hatujawahi kuwa na kumbukumbu ya Muwekezaji kukosa eneo la Uwekezaji.

(a) Mhe. Spika, Wizara inapogundua kuwa Mwekezaji haitumii ardhi iliyokodishwa kwa mujibu wa makubaliano ya Uwekezaji na kwa muda uliopangwa hatua inayofuata ni kutoa indhari ya ufutaji wa Mkataba ikifuatiwa na hatua ya ufutaji baada ya muda wa indhari kupindukia.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu tayari imeshafanya uhakiki wa maeneo kwa kushirikiana na taasisi nyengine ambazo ni wadau wakubwa katika Uwekezaji na hatimaye kutoa ripoti ya maeneo yote ambayo hayajaendelezwa na tayari imeshachukua hatua ya kufuta miradi kadhaa na kutoa indhari kwa Wawekezaji ambao bado wanashindwa kuendeleza bila ya sababu ya msingi.

Maeneo ambayo hati zake zimefutwa katika eneo la Kiwengwa na wawekezaji wake ni:-

| **Mkataba wa ukodishwaji Ardhi** | **Mmiliki** |
|---|---|
| i. DP. No.181/1995 | KAMPUNI YA LOTUS BEACH VILLA |
| ii. DP. No.832/2007 | KAMPUNI YA MASAI RESORT |
| iii. DP. No. 866/2007 | KAMPUNI YA LAND MARK HOTEL |
| iv. DP. No. 1099/2011 | KAMPUNI YA ZANZISUN |

2. Maeneo ambayo yamezungushiwa kuta bila ya kuendelezwa ni kama haya yafuatayo:-

i. Hafidh Seif Majid
ii. Kassim Maalim
iii. Blue Bay
iv. Yakub
v. Muzammil
vi. Turki
vii. Kampuni ya Uroa Safari Inn

Mhe. Spika, Wizara yangu imebaini pasi na shaka kuwa lengo la wananchi kuhodhi ardhi kwa kuzizungushia ukuta ni kuipandisha thamani ardhi hizo na kuuza kwa bei kubwa. Mtindo huu unafanywa katika maeneo ya fukwe. Wizara yangu imeshaanzisha utaratibu wa kuzifuta hati hizo na kuzirejesha ardhi hizo katika mikoni ya Serikali.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Spika, nataka kujua kwa muda gani indhari huchukua kabla ya muwekezaji kufutiwa ardhi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, muwekezaji yeyote anapokuja katika wizara yetu na kudai eneo, kitu cha mwanzo tunafunga mkataba wa kumkodisha ardhi hiyo na tunampa muda maalum wa kuliendeleza lile eneo, na pindipo utakapomalizika ule muda ambao tunakubaliana hajaliendeleza eneo lile basi ni kulifuta eneo lile na hususani inategemea na inawezekana pengine kutokana na shughuli zake yeye na makubaliano mara nyengine tunakubaliana aidha miaka mitatu, mitano au hadi miaka saba. Kwa hiyo, inategemea kwa vile ambavyo tunavyokubaliana.

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri anayotupa kutokana na swali hili muhimu.

(a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kuwa Wizara yake imefanya utafiti wa maeneo haya na wizara ikishirikiana na taasisi nyengine katika kufanya uhakiki huo, ningeliomba kujua ni taasisi gani hizo.

(b) Kwa sababu swali mama limesema kuwa kuna wawekezaji wengi tu wanataa maeneo lakini kutokana na sababu zilizoelezwa katika swala wanashindwa na kuvunjia moyo.

Mhe. Spika, naomba kujua mpaka hivi sasa tuna wawekezaji wangapi wamekuja kwa muda gani na hawajapata hayo maeneo, na kwa sababu wawezekaji ni kitega uchumi kikubwa kwa serikali yetu wizara yake ina mpango gani hasa wa kuona hili suala limemalizika kikamilifu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, taasisi ambayo tumeshirikiana nayo katika kulifuatilia hili ni Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar hilo moja.

Vile vile katika suala la wawekezaji ambao wamekuja ndani ya Afisi yetu na kuja kudai maeneo kama nilivyoeleza hapo awali hatujapata malalamiko ya muwekezaji yeyote kuja kudai ardhi ya uwekezaji na akakoseshwa ardhi hiyo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri pamoja na maneno yako mazuri sana umeeleza hapa kuwa upo katika hatua za mwisho wa kuweza kuwafutia hao wawekezaji ambao walioweka mafuta na halkadalika na wengine.

Je, Mhe. Naibu Waziri umewahi kuwapa *notes* ya kutoa indhari jambo hilo, na kama hujatoa huoni Mheshimiwa ukianza kuwafutia tu moja kwa moja suala hilo iko hatari ya kupelekwa wizara yako Mahakamani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba hatuwezi kumfutia mwekezaji yeyote au mwananchi yeyote ambaye tumempa eneo la kujenga nyumba au la kujenga hoteli bila ya kumpelekea barua ya indhari yaani *notice*.

Kwa hiyo, hatuwezi kufanya hivyo, kwa hiyo wale wote ambao tumewafutia basi tumetanguliza *notice* kwa ajili ya kumpa indhari ya kutaka kufuta kiwanja hicho. (*Makofi*)

**Nam. 65**

**Ulipaji Kodi katika Nyumba za Serikali**

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza**:**

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, Rais wa Kwanza marehemu Sheikh Abeid Amani Karume alijenga nyumba za kisasa na kuzigawa kwa baadhi ya wananchi wake kwa misingi ya kuwapatia makaazi bora. Aidha, kwa muda mrefu wananchi hao wamekuwa wakiishi bila ya kulipa kodi.

(a) Na kwa kuwa Serikali ilikuwa na dhamira ya kuwajengea maisha bora kwa kila Mzanzibari, Je, kwa nini Serikali imekuwa ikitoza kodi katika nyumba hizo.
(b) Je, ni nyumba ngapi kwa upande wa Unguja na Pemba zilizopangishwa na kumilikiwa na watu binafsi.
(c) Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonesha kuwa viongozi na baadhi ya watendaji wengi wa Serikali ndiyo wadaiwa wakuu. Je, Serikali imechukua hatua gani ili iwe mfano kwa wananchi katika suala zima la ulipaji kodi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye kufungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado imeendeleza kuheshimu na kutekeleza maamuzi ya Mhe. Abeid Amani Karume ya kuwapatia makaazi bora bure kwa wale wote waliopewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Wananchi wote waliopewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ambao bado wapo hai wataendelea kuishi katika Nyumba za Maendeleo bure hadi mwisho wa maisha yao.

Pindi wananchi hao watakapotangulia mbele ya haki, nyumba hizo watakodishwa watoto wao.

(b) Kwa upande wa Unguja Nyumba za Maendeleo katika maeneo ya Kikwajuni, Michenzani, Kilimani, Gamba, Makunduchi, Bambi/Mpapa jumla ni 2,253 kati ya hizo za Serikali ambazo zimepangishwa ni 1,138 na za binafsi ni 1, 115.

Kwa upande wa Pemba Nyumba za Maendeleo katika maeneo ya Machomane, Wete, Mtemani, Madungu, Micheweni, Kengeja na Mkoani jumla ni 488 kati ya hizo za Serikali ni 274 na za binafsi ni 214.

(c) Ni kweli kuwa Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonesha kuwa nyumba zilizokodishwa kwa Taasisi za Serikali ndizo zenye madeni. Taasisi hizo nyengine zimerekebisha na kulipa madeni yao, na pia baadhi ya viongozi wenye madeni wamelipa madeni hayo.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Naibu Waziri juu ya swali la lile watu ambao wanapewa zile nyumba kukaa mpaka watakapofariki.

Mhe. Spika, katika kulifatilia suala hili lilifikia pahala sasa kuna wajane ambao walikuwa wameachwa na marehemu wale. Sasa je, katika utaratibu ambao umepangwa na serikali wale wajane ambao wameachwa na waume zao ambao walikuwa wamepewa nyumba na marehemu Mzee Abeid Aman Karume serikali imewatengenezea utaratibu gani katika kuendelea kukaa katika nyumba zile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza Wizara yangu kupitia Idara ya Nyumba imewaita wale wote ambao wamepewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume wakiwemo wale wenyewe pamoja na wajane na watoto wao. (Makofi).

Lakini pia tumepata malalamiko ya aina hiyo kwamba je, wale wajane watachukuliwaje. Kwa hivyo, Wizara yangu imewataka wale wajane wote wa wale waliopewa nyumba hizo na marehemu Mzee Abeid Amani Karume waje Wizarani na tutawaelekeza jinsi gani ya kuwasaidia. (*Makofi*).

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mbali na majibu ya Mhe. Naibu Waziri na katika majibu yake ametaja idadi ya nyumba ambazo zinakodishwa kwa Unguja na Pemba. Na kwa Unguja ametaja kwamba nyumba 1136 na kwa Pemba ni 488, jumla ni 1,624.

Je, ni kiasi gani cha fedha ambazo zinakodishwa nyumba hizi ambazo zinazopatikana kwa mwaka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, ahsante sana naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kama nilivyoeleza na kama alivyofahamu kwamba nyumba ambazo tumezipangisha ni sawa sawa na idadi hiyo aliyoitaja, lakini pato ambalo tunalolipata kwa mwaka basi Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi nimjibu kwa maandishi. (*Makofi*).

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante na mimi niweze kujibu maswali mawili Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, nilikuwa ninawaamshaamsha Waheshimiwa naona kama walikuwa na baridi baridi, ndiyo nikaona nitie nahau kidogo angalau na nini. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa wangu Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mzee wetu Abeid Amani Karume alikuwa na historia ya kukaa na marafiki pamoja na watu waliokuwa karibu nao katika utendaji wa kazi.

Lakini baada ya hapo aliamua kwa makusudi kujenga nyumba zile na kuona awape kama kitu ambacho iwe ni historia na wao waweze kumkumbuka.

Je, Mhe. Naibu Waziri kutokana na hali ilivyo hivi sasa na kutoa kauli ya Serikali kusema kuwa hao wataendelea kuishi, lakini watoto wao watakuja kulipa kodi. Je, huoni ile dhana yake Marehemu kuwa munaiondosha.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, naomba kuongezea jibu la nyongeza la Mhe. Mshimba kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama jibu la msingi linavyoeleza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuheshimu maamuzi ya Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume na wale wote ambao walipewa nyumba na Marehemu Karume, basi nyumba hizo wataendelea kukaa katika kipindi chote cha maisha yao.

Watoto ambao ni warithi wa wazee hao, hao umewekwa utaratibu maalum wa Serikali na ndiyo maana wameitwa ili watoto hao kwa wale waliopewa nyumba, basi tutatengeneza utaratibu waweze kukodishwa. Kwa kufanya hivyo ni namna ya kuendelea kuwasaidia lakini wale ambao nyumba zao zilivunjwa na wakalipwa, basi wale wataendelea kumiliki nyumba hizo ni zao na zitaendelea kurithiwa na warithi wao.

Lakini wale ambao walipewa kwa hisani na urafiki, wale watoto wao warithi wao hawatoendelea kuwepo pale kwa kukaa bure, wao watabidi wakodishwe ili waweze kuendelea kukaa pale.

Kwa hivyo, huo ni uamuzi wa Serikali na tumefanya hivyo kuwasaidia wao. Kwa sababu Marehemu Mzee Karume alichokifanya ni kuwasaidia wale tu marafiki zake, hakufanya pamoja na warithi wake ni kama mfano wa eka, tunasema eka hairithiwi ndiyo utaratibu mzima unaotokana na *logic* ya maneno haya.

Kwa hivyo, wale watoto ama watu wengine ambao wana mirathi wa yule ambaye amepewa nyumba na Marehemu Mzee Karume, watafanyiwa utaratibu wa kukodishwa. Ndiyo maana tumetaka wote waje tusikilizane nao na kodi zenyewe zitakuwa ni za muafaka sana ili waweze kuishi bila ya matatizo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe jana muliunga mkono hoja hii, kuruhusu kwamba sasa hoja hii ijadiliwe. Naomba basi kumkaribisha kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe muhtasari wa hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, kabla sijawasilisha hotuba naomba nimpongeze Mhe. Haji Mwadini Makame - Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa majibu yake ya kuridhisha. (*Makofi*).

Baada ya pongezi hizo naomba nichukue nafasi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili kutekeleza wajibu wa kulijenga Taifa letu.

Aidha ninapenda kuchukua nafasi hii pia kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Abubakar Khamis Bakar, Katibu Mkuu ndugu Asaa Ahmad Rashid na Naibu Katibu Mkuu wake Ndugu Mdungi Makame Mdungi na watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria ambao kwa kipindi chote cha miaka miwili na nusu tumefanya nao kazi kwa mashirikiano makubwa. Naomba nikiri kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara ambazo zimefanikiwa sana katika utendaji wake kutoka na kupokea na kufanyiakazi kwa vitendo ushauri unaotolewa na kamati. Nidhamu hii ya utendaji ndiyo leo inanifanya kwa niaba ya Kamati, kuwapongeza watendaji wa Wizara hii, na kuwataka waendelee kudumisha mashirikiano baina yetu na wao.

Mhe. Spika, kazi yetu ya kupitia Bajeti ya Wizara hii isingekamilika bila ya mashirikiano ya hali ya juu ya wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao walifanya kazi hii kwa kujitolea. Kazi kubwa imefanywa na

Kamati hii chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu mahiri, Mhe. Ussi Jecha Simai ambaye hivi sasa anapata nafuu kutokana na mitihani wa maradhi, na tunamuomba Mwenyezimungu ampe afya njema na uzima ili arudi tena na kuungana na sisi katika kuwatumikia wananchi wetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba nitumie muda huu mchache, kuwatambuwa Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala huku nikithamini mchango wao mkubwa uliofanikisha Kamati hii kuwasilisha muhutasari huu wa hotuba. Naomba niwataje kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ussi Jecha Simai | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe |
| 4. Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Mjumbe |
| 7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |

Mhe. Spika, Katika kipindi chote cha miaka miwili na nusu ya uhai wa kamati hii, shughuli zake zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wetu wa Kamati, ambao nawashukuru kwa kushirikiana nasi kwa kipindi chote hicho, pamoja na shukurani hizo naomba niwataje kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Aziza Wazir Kheir | Katibu |
| 2. Ndg. Khamis Hamadi Haji | Katibu |

Mhe. Spika, Kwa niaba ya wajumbe wa kamati tunawashuru sana.

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo sehemu ya kielelezo cha utawala wa sheria katika nchi, kukosekana kwa Wizara hii kunapelekea utaratibu mbovu wa utekelezaji wa sheria za nchi. Wizara hii ndiyo inayoratibu uendeshaji wa moja ya mihimili mitatu ya dola ambao ni Mahakama, kutokana na jambo hilo ndiyo maana nikatangulia kusema kuwa Wizara hii ni sehemu ya kielelezo cha utawala wa nchi kutokana na umuhimu wake huu.

Mhe. Spika, Katika bajeti ya mwaka huu inayotumia mfumo wa programu, Wizara ya Katiba na Sheria, imepangiwa programu kuu mbili katika fungu la Wizara, ambazo ni programu ya Usajili na Usimamizi wa Masuala ya Dini yenye programu ndogo nne, na programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta na sheria yenye programu ndogo tatu.

Mhe. Spika, Katika programu kuu ya kwanza, kamati imepitia programu zake nne, ambapo programu ndogo ya kwanza ya Usajili wa Matukio ya kijamii

inayosimamiwa na Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, imewekewa lengo kuu ambalo ni kuimarisha mfumo wa usajili wa matukio. Katika kufikia lengo hilo ofisi ya Vizazi na Vifo imepangiwa Shilingi 421, 191,000. Kamati yetu imetazama changamoto za Ofisi hii na kuona kuwa kiwango hicho cha fedha ni kidogo kuweza kufikia malengo hayo kwa ufanisi, na kwa kuwa keki yetu haitoshelezi kamati yetu inaomba Serikali kuhakikisha kuwa hicho kidogo kilichokasimiwa kwa Ofisi hii basi kipatikane ili Ofisi hii ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo iweze kufikia sehemu ya lengo na shabaha zilizomo katika programu iliyopangiwa.

Mhe. Spika, Kamati yetu inachukuwa nafasi hii kutambuwa na kuipongeza Ofisi hii kwa kujitahidi kutanuwa wigo wa usajili kwa maeneo yote nchini. Takribani kila Wilaya nyingi sasa imeshawekwa Afisi za Usajili wa Vizazi na Vifo na kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Mhe. Spika, Kamati imeelezwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na sheria imetayarisha Mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Sheria *(Zanzibar Legal Sector Reforms)* ambapo pamoja na mpango kazi, miradi sita imeambatanishwa na Mkakati huo. Moja ya mradi huo ni Mradi wa kuimarisha Usajili wa Vizazi, Vifo, ndoa, talaka na kuasili mtoto. Kamati yetu inapongeza hatua hiyo kubwa iliyofikiwa, hofu yetu kubwa katika utekelezaji wake ni ile ile ya upatikanaji wa fedha za kutosha katika kuendesha Mradi huo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kupitia Tume ya Mipango, ambayo miradi hiyo itapelekwa kwake kwa hatua zaidi, kukaa na Wizara ya Katiba na Sheria na kuona ni namna gani miradi hiyo itaingizwa katika mipango ya Serikali ili kupatiwa fedha na hatimaye iweze kutoa matokeo yanayokusudiwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, Kamati imepitia programu ndogo ya pili, ya usajili wa Biashara na Mali, ambayo katika bajeti ya mwaka huu 2015/2016, imetengewa shilingi 1,290,605,000, chini ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali. Katika kufikia lengo kuu la kuimarisha mfumo wa usajili wa biashara na mali, kamati inashauri Serikali kuitumia Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, kuweka mfumo mmoja wa usajili wa Kampuni, jumuiya na nyaraka kwa njia ya dijitali.

Mhe. Spika, Mfumo mmoja wa usajili wa Kampuni na jumuiya nyengine kwa njia ya dijitali ni muhimu katika kuimarisha ukusanyaji kodi na uwekaji wa takwimu kwa usahihi. Kamati imeona kuwa kampuni zinazosajiliwa nchini taarifa zake za usajili zinawekwa na Wakala wa Usajili wa Bishara na Mali, kampuni hizo hizo zinafanya biashara na kutakiwa kulipa kodi ambapo baadhi ya Kampuni hizo zinapopeleka marejesho katika taasisi za kodi, huwa hazipeleki baadhi ya taarifa

muhimu kwa nia ya kukwepa kodi au kupunguza viwango vya matozo na kuikosesha mapato Serikali.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ametutaka wajumbe wa Baraza hili kumsaidia kutambua vyanzo vya mapato na yeye atavishughulikia. Katika kutambua huko kamati yangu inaona kuwa uwepo wa mfumo mmoja wa usajili wa Kampuni kwa njia ya dijitali ni chanzo muhimu cha mapato na kitasaidia kuongeza mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, katika mfumo huo taarifa za Kampuni zote zitawekwa katika mfumo wa dijitali na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, ambapo taasisi nyengine za kodi kama *TRA* na *ZRB* zitaweza kupata taarifa hizo kwa usahihi kutoka kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na kuweza kuzitoza kodi taasisi hizo kwa usahihi. Kamati yangu inaomba Serikali kuisaidia mipango ya kuanzishwa kwa mfumo huo ambao wataalamu wameshafanya *'study'* kwa awamu ya kwanza, na hivi sasa umekwama utekelezaji wake katika hatua zilizobakia kutokana ukosefu wa fedha.

Mhe. Spika, baadhi ya nchi za hapa hapa Afrika, zimefanikiwa katika kuimarisha mapato yake ya ndani kupitia mfumo huu wa usajili wa Kampuni na Jumuiya nyengine kwa mfumo mmoja wa dijitali, mfano mzuri wa hizo ni jirani zetu Rwanda, ambapo wao wameanza kupata mafanikio katika mfumo huu. Kamati imeona kuwa katika bajeti ya mwaka huu 2015/2016, kuna Mradi wa Mageuzi ya Mfumo wa Usajili wa Biashara umetengewa shilingi bilioni moja, kamati inasisitiza sana fedha hizo zipatikane ili mfumo huo uanzishwe.

Mhe. Spika, katika programu ndogo ya Usimamizi wa Hakimiliki, imewekewa lengo la kuimarisha Usimami wa upatikanaji wa haki za wasanii na wabunifu. Kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Hakimiliki na Mkurugenzi wake kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia haki za wasanii na wabunifu licha ya uchanga wake na changamoto kadhaa zinazokabili Ofisi yake.

Mhe. Spika, programu hii ndogo ya Usimamizi wa Hakimiliki imetengewa shilingi 240,000,000, ambazo hizo zimekusudiwa kuleta matokeo yaliyolengwa kwa Ofisi hii. Kamati yangu imekuwa ikitafakari kwa kiasi gani fedha hizo zitaweza kutatuwa changamoto za Ofisi, mbali ya kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kamati imetembelea Ofisi hii na imebaini kuwa kuna baadhi ya vitendea kazi muhimu vinakosekana kama vile usafiri. Kama tunavyojua kazi za Ofisi hii siyo za Ofisini tu, pia inahitajika kufatilia ukusanyaji wa mirahaba katika vyombo mbali mbali vya habari na mahoteli. Kamati inashauri Serikali kuiongezea bajeti Ofisi hii ili iweze kutatua changamoto hizo na kufikia malengo yake.

Mhe. Spika, Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki ina upungufu wa wataalamu mbali mbali hasa katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, tokea mwaka 2012 Ofisi hii imekuwa ikiomba kupatiwa wataalamu hao na wengine katika fani mbali mbali, lakini hadi hivi sasa bado Tume ya Utumishi Serikali haijafanikisha kupatikana kwa nafasi hizo.

Mhe. Spika, Kamati inaitanabahisha Serikali kuwa isitegemee mfumo huu wa bajeti wa *PBB* ulete matokeo wanayokusudia kwa haraka bila ya kwanza kuziwezesha taasisi zinazosimamia progamu hizo, kwa kuzipatia nyenzo na wataalamu wa kufanikisha mipango hiyo. Tunaitaka Tume ya Utumishi ya Serikali kuwapatia wataalamu hao ili lengo lililowekwa katika Programu hii ndogo ya Usimamizi wa Hakimiliki liweze kufanikiwa.

Mhe. Spika, Kamati imebaini changamoto nyengine ya usimamizi wa hakimiliki kwa vyombo vya sheria hasa baadhi ya mahakama zetu ambazo wanapopelekwa watuhumiwa wanaonyonya haki za wasanii sheria hazifatwi ipasavyo. Kamati yangu inataarifa ya kesi ambayo inamuhusisha mtu mmoja aliyetumia kinyume na sheria hakimiliki na mtu huyo kutakiwa kulipa na akakataa. Jambo la kusataajabisha, wakati mtu huyo anapelekwa mahakamani akajisifu kuwa atatumia uwezo wake wa kifedha kuachiwa, na kweli kesi ilipofika mahakamani mtu huyo aliachiwa kwa sababu zinazotia shaka.

Mhe. Spika, mambo haya ndiyo tunayoyapigia kelele kila siku katika Baraza hili na vyombo vyetu vya kusimamia haki vifuate sheria, haiwezekani mtu anapelekwa mahakamani anajisifu kutumia uwezo wake wa kifedha na kuachiwa na huku ameshadhulumu haki ya mtu. Kamati inaomba Wizara kulichunguza suala hili kwa kumchukuliwa hatua za kinidhamnu Hakimu aliyehusika na kadhia hii ya aibu kwa mujibu wa sheria. Aidha, tunaiomba Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ilifuatilie suala hili kwa kuwasiliana na Taasisi ya Hakimiliki, na hatua stahiki zichukuliwe ili kukomesha mambo haya yasijitokeze tena na kuvunja moyo juhudi za wasanii na ofisi zetu zinazosimamia haki zao.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Dini imewekwa chini ya Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana na Ofisi ya Mufti ambapo Kamisheni ya Wakf imekasimiwa shilingi 587,800,000 na Ofisi ya Muft imetengewa shilingi 357,612,000. Kiasi hicho cha fedha ni kidogo kwa taasisi hizo, zenye majukumu makubwa yanayogusa jamii moja kwa moja. Kamati yangu inashauri kuwa katika kuhakikisha kuwa Taasisi hizo mbili angalau ziweze kufanya majukumu yake ya kawaida, basi zipatiwe fedha hizo kwa wakati na kama zilivyokasimiwa.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakf, imekuwa ikikusanya fedha kutoka katika ada za huduma mbali mbali wanazotoa kama vile mirathi. Hata hivyo, fedha hizo hivi sasa zimepunguzwa kiwango chake na hicho kilichobaki kinakusanywa na *ZRB*. Hatua

hiyo imedhoofisha Kamisheni ya Wakf, ambayo imekuwa ikizitumia fedha hizo kutatua baadhi ya changamoto za kiofisi kama vile kufatilia mali za Wakf, mirathi zakka na sadaka. Shughuli hizo zote zinaweza kuzorota ufuatialiji wake iwapo fedha hizo zitaendelea kuingizwa katika mfumo wa serikali kupitia *ZRB*.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba sana Wizara ya Fedha, kufikiria upya makusanyo ya fedha za Mirathi, kuzibakisha kwa Kamisheni ya Wakf ili ziendelee kusaidia uendeshaji wa shughuli zao muhimu ambazo zinakwama kutoka na uingizwaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Hivi karibuni kumekuwa na mizozo mingi inayohusu mali za wakf na mirathi, na kupelekea hata mahakama zichukuwe hatu kali zidi ya wahusika ambao mara nyingi wamekuwa ni wana ndugu wa familia. Mnamo mwezi Febuari, mwaka 2015 kumeripotiwa katika vyombo vya habari hapa nchini, ikiwemo *ZBC*, kuhusu uamuzi wa Mahakama kuwafunga gerezani kwa muda wa wiki mbili wanafamilia wa familia moja maarufu nchini, kwa kupinga maamuzi ya mahakama kutoka na kesi ya Wakf iliyohusu wanandugu wa familia hiyo.

Mhe. Spika, Uwepo wa Kamisheni ya Wakf ulitegemewa matukio kama hayo yasiwepo au yasijitokeze katika hali kama hiyo, kwa vile Kamisheni inajukumu la kusimamia na kutoa elimu ya kutosha kwa jamii, kuhusu namna ya usimamizi wa mali za wakf na mirathi na kuweka dawati maalumu la ushauri wa kitaalamu kwa familia zinazokinzana, ili kabla ya familia hizo kufikisha mashauri yao mahakamani ziweze kwanza kupata ushauri kutoka kamisheni ya Wakf na ikishindikana ndiyo hatua nyengine zifuate. Kwa kufanya hivyo, Mhe. Spika, tutaweza kupunguza migogoro ya familia kuhusu mali za mirathi na wakf na kupunguza utitiri wa kesi katika mahakama zetu.

Mhe. Spika, Katika kufikia lengo la programu hii ndogo ya usimamizi wa masuala ya dini, Ofisi ya Mufti inajukumu kubwa la kuhakikisha kuwa jamii inaepukana na vitendo viovu na mpromoko wa maadili. Kamati yangu inashauri Ofisi ya Mufti kutambuwa jukumu lake na kusaidia kubainisha mambo mbali mbali katika jamii yanayosababisha mporomoko wa maadili kwa kushirikiana na miskiti na madrasa kuyakemea kwa nguvu zote na kuyaondoa.

Mhe. Spika, Aidha tunaitaka Serikali kushirikiana na Ofisi ya Mufti katika kuchukuwa hatua dhidi ya vitendo viovu vinavyochangia mporomoko wa maadili ya jamii yetu katika jamii. Sote tunatambuwa kuwa jamii yetu imejengeka katika maadili mazuri ya heshima na ustaarabu wa hali ya juu. Haitawezekana kuacha mporomoko wa maadili uendelee katika jamii kama vile hakuna mshughulikiaji, Ofisi ya Mufti ilibebe jukumu hili kwa nguvu zote na wananchi watowe

ushirikiano na Ofisi ya Muft, katika kupiga vita vitendo vyote vinavyopelekea mporoko wa maadili katika jamii bila ya kuona haya waka muhali.

Mhe. Spika, Katika programu kuu ya pili ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Sheria, jumla ya shilingi bilioni tatu, milioni kumi na mbili na tisini na mbili elf, (3,012,092,000) zimepangwa kwa uendeshaji wa programu ndogo za uongozi na uendeshaji wa Sekta ya Sheria, Mipango, Sera na Utafiti na Uendeshaji wa Wizara Pemba. Kamati haina tatizo na programu hii, isipokuwa tunasisitiza kuwa maslahi ya wafanyakazi wa Mahakama hasa kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo yatazamwe upya. Kamati yangu inashauri serikali kuharakisha sera ya malipo ili mahakimu wa mahakama za mwanzo nao wapatiwe nyongeza stahiki.

Mhe. Spika, kengo jipya la Wizara ya Katiba na Sheria, liliopo Mazizini limekamilika na tunaipongeza serikali kwa hatua ile kubwa ya kimaendeleo. Katika kukamilisha ujenzi ule bado kuna changamoto ndogo ndogo ambazo Mhe. Waziri amezieleza, na sisi kamati tunaisisitiza zitatuliwe hata kwa kubana vifungu ili jengo lile lihamiwe.

Mhe. Spika, Katika fungu G 02, la Mahakama Kuu, kuna programu kuu mbili. Programu ya kwanza ni usimamizi wa upatikanaji wa haki ambayo ina progamu ndogo moja ya usimamizi wa upatikanaji wa haki. Programu ya pili ni ya usimamizi wa shughuli za uendeshaji na utawala wa Mahakama, ambayo ina programu ndogo za uendeshaji na utawala wa Mahakama Unguja na uendeshaji wa shughuli za Mahakama Pemba.

Mhe. Spika, Programu zote hizo zimepangiwa jumla ya shilingi bilioni tano, milioni mia moja na arobaini na tatu na laki moja, (5,143,100,000). Kamati yangu imetazama vizuri programu ndogo ya pili ya kusimamia shughuli za Mahakama Pemba, ambayo imepangiwa shilingi bilioni moja, milioni mia tano na tisini na nne, laki tano na kumi na tisa elfu, (1,594,519,000) ambapo kamati imeona kuwa kiasi hiki cha fedha hakitawezesha kukamilisha hatua ya ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu, Chake Chake ambapo kwa mwaka huu wa fedha ilihitajika kiasi cha kutosha cha fedha ili kuwezesha kukamilika kwake. Kamati inataka kujuwa ni kiasi gani katika fedha hizi zilizotengwa kitaweza kufanikisha kukamilisha ukarabati wa jengo la mahakama ya Chake Chake.

Mhe. Spika, Kamati yangu imeshapiga kelele sana tokea bajeti ya mwaka jana 2014/2015 kuwa jengo la Mahakama ya Chake Chake Pemba lipo katika hali mbaya, wanaofanyaka kazi pale ni banaadamu wenzetu, wanastahiki kufanyakazi zao katika mazingira salama na sivyo Kama lilivyo hivi sasa.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilitegemea sana katika bajeti ya mwaka huu serikali ingeona umuhimu wa kuweka fedha za kutosha ili ukarabati wa jengo lile ukamilike. Kamati haijaridhika na kasma hii ndogo katika programu ndogo ya kusimamia shughuli za Mahakama Pemba, tunaitaka serikali kubana vifungu vya matumizi mengine na kusaidia kupatikana fedha ya kutosha, ili ukarabati wa Mahakama Pemba ukamilike.

Mhe. Spika, Katika fungu G 03, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, kuna progaramu kuu mbili ambazo zimetengewa jumla ya shilingi bilioni moja, milioni kumi na laki mbili (1,010,200,000). Kamati yangu imebaini changamoto kadhaa zinazokabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambazo zinaweza kuathiri utekelezaji wa programu hizo kwa kiwango hicho cha fedha kilichowekwa. Moja wa changamoto hizo ni uhaba wa fedha na kutoingizwa kwa fedha kwa mujibu wa maombi wa '*cash flow'* iliyopelekwa Wizara ya Fedha. Kamati yangu bado inasisitiza kuwa serikali izingatie sana umuhimu wa taasisi zinazosimamia haki, hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo inasimamia kesi zote za madai za serikali. Kamati inatanabahisha kuwa shughuli za Ofisi hii zinapokwama athari yake ni kubwa kwani serikali inaposhindwa kesi italazimika kulipa gharama kubwa za kesi hizo.

Mhe. Spika, changamoto nyengine kubwa ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ni kutopata ushirikiano wa kutosha kwa baadhi ya taasisi za serikali ambazo zimeshitakiwa Mahakamani. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekuwa ikifanya mawasiliano na taasisi hizo kuwatanabahisha juu ya athari za kutotoa ushirikiano, ambazo hupelekea serikali kushindwa kesi na kulipa fedha nyingi kama fidia.

Mhe. Spika, kamati yangu inaitaka serikali kutoka toleo kwa taasisi zote za serikali, kuhakisha kuwa kila taasisi ambayo ina kesi inayosimamiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuwapeleka maafisa wa sheria wa taasisi hizo kuripoti kila inapohitajika kwa mwanasheria Mkuu, na kuhakikisha kuwa ushauri unaotolewa na Mwanasheria Mkuu unafanyiwa kazi na maafisa hao kwa kushirikiana na wakuu wa taasisi hizo.

Mhe. Spika, aidha, tunaitaka serikali kutumia vyema sheria namba 3 ya mwaka 2010, sheria ya Mwenendo wa Mashitaka Dhidi ya Serikali, katika kifungu cha 7 cha sheria hiyo, kumuwajibisha afisa yoyote wa umma ambaye kwa uzembe wake atasabisha serikali ishindwe kesi mahakamani, ikiwemo kutotoa ushirikiano kwa Mwanasheria Mkuu, na kumtaka afisa huyo kulipa fidia ambayo serikali itatakiwa ilipe kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, katika fungu G04, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nayo imepangiwa programu kuu mbili za uendeshaji na usimamizi wa kesi za jinai, na mipango na uendeshaji ambazo kila moja ikiwa na programu ndogo mbili, jumla

yake ni shilingi bilioni moja , milioni mia sita na ishirini na saba na laki moja (1,627,100,000).

Mhe. Spika, programu zinazosimamiwa na ofisi hii ni kubwa, na kiwango cha fedha kinachoingiziwa hakilingani na ukubwa wa progamu hizo, ofisi hii inalazimika kufanya kazi zake kwa vile ni wajibu wake, lakini kamati tumeona kuwa inafanya kazi hizo katika hali ngumu.

Mhe. Spika, uendeshaji wa mashitika unataka ufanisi na ufanisi unatokana na matayarisho kwa waendesha mashitaka, kuimarishwa kwa maslahi yao ili kuwajenga nguvu na morali kwa kazi ngumu ya kupambana na wahalifu. Hivyo, kamati bado inarejesha kilio kwa serikali kuwatazama vizuri kimaslahi wanasheria wa *DPP*, ambao tunawetegemea sana kutuondolewa wezi, majambazi, wabakaji, matapeli n.k katika jamii, kwa kuthibitisha mashitaka yao mahakamani na kufungwa gerezani.

Mhe. Spika, tujiulize iwapo kama waendesha mashitaka hao, kama hawatafanya kazi hiyo kwa ufanisi, jamii yetu itakalika? Tusisahau kuwa kwa sababu hiyo tu, waendesha mashitaka wengi wenye uwezo mkubwa katika Ofisi ya *DPP*, wameshaacha kazi na kutafuta shughuli nyengine za kufanya. Kamati yangu bado inasisitiza tena kuwa serikai ione umuhimu wa vijana wetu hawa kuwaongezea maslahi yao ili tusiendelee kuwapoteza.

Mhe. Spika, mashitaka hayathibitiki mahakamani bila ya ushahidi, na ushahidi katika dunia ya leo siyo ule wa kuona kwa macho na kusikia, matendo mengi ya jinai yanayofanywa na wahalifu kama vile udhalilishaji na mauwaji, hufanyika kwa namna ambayo siyo macho wala masikio yanaweza kushuhudia, isipokuwa kwa vyombo maalumu ambavyo hutumika kushuhudia matokea ya jinai hizo. Mfano wa vyombo hivyo ni mashine ya vinasaba ya *DNA*.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine, kamati yangu inarejesha kilio chetu kwa serikali, kuhakikisha kuwa mashine ya *DNA* inapatikana ili Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, iweze kuthibitisha makosa hayo mahakama kwa njia za kitaalamu na kupatikana hatia kwa wahalifu. Sote tunafahamu hali ya vitendo vya udhalilishaji ilivyo nchini kwetu na namna tunavyokerwa na hali hiyo, kama ni hivyo basi, kamati yangu inaikumbusha serikali kuwa kama ilivyofanya kwenye mkakati wa ununuzi wa meli mpya ambayo karibuni itawasilia nchini na mkakati kama huo ufanyike ili mashine ya *DNA* ipatikane, hilo linawezekana tukitimiza wajibu wetu.

Mhe. Spika, kamati yangu pia inataka maelezo kutoka kwa Waziri, vipi bajeti ya *DPP* imezingatia upatikanaji wa jengo la kudumu kwa Afisi ya *DPP* kisiwani Pemba, pamoja na hatua za kumalizia ujenzi wa nyumba za waendesha mashitaka

Mkokotoni. Kamati inataka kujuwa ni vipi wizara kwa kushirikana na Wizara ya Fedha, itasaidia kupatakana fedha kwa ajili ya kukamisha ujenzi wa nyumba hizo, ili ule mpango wa kuendesha mashitaka kiraia uweze kuenea katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria, imepangiwa jumla ya shilingi milioni mia tano na ishirini na saba (527, 000,000), kwa ajili ya kuendesha programu kuu mbili za Mapitio ya Sheria na Utawala na Uendeshaji. Mafanikio makubwa yamepatikana tokea kuimarishwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria chini ya Mwenyekiti wake Jaji Mshibe Ali Bakari na Katibu wake ndugu Asma Jidawi. Kamati inawapongeza sana pamoja na watendaji wao wote na tunataka waendeleze juhudi za kuisaidia serikali kuwa na sheria nzuri zinazotekelezeka.

Mhe. Spika, nitumie fursa hii kuzitaka taasisi za serikali, ambazo zinafanya mapitio ya Sheria zao kwa nia ya kufanya marekebisho kushirikiana na tume, kwani wao ndiyo wenye jukumu la kisera na utaalamu kufanyakazi hiyo. Aidha, kamati inaipongeza Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kurejea kuwa mwanachama hai katika Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Afrika Mashariki na Kati (*ALRAESA*) na kufanikiwa kujiunga na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (*CALRAs*), pamoja na kuanzisha ushirikiano na taasisi mbali mbali za kimataifa zenye jukumu sawa na tume. Kamati yangu inaishauri tume kutumia vyema fursa hizo katika ngazi ya kimataifa, ili iweze kupata utaalamu na uzoefu katika kukabiliana na changamoto za maboresho ya sheria.

Mhe. Spika, kamati yangu ina mengi ya kueleza katika wizara hii, ambayo lazima nikiri tena kuwa imekuwa ikipokea na kutekeleza kwa vitendo ushauri wa kamati. Lakini kutokana na muda naomba nimalizie kwa kukushukuru na kuwashukuru wajumbe wako kwa utulivu wao wakati wote wa kuwasilisha muhtasari wa maoni haya ya kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nawaomba wajumbe tushirikiane katika kuichangia kwa kutoa ushauri, maelekezo na hatimaye kuipitisha ili Mhe. Waziri apate kutekeleza programu alizopangiwa katika bajeti hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, nikushukuru sana, lakini watu wengi sana huwa wanajiuliza, mbona wewe kila siku unakuwa wa mwanzo aidha, akiwepo Mhe. Spika. Nawaambia mwenyewe Mhe. Spika, anaona hali halisi ilivyo na mimi ameni- *train* vizuri ndio maana akaona aweze kunipa mara kwa mara mimi wa mwanzo. Watu hawajui undani wetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nianze kusema katika kitabu hiki na hasa wizara hii ambayo ndio yenye muhimili hasa katika Serikali Kuu. Mimi naona hata hizi bajeti zake zinakuwa zina kasoro za kuweza kukamilika katika utendaji wake wa kazi, ambapo ni kitu ambacho sio cha masihara sana, kwa sababu huu ni muhimili. Katika muhimili huu wananchi wapo wengi sana, lakini bado serikali haijataka kutizama kwa makini sana muhimili huu, kwa sababu tunauchezea chezea, maana yake tunasema katika muhimili huu bado hatujawa *serious* nao katika kuu- *handle* vizuri katika utekelezaji wake, ni kitu ambacho kina masikitiko makubwa sana.

Mhe. Spika, hebu twende kwenye Mahakama sasa. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 8 kuna kijisentesi kidogo tu hapa kinaeleza kuwa, mahakama ina jukumu la kusimamia utoaji wa haki. Sasa tuone *example*, Mhe. Mwenyekiti aliyeondoka alisema bado mahakama zinataka ziangaliwe kwa ufanisi kabisa, hasa katika mafao. Nikisema mafao watu wananifahamu, mafao ya mishahara. Kwa kweli Mhe. Spika, inasikitisha sana.

Mhe. Spika, haidhuru serikali imewasaidia katika Mahakama hizo Kuu, Mahakama za Mikoa. Naamini tayari imewatengenezea kidogo na hata vilio vyao sio vikubwa sana, lakini kwa kuwa pesa haitoshi ni haitoshi tu na hasa kwa kuwa zile kesi ambazo zime-*deal* na matajiri. Maana yake lazima tajiri atashtakiwa, tajiri atashtaki, pengine na mnyonge atakuwemo humo atashtakiwa na tajiri, pengine mnyonge atamshtaki tajiri. Lakini tunamuona pale saa zote anakaa Jaji kwenye kiti kama unavyochukua masaa wewe Mhe. Spika, pengine yeye anakuwa anapoteza lengo au ubongo kwa kufikiri kesi nyingi kwa muda mrefu. Halafu leo unakuja kumpa fedha ambayo haistahiki, asimpe tajiri anangoja nini, atampa tu tajiri, kesi ataifanya anavyotaka yeye mwenyewe. Wana ustadi kwa sababu wamesoma sheria, pengine sentensi ndogo sana inaweza ikamtoa tajiri au ikamtia hatiani tajiri au maskini ikamtoa au akaingia kwenye hatia.

Mhe. Spika, hili suala naomba sana tusiipe mzigo mkubwa sana, fedha tunazozitaja hapa ziendane na wakati. Siku moja hata ile karatasi walishindwa kuwa nayo na mimi nikisema jambo sisemi kwa kubuni, humu mote naranda, msifikirie nakwenda kwa kutia pozi, hapana. Nakwenda kwa lengo lakini ndani yake unapata.

Mhe. Spika, kuna makarani vile vile bado hatujawaangalia kimaslahi. Karani ndio mbaya zaidi kuliko Hakimu au Jaji mwenyewe. Anaweza akaficha faili akasema limepotea, Jaji asiseme chochote, inakuwa kazi keshapunguziwa anasema *Alhamdulillah*, anashukuru kuwa kazi imempungukia kwa upande mwengine, tayari ni jukumu kubwa lile.

Mhe. Spika, nao hebu tuangalieni nao maslahi hawa makarani, wapiga-*type* wale Sekeritarieti bado na hawa ni watu hatari sana hawa Mhe. Spika, tuache huyu

ambaye aliyesoma Jaji au Hakimu, tuangalie sana hawa kwa sababu ndio upotevu wa mambo yanaweza kutoka hapo ataweza kusema mimi Jaji fulani namjua bwana si yupo wapi pale ndio Mheshimiwa anaweza kutengeneza mambo basi akalificha tu lile faili kila likitafutwa halionekani. Nimuombe sana Mhe. Waziri tuwatizame sana hawa tuwe na ustadi wa kuweza kuwarekebishia mafao yao na wao waendapo wanasikitika Mheshimiwa, ukweli wanasikitika sana wana akili kikubwa na wao.

Sasa mimi ningeomba Mheshimiwa tuangalie nao kada hizi angalau tusidharau, hizi ni kada ambazo hatari sana katika utendaji wa kazi naomba sana hivi vilio mimi naamini mwaka kesho vitakwisha kwa sababu tayari tuna hii bajeti nzuri ya *PBB* itakwisha masuala kama haya, kwa sababu tayari tuna *special target* ya zile *projects* ambazo tumekusudia kuzipandisha mimi nafikiria hilo. Lakini kwa kukazia Mheshimiwa naomba sana kuangalia.

Mheshimiwa kuna hawa ma-*assessor* hawa mheshimiwa mpaka leo naamini si chini ya miezi sita au miezi saba pengine hawajalipwa naamini hivyo, hebu tujiulize sababu gani pengine Mheshimiwa Waziri hawezi kubania hizo fedha hajatiliwa fedha na wahusika, na tangu hapo pengine Waziri mwenyewe si msemaji, mnyonge masikini ya Mungu, hajui apenye wapi kwa sababu kuna wengine wanakuwa wajanja Mawaziri, ndio tunajua tena kila mtu anakula kutokana na urefu wa kamba yake. Lakini ni jmbo la kusikitisha sana ma- *assessor*, wazee wetu hawa utatoa haki vipi wakati huna hawa, utatoa haki vipi wakati hawa huwapi fedha kwa wakati na kwa mujibu wa taratibu, hichi kilio siku zote hebu tuwafikirieni jamani pesa yenyewe ndogo, kwanza pesa yenyewe inasikitisha Mhe. Spika, pesa ndogo inawachukua mtu miezi sita hawajalipwa wazee wetu masikini ya Mungu jamani. Mimi naomba sana waangaliwe wazee hawa, wana madeni, wana watoto wengine wanatoka mbali inabidi watumie nauli.

Mhe. Waziri hebu nisaidie hawa watu ni lini wataweza kulipwa hili deni lilokuwa la miezi sita au saba hawajalipwa mpaka leo. Niambie nikusaidie tatizo liko wapi, tatizo pesa hazijaingia kwa wakati au tatizo ni nini Mheshimiwa tukusaidie hapa ndio pahali pako. Kwa kweli ma- *assessor* wetu tunakuwa tunawavunja moyo, itatoka haki kweli hapa, atakwenda kuchukua rushwa tu hapa ndio tunaitengenezea rushwa *open* kabisa Mheshimiwa haina kimeme hapa, atamwambia wewe usijali yule wangu mwenyewe Jaji si nikimwambia ananisikiliza, basi mzee anachukua chake pale hatimae anakuja kufanya jambo liliokuwa sio zuri.
Hawafanyi hivyo lakini nadharia tunachukua kitu nadharia, na hata hakimu anaweza kukufunga kwa kuchukulia sheria nadharia nadharia pale anapoamua mwenyewe basi anaamua lile jambo analoweza kufanya yeye.

Mhe. Spika, Mahakama za mwanzo tumeshazisema sana, nimeisahau *Hansard* na ulisema hili suala utalichukulia jukumu katika kurekebisha mafao yao na wao,

hawa ndio wanaoanzia zile kesi za chini sasa katika ligi zetu zinazoanzia daraja za chini kabisa, daraja la kwanza, daraja la pili, daraja la tatu mpaka wanaingia katika timu kubwa huko daraja kubwa na zote zinatoa hukumu.

Mheshimiwa naomba sana tena basi umefika katika viwango ambavyo wanastahiki kimishahara wamefika *Diploma* wengine na mambo mengine ya kupindukia Mheshimiwa.

Mimi naomba sana nao hawa kwa kweli tuwafikirie *wallahi* tunawaonea huruma, tumeshasema sana wanaona choyo kwa wenziwao ila useme ukweli, pengine Jaji wa Mkoa naye kafika mpaka *Diploma* na wa Mahakama ya mwanzo naye kafika ile ile *Diploma*, akajitizama hana mshahara mwenzake ana mshahara mzuri. Hebu hii tuone sheria hizi saa nyengine inakuwa mimi nazitafuta sijui zinalingana na nchi gani, hapa kitu ambacho mimi kinanisumbua sana mimi niombe sana hilo suala.

Suala la marekebisho ya kutengeneza Mahakama zetu mmepiga hatua kubwa sana, hili nilipongeze sana, kwa kweli Mahakama zetu nyengine *Alhamdullillahi* zinaendana na wakati na hasa katika hali hii, mmejitahidi hapa nikushukuru sana kutokana na hali ambayo inastahiki kuwekwa shukurani.

Niende kwa Mwanasheria Mkuu, Mwanasheria Mkuu ana jukumu kubwa katika Serikali hii hasa katika maeneo ambayo ya kuingiliana masuala ya mikataba yeye ndio msimamizi mkuu na ndio shuhuda mkuu, lakini Mheshimiwa tunapokuelekezeni tunapokwambieni msije mkatujibu hoja zilizokuwa si za msingi, kwa sababu na sisi tunafuatilia, mimi ningekwambia suala moja tu sijui nani aliyesimamia kati ya wewe au mwengine suala la mkataba wa utekelezaji wa kazi ya uwanja wa ndege sasa sijui kama aliyepita au wewe.

Naomba uupitie tena upya mkataba ule kwa sababu umesainiwa wakati huku kampuni ya wazawa haijawa *registered*, sasa sijui sheria inasemaje hapa na sijui na wewe unaishauri nini Serikali, sijui utakuja kunambia nini hapa wakati tayari vitu vyote kwenye kichwa vimeshakaa.

Nakuomba sana Mheshimiwa hebu fuatilia kwa kina kabisa na hasa na muda wenyewe umeshakucha sasa hivi, ule muda wenyewe hasa ulikuwa umeshakwisha ya miezi sita imeshakwisha, sasa sijui Serikali utaiambia nini, utakuwa mzuri utakapoiongoza Serikali kwa mujibu wa sheria, kwa sababu sheria watu wote wanaangalia mpaka leo wajumbe wote wanasoma sheria hapa wote wana sheria zao wanasoma.

Sasa mimi ningekuomba sana tuwe waangalifu sana katika vitu kama hivi, kwa sababu tunafikia pahala Serikali tutaipeleka pabaya, Serikali itapigwa faini, serikali itatangazwa kwenye magazeti ya nje, haiwezekani sisi Serikali nzuri inasimamiwa na uangalifu mzuri wa Utawala bora mwenyewe Dkt. Shein, lazima tuwe *active* katika masuala kama haya.

Mimi naomba sana Mheshimiwa, naomba sana vitu katika sheria kwa sababu ndio fani yako Mheshimiwa, wewe si fani yako siasa kama mimi mpiga debe tutalingana tu, lakini mimi nina siasa na sheria ninazo hapo, na hapo kidogo kidogo nadokoa kwa sababu si mchovu wa kuuliza sheria, na utaona huko mbele mimi nitakavyoweka sheria nitakavyokuonesha sheria inatakiwa ufanye vipi nitafika huko mbele ya safari.

Mheshimiwa naomba sana kitu kama hichi nilikuwa najiuliza sana kwenye Baraza hili Mwanasheria nini kazi yake, lakini kumbe *simple* tu Mheshimiwa nimegundua suala hilo nikaona *alhamdullillahi* basi mwenzangu niweze kumuongoza, kuwa muongozo wako hasa katika Baraza hili kusimamia sheria. Naendelea Mheshimiwa hili nimeona kidogo niweze kumshutua na niweze kufamfahamisha hali halisi ilivyo.

Nikiingia Mkurugenzi wa Mashtaka ukurasa wa 16. Mwenyekiti wangu alisema wimbi kubwa limewakumba sasa hivi wanaondoka na kweli wanakwenda katika sehemu kubwa wanachukuliwa sehemu mbali mbali Mheshimiwa ambako kule tayari wanapata mishahara mikubwa ambayo ni mizuri, ndio maana utakuta kesi nyingi sana zinakwama Mheshimiwa kutokana na hali halisi ya uchovu, ya ufuatiliaji sasa hapa mimi naomba sana Mheshimiwa nitoe ushauri wangu wa kina kabisa, ili kufanikisha suala ambalo kubwa sana hata Mhe. Rais Dkt. Shein alilipigia kelele sana suala hili.

Vitu viwili kama havikukaa pamoja Polisi na hawa waendesha mashitaka basi kila siku Polisi watakuwa hawana ushahidi wanaopeleka pale, kabisa hivi vitu lazima washuke wakae pamoja, ili kwa kupeana maarifa, kwa sababu na hawa wanaoendesha mashtaka washuke chini ili kuweza kukamilisha na wao ushahidi, lakini kwa kukaa kama golikipa tu itakuwa kila siku hakuna kesi zinazopelekwa pale, kwa sababu muendesha mashitaka ataangalia eneo ambalo linamuhusu yeye hataweza kutiwa hatiani kwa sababu kapelekewa. Lakini wakishuka chini pamoja na polisi basi sidhani kama hakuna kitu ambacho watakuwa wanarembewa mara kwa mara polisi nenda rudi karekebishe hichi, katengeneze hichi, naomba sana na hasa katika kesi za ubakaji.

Mhe. Spika, kesi za ubakaji kila siku zitakuwa nenda rudi polisi nenda rudi hizi kesi tuziweke *special* kesi Mheshimiwa, lazima wakae timu, wazo zuri sana lazima

wakae timu, watakapokaa timu tutafanikiwa. Mheshimiwa wanatamba hawa akina vitangi kwa sababu wameshaona hii *weakness* zilipo hapa, wanajua hilo, anajua wazi mimi nikipelekwa kwa Muendesha mashitaka anajua wazi hii ataikataa tu, tizama anavyojipa moyo keshaona na keshadomasa si ndio sisi waendesha mashitaka tunakaa pamoja.

Sasa mimi ningeomba ushauri wangu wa bure kabisa Mhe. Spika, kuwa hawa watu lazima wakae pamoja kwa kesi kama hizi wakae *team work, wallahi* Mheshimiwa tutafanikisha tutawakomesha hawa watu, lakini kwa misingi hii tutajidanganya Mhe. Spika, na tutapiga kelele.

Rais ataunda tume zaidi ya hamsini lakini haliwi Mheshimiwa. Lakini pamoja na hayo Mheshimiwa mimi nilisema kipindi kilichopita lakini leo Mwenyekiti wangu kanisaidia hii mashine ya *DNA*.

Mimi nataka kuuliza Mheshimiwa hebu njoo uniambie kiasi gani hii mashine iwashinde, pengine mimi nitakuwa na uwezo ninaweza kuinunua. Hebu naomba sana Mhe. Waziri mara hii utakapokuja kunijibu njoo uniambie *cost* yake kiasi gani, kweli Mhe. Spika, nina uwezo mimi wa kukopa benki nitafanyiwa tathmini, lakini siku zenyewe zimeisha nimesahau Mheshimiwa kumbe siku zimeisha, ingekuwa siku hazijaisha ningesema mimi nikatwe kidogo kidogo kwa sababu mashine hii ni moja katika kusaidia ushahidi. Lakini kila siku Mheshimiwa tunaimba tunaimba tatizo liko wapi, Mhe. Waziri njoo unieleze tatizo liko wapi mashine hii haipatikani. *Alhamdullillahi*, mimi naamini hatujataka, na kwa sababu hatujataka Mwenyezi Mungu akuepushieni mbali hajabakwa mtoto wa Waziri, akibakwa mtoto wa waziri au Mheshimiwa hapa *wallahi* mashine itanunuliwa *immediately* kabisa.

Tatizo lenyewe wanabakwa watoto wa wanyonge, masikini ya Mungu, wavuja jasho wanadhalilishwa watoto wao wanaharibiwa, si mwanamme si mwanamke.

Kweli leo mashine hii inakuwa nyimbo ya Taifa kila siku Mungu aibariki Zanzibar, kila siku tunaimba hivyo hivyo kwa kimashine hiki kidogo tu, ambacho hata mfukoni hakiingii. Hebu tuangalieni jamani tunakosa ushahidi wa kisheria kwa sababu hii mashine haisemi uongo.

Mimi ningeomba sana hivi kweli tushindwe hii hali kwa kweli inasikitisha sana. Mashine ndogo sana ndani ya mfuko haingii halafu leo tunashindwa, mimi naomba sana ni suala ambalo linanisikitisha sana, tena sana.

Sasa mimi ningeomba tuone wapi inakwamishwa hata ikabidi tushindwe kuipata, tuko *serious* kweli mara ile iliyopita nilipanga *plan* mimi nilisema si vibaya

tukafanya harambee, hakuna watu watakaokataa kwa suala hilo, mimi naamini wako watu watakubali Mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Tumia dakika tano kumaliza hotuba yako.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mheshimiwa watu wanaweza wakatusaidia wafanya biashara wapo, mabenki yapo, kwa nini tushindwe kuipata mashine hii, tusione haya. Mimi tatizo letu nasema tusione haya tuwe katika hali ambayo tunaweza kufanya kitu hicho tuiteni, hebu nichaguliwe mimi Mwenyekiti uone kama suala kama hilo kama haitopatikana mashine pengine wiki moja tu haki ya Mungu nakwambia.

Hebu na leo Dkt. Shein simuombi kwa sababu namuomba kwa uchungu, nichaguliwe Mwenyekiti wa harambee wa kutafuta mashine hii ya *DNA* uone kama mimi sijaipata, tutaipata tu mashine kwa nini tusiipate, lakini mimi inanisikitisha sana.

Mheshimiwa katika kutumia dakika zangu tano niingie katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Sheria sasa hivi kweli zimepitwa na wakati, nitatoa *examples* mbili; sheria ya ubakaji ni mtu mzima anakwenda kumbaka mdogo lakini yule mtu mwenyewe kidogo na akili zake ndio tuseme hajaugua lakini pale unapomfanyia kile kitendo ndio anapata kuugua, imekuwa sheria ya miaka thalathini au kifungo cha maisha, lakini kuna sheria hii inaeleza tena kuwa wagonjwa wa akili wanaoingiliwa acha miaka kumi na nne hii sheria iko wapi hii, imeshapitwa na wakati Mheshimiwa, huyu mtu ni wa kunyongwa kwa sababu kaenda kamuingia mtu ambaye mgonjwa *times three* ni mgonjwa wa akili, unakwenda kumuongeza na magonjwa mengine hii Mheshimiwa hakuna sumile, hawa Tume hawa wanafanya kazi nzuri lakini hamuwawezeshi, tatizo hamuwawezeshi tu.

Kwa sababu watunga sheria na wananchi wanatakiwa, kwa sababu kila siku tuna-*quote,* tunakuwa tuna-*quote* sheria ya Mainland, Kenya, au Nairobi na sisi tunataka kutoa *new* sheria zetu wenyewe kwa kupitia wananchi wetu ni moja hili Mheshimiwa, au mtu anakwenda katika sheria hii anaitwa zuzu, hivi kweli binadamu unakwenda kumuita zuzu, kweli kwenye jamii inaingia hiyo, hii *total* kabisa kwenye haki za binadamu sheria hii imepitwa na wakati, asilimia 99 imepitwa na wakati.

Ningeomba sana Mheshimiwa sasa hapa pawe *exchange,* hapa huyu mtu anayefanya hivi Mheshimiwa anyongwe au afungwe maisha kabisa, sio miaka kumi na nne. Tunaona wanawazalisha watoto wale wanaopita na njia, wendawazimu wanawake wale wagonjwa wa akili wanavyotiwa mimba, kama yule wewe si unakwenda kumtia nakama ee mtu mzima na akili yake anavyobeba ile

mimba hali kadhalika mnamuona hali yake, je yule leo hatujui. Mheshimiwa hii sheria mimi naomba sana hii sheria nitakuja kulia sana huko mbele kwa sababu hapa walemavu wanawaonea.

Mhe. Spika, nimalizie naamini Serikali imeshajua na ishasikia nini *target* ya Tume hii. Tume hii iwezeshwe, ipewe *funds* iweze kufanya kazi zake, ishuke chini ili iweze kusikia wananchi maoni yao na kuweza kutengeneza sheria zilizokuwa za msingi.

Nimalizie nimshukuru sana Mheshimiwa Mkurugenzi wa Hati Miliki. Mheshimiwa watu ni wezi kama alivyosema hapa mtu ambaye ameiba, lakini sheria imempa yeye yule aliyekwiba.

Mkuruganzi anajitahidi sana katika kipindi cha nyuma alipata vitisho vikubwa sana katika masuala ya kufuatilia kuwatetea wanyonge ambao wame- *resist* kwa mujibu wa sheria, sasa nimpongeze sana jitihada hizi aendelee asichoke, kwa sababu ndio utamaduni wetu wa Zanzibar hapa utamaduni mwengine inakuwa hatujauzoea lakini mwengine tunakuwa tunauzoea.

Kwa hivyo atufanyie subra, astahamili na aondoshe ujasiri wake ule ule ambao alitoka nao nyuma asiogope vitisho, na kesi kama hizi aendelee kutafuta sheria njia nyengine kwa sababu kuna Mahakama ikiwa ya Mwanzo nenda kwenye Wilaya, ukitoka Wilaya nenda Mkoa mpaka atafika pahali atashinda kwa uwezo aliompa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, niseme niwaombe sana ndugu zangu bajeti hii tuipitishe kwa nguvu zote, lakini muhimu tusimame katika vifungu ambavyo tunavyovisema ndio inayoleta usimamizi mzuri katika Serikali yetu.

Mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia na wengine waje kuunga mkono kwa asilimia hiyo. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kupata nafasi na kutoa machache niliyonayo kuhusu Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mhe.Spika, kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wanaomsaidia katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, hasa wale waliomsaidia kutunga kitabu hiki cha bajeti ya mwaka huu 2015/2016 wamefanya kazi nzuri na inafaa kupongezwa kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye Mahakama, Mahakama Mhe. Waziri kasema ni chombo cha kusimamia utoaji wa haki, Mhe. Spika, miaka ya nyuma Mhe. Waziri tulisoma pamoja na tulifanya *debate* iliyokuwa na maana inayosema *'Mercy should be set aside so to maintain justice'*, Mhe. Waziri kwa wakati huo alikuwa ni mwanafunzi na yeye alikuwa ni *Principal Speaker* ku-*oppose motion hii*, kwa sababu *motion* inakuwa siku zote wanaounga mkono na wanaoipinga, yeye alikuwa ni msemaji wa kuipinga hii. Bahati nzuri pamoja na uzuri wake huo wale walioipinga mada hii ndio walioshinda, kwa sababu zao walizotoa majaji wakaona kuwa wapinzani walikuwa na hoja nyingi zaidi kuliko waliounga mkono hoja hii.

Mhe. Spika, nimetoa hii kwa sababu gani, kwa *mercy should set aside so as to maintain justice.* Ili haki itendeke lazima huruma na mengine tuyaweke kando. Je, Mahakama zetu ziko hivyo, katika kusimamia haki huruma wameziweka kando. Je, katika kufanya haki hakuna upendeleo wowote. Je, katika kusimamia haki hakuna harufu ya rushwa katika Mahakama zetu. Ikiwa haya yapo basi bado huu usimamizi wa haki uliotajwa utakuwa bado haujafikiwa. Ili haki ifikiwe katika Mahakama ni lazima haya yatendeke.

Mhe. Spika, Jaji Mkuu wa mwanzo wa Tanzania alikuwa ni mgeni sio wa Zanzibar, wa Tanzania, nadhani alikuwa ni mtu kutoka Burma na alikuja kule Fidel- Castro kuzungumza na wanafunzi mimi nilikuwa nipo na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alikuwa yupo.Yule Jaji katika maelezo yake mengi alisema Mahakama haitafuti *who is guilty,*inatafuta nani kajua kujieleza vizuri. Ina maana inaweza kuwa una makosa lakini ukaja kujieleza makosa yakakuvuka. Inaweza ukawa hukukosea lakini ukashindwa kujielezea Mahakamani, kosa likakuandama. Sijui wenzetu Mahakimu na Majaji wana vigezo gani vya kujua kwamba maelezo haya ni sahihi na maelezo haya ni ya kupanga.

Mhe. Spika, ndio maana baadhi ya watu wanapokuwa na kesi wanalazimika kuweka mawakili. Hawa wanasheria ni watu wazuri sana lakini na wao wana hatari zake. Kwa sababu mara nyengine wanamsimamia mtu aliyekuwa kafanya kosa ili wamvue kosa, hili ni tatizo. Lakini kwa sababu lipo kisheria tuseme halina matatizo kwa sababu sheria inaruhusu.

Mhe. Spika, kitabu kimeeleza kuwa kesi za Mahakama Kuu mpya ni 163 na kulikuwa na kongwe 116, kwa hiyo jumla ya kesi zilizokuwepo Mahakama Kuu kuwa ni 279 na wamesema ni masuala manne tu yaliyotolewa uamuzi.

Mhe. Spika, katika mashauri hayo 279, yaliyotolewa uamuzi yakiwa ni mashauri manne tu bado ni machache mno. Pamoja na kuwa ni jambo la kisheria, lakini huu mwenendo wao ya kuwa katika kipindi chote hicho ni mashauri manne tu ndiyo

yaliyopatiwa uamuzi, sijui wanakwenda katika mwendo gani mpaka ikawa ni hivyo tu.

Katika Mahakama hii hii kuna *division* ya Mahakama ya Kadhi ambayo kuna mashauri karibu 18 lakini hakuna shauri hata moja lililopatiwa uamuzi katika Mahakama ya Kadhi. Kwa hivyo hapa Mhe. Spika, inaonesha huu mwendo wa kutoa uamuzi wa Mahakama ni mwendo wa kudorora mno.

Mhe. Spika, ukiacha Mahakama Kuu, Mhe. Waziri kasema kuwa mashauri yalipotolewa katika Mahakama za Mkoa ni mapya 221, makongwe yalikuwa ni 316, kufanya jumla ya 537wakati ambao yaliyotolewa maamuzi ni mashauri 47 tu. Mashauri 490 bado hayajatolewa maamuzi. Bado upo ule upole wa kutolea maamuzi katika Mahakama zetu. Kadhalika katika Mahakama za Wilaya kwa jumla zipo kesi 4863, zilizopata maamuni ni kesi 1865 bado kuna uzorotaji wa kupata maamuzi.

Mhe. Spika, pia Mhe. Waziri kaeleza kwenye Mahakama za mwanzo kuna mashauri mapya 2783, makongwe ni 2602 yote 5385 yaliyopata maamuzi ni 2448, bado katika Mahakama zetu mwendo wa kutoa hukumu unakwenda pole pole.

Mhe. Spika, kasema kuna Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, mashauri hapa mapya ni 37, makongwe ni 38 yote 75, lakini katika jumla ya Mhe. Waziri yameonekana kama ni 72 inawezekana kuwa mimi nimekosea au yeye kakosea, lakini yametajwa kuwa ni 37 na 38, Na hapa yaliyopatiwa maamuzi ni 17 yaliyobaki bado hayajapatiwa maamuzi.

Mhe. Spika, inaonesha kwamba mwendo wa Mahakama zetu ni mwendo wa kinyonga, ni mwendo wa pole pole mno. Kadhalika Mhe. Spika, kuna Mahakama ya Rufaa ya Tanzania nafikiri itakuwa kanda ya Zanzibar hii, wamepokea mashauri mapya 6, yalikuwepo makongwe 10 yote yakawa 16, mashauri 6 yametolewa maamuzi.

Mhe. Spika kuna Mahakama ya watoto ambayo imeanza karibuni sana, ambayo ina mashauri mapya 28, makongwe 23 yote ni 51 yaliyopata maamuzi ni 9. Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa ufupi nilikuwa naonesha jinsi Mahakama zetu zinavyokwenda pole pole katika kutoa maamuzi.

Sasa mimi nilipofanya majumuisho ya mashauri yote haya nimetofautiana pakubwa sana na Wizara. Ningeomba Wizara kama mimi nimekosea au sijui kwa sababu ni mambo ya kisheria, ningeomba wanielekeze.

Wizara kwa ujumla mashauri yote haya wameyafanya ni 6783, lakini mimi nimeyaona kuwa ni 11,236 kwa kweli tumetofautiana pakubwa sana, ama itakuwa kwa sababu ni jambo la kisheria na Kimahakama sijui. Ningeomba nielekezwe ili nami nifahamu vizuri. Ni kesi nyingi zaidi kuliko zile ambazo bado hazijapata maamuzi. Lakini kwa hesabu yangu mimi ilotolewa maamuzi *just* asilimia 39 na asilimia 60.9 bado hazijapata maamuzi. Lakini hili nasema inawezakuwa mimi kwa sababu mambo ya kisheria siyajui inaweza ikawa mimi ndiyo niliyekosa kufahamu huu mpangilio wenyewe.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye Mahakama niende kidogo katika Ofisi ya Mufti. Ofisi hii imeelezwa hapa kuwa; nichukue sentensi ya mwanzo mwisho huku,

- Kufanya ziara za Misikiti na vyuo vya *Qur-an*,
- Kujibu maswali ya wananchi,
- Kutatua migogoro ya kidini pamoja na kuhamasisha amani na utulivu.

Mhe. Spika, niipongeze hii Ofisi kwa kujaribu kuvitembelea hivi vyuo vya *Qur-an* pamoja na misikiti na kujaribu kutatua migogoro ya kidini. Kwa sababu dini inapokuwa na migogoro hata kuabudu kwetu itakuwa kuna migogoro hivyo hivyo. Kwa hivyo niwapongeze kwa kuchukua juhudi hizo za kujaribu kutatua migogoro ya kidini inayojitokeza. Hata baadhi ya wakati migogoro hiyo inatoka ama katika vyuo au misikiti. Kwa hivyo ni wajibu wa taasisi hii kwa kuwa ni ya kidini kusimamia matatizo hayo yasijitokeze.

Mhe. Spika, kifungu cha 60 Mhe. Waziri wa Katiba, kasema jumla ya fomu 215 za mikisiti na 215 za madrasa zimesambazwa na fomu 158 za Misikiti na Vyuo zimerejeshwa kupitia fomu hizo jumla ya Misikiti 1018 na Madrasa 1079 zimetambuliwa.

Sasa nataka kujua hapa Mhe. Spika, fomu moja inasajili zaidi ya Msikiti mmoja au Chuo kimoja. Kwa sababu fomu zilizotolewa ni chache lakini Misikiti na Vyuo vilivyotambuliwa ni vingi kuliko fomu zilizotolewa, Kama fomu moja inasajili zaidi ya mmoja ni sawa, lakini kama si zaidi ya mmoja ningependa nipate maelezo ilikuwaje fomu zikawa kidogo lakini Taasisi zilizotambuliwa za vyuo na Misikiti ikawa ni mingi zaidi.

Halafu paragrafu ya 61 kuna sentensi inayosema; aidha taasisi imepokea migogoro minne ya misitikiti na mmoja wa Madrasa, kati ya migogoro hiyo migogoro saba imepata ufumbuzi. Migogoro ya ndoa 83 imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, nilikusudia kugusia hii migogoro ya ndoa. Mhe. Spika, tunapenda sana kuoa. Ingawa dini imeanzia wawili, watatu, wanne na kama mtu hajimudu

katika mambo mengine hata mmoja. Lakini wengi tunaoa lakini sheria ya ndoa hatuijui. Watu wanaoa tu siku mbili tatu wanampa *red card* kwa matatizo madogo madogo. Hii ni kwa sababu hatukusoma au hatuijui dini yetu juu ya hii ndoa.

Mhe. Spika, kuacha ni sheria au ni haki lakini ni jambo ambalo Mwenyezi Mungu analichukia. Sasa sisi tunaoa leo kesho tunaacha, kesho tunaoa mwengine, tunabadilisha kama tunavyobadilisha shati au kanzu zetu. Ningeomba Ofisi hii kwa hivyo itoe mafunzo au taaluma kwa waoaji jinsi ya kukaa na kuishi na wake waliowaoa.

Mhe. Spika, sasa hivi kwenda kijana akataka mke na kwenda mimi *baby* nikataka mke, naweza nikampata mimi kuliko kijana. Kwa sababu pengine naonekana mimi niliyesogea kidogo kiumri mimi nina maarifa, nina na hekma ya kuishi naye, yule anayevaa suruali ya kuning'inia wakati wowote anaweza akatoa maamuzi yasiyofaa. Kwa hivyo taasisi hii Mhe. Spika, ni vyema ikatoa mafunzo kwa sisi waoaji juu ya kuoa na kuishi na wake tuliowaoa, kuliko mara kwa mara kutoa talaka ambazo hazina msingi.

Mhe. Spika, kwa kuwa Ofisi hii inasimamia talaka, ndoa na mirathi ni lazima wajitahidi katika mambo haya kutenda haki. Taasisi hii imeingizwa katika serikali na katika kitabu lakini hii ni Taasisi ya Kidini, hukumu zake zote lazima iendane na matakwa ya dini ya Kiisalamu inavyotaka. Kwa hivyo wakimdhulumu mtu katika ndoa, kumpa mtu mke pengine waliachana, sheria haimpi tena. Wasimrithishe mtu mali ambapo hana haki.

Mhe. Spika, nina mfano wa kutoka mahala fulani. Mtu alimuacha mkewe lakini bado anamtaka. Mwanamme akaenda kufungua shauri Mahakama ya Kadhi alilolifanya ni kwenda kusema kwamba huyu mimi sijamuacha. Mwanamke akasema uliniacha, akamwambia sikiliza Mhe. Kadhi, huyu tulikuwa tunagombana, kwenye kugombana nilimkamata, nilipomkamata akadai nimwachie. Nikamwambia haya nimeshakuacha, lakini ilikuwa kuacha hii siyo ya talaka, ilikuwa niache kwa sababu nilikuwa nimemkamata. (*Makofi*).

Mhe. Spika, huyu mume unaona Mhe. Spika, alivyopinga ili apate mke ambaye tayari kaachika. Lakini sasa Hakimu anahukumu yale ambayo tunayatamka, nia zetu hazijui. Kwa hivyo akamwambia kama ni hivyo bado ni mkeo, akatoka naye bwana lakini kumbe alikuwa kampa talaka hasa, lakini kwa sababu anamtaka akajenga hoja ya aina hii. Mhe. Spika, kwa hivyo Ofisi hizi zina dhima na lazima tunapokuwa na matatizo waweze kutuhoji kiasi cha kutosha ili watoe hukumu ambazo zinastahiki.

Mhe. Spika, niende katika Mrajis wa Vizazi na Vifo, hapo imeoneshwa vizazi zilivyopatikana katika kipindi hicho wanaume na wanawake. Hapa mara hii wanaume wamezaliwa wengi zaidi kuliko wanawake, lakini pia wanaume wamekufa wengi zaidi kuliko wanawake vile vile, kutokana na wale waliosajiliwa.

Mhe. Spika, hapa nilitaka kutoa ushauri au kuiomba Ofisi hii kutuelimisha juu ya kukitafuta kile cheti cha kifo. Mara nyingi tumehamasika kutafuta cheti cha kuzaliwa, lakini bado hatujatoa uzito unaostahiki juu ya pale ambapo mtu kafariki kutafuta kile cheti cha kufariki kwake, tena mtu keshakufa tunaona cheti kina maana gani. Kumbe serikali inarikodi zake inataka kujua. Hili hatulitilii maanani. Kwa hivyo ningeomba watoe elimu ya kutosha ya kutuelekeza kuona hichi cheti cha kifo nacho kina umuhimu wake.

Mhe. Spika, mara nyengine inatokezea mtoto yatima kuna msaada maalum anataka kuupata, lakini taasisi husika itataka ushahidi kupata cheti cha kifo cha baba yake, kama cheti hicho hakipo taasisi ile inaweza isiamini kuwa huyu mtoto ni yatima. Kwa hivyo msaada uliokusudiwa unaweza ukakosekana kwa sababu waliopo baada ya kufa baba hawakuandika kile cheti cha kifo. Kwa hivyo ningeomba elimu itolewe tuhamasishwe kuona pale mtu alipofariki uko umuhimu wa cheti hiki kupatikana nacho.

Halafu Mhe. Spika, juu ya vyeti vya wale ambao watu waliochelewa kuchukua vyeti baada ya kuzaliwa *late registration* hawa, hawa Mhe. Spika, wanapata usumbufu mkubwa na hata ile ada yao kidogo ni kubwa. Ningeomba wizara ipunguze kidogo urasimu uliopo na pia ipunguze ile ada ya hiki chetu, ili watu wengi wenye umri huo wanaohitaji vyeti waweze kuvipata kwa wakati kama wanavyopata wale ambao wamepata kwa wakati unaostahiki.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache niseme kuwa naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kutujaalia asubuhi hii kuwepo katika Baraza lako hili ili kuendeleza majukumu yetu ya kuisimamia Serikali na kuwatetea wananchi ambao wanatusikiliza.

La pili, nachukua nafasi ya kukushukuru kunipa nafasi ya angalau na mimi kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

La tatu, katika utangulizi wangu ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria juu ya uwasilishaji wake wa ripoti hii kwa ufasaha na kwa utulivu wa hali ya juu.

Pia niwapongeze watendaji wake wote wa Wizara kwa sababu wao ndio waliochangia kwa kiasi kikubwa Mhe. Waziri kusimama mbele yetu na kueleza yale yote ambayo yapo katika Taasisi zake za Wizara ya Katiba na Sheria.

Mbali ya utangulizi huo Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika kitabu kilichopo mbele yetu ukurasa wa 8 kifungu cha 24 naomba Mhe. Spika, ninukuu:

"Mhe. Spika, katika kipindi hicho Mahkama Kuu imepokea mashauri mapya 163 ukijumuisha na mashauri 116 imekuwa na jumla ya mashauri 279 mashauri manne yametolewa uamuzi. Katika divisheni ya Mahkama ya Kazi yamepokelewa mashauri mapya 11 na kuifanya divisheni hiyo iwe na mashauri 18 kwa kujumuisha mashauri 7 yaliyosajiliwa kabla. Hakuna mashauri yaliyotolewa maamuzi katika mahkama hiyo".

Mhe. Spika, kwanza niungane na Mhe. Haji Khalid katika kuzungumzia ule mrundikano wa kesi ambazo zinakosa maamuzi kwa wakati na kuchelewa sana. Lakini kwa kutaka kufupisha muda niseme kwamba katika Divisheni ya Mahkama ya Kazi kuna mashauri 18, lakini hakuna hata shauri moja ambalo limetolewa maamuzi na Mahkama hiyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri ni kikwazo gani katika Mahkama hii ya Kazi ambayo inarundika kesi na mashauri yanachelewa kutolewa katika hali hii.

Tunajua kwamba kuna Mahkama hii ya Kazi ambayo kuna wafanyakazi mbali mbali wana haki zao, wana taratibu zao lakini bado Mahkama hii imeshindwa kutoa maamuzi ya kesi yoyote katika kesi hizi ambazo ziko mbele ya Mahkama hii.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 12 kifungu cha 40. Mhe. Spika, naomba ninukuu:

"Afisi ya Mwanasheria Mkuu imekusanya na kuyaweka pamoja Magazeti Rasmi ya Serikali kuanzia mwaka 1910 hadi mwaka 1955 kazi hiyo inaendelea na lengo ni kukusanya Magazeti Rasmi hadi kufikia mwaka 1963".

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na ni jambo ambalo litaifanya Afisi ya Mwananasheria Mkuu kuwa na kumbukumbu halisi za tokea miaka na karne zilizopita. Mheshimiwa ninaiomba Afisi hii iendelee na juhudi hii ili kukipakizazi chetu kinachokuwepo na kinachoendelea kumbukumbu za kujua mambo tofauti yaliyokuwepo kabla na yanayoendelea sasa. Kwa kweli ukusanyaji wa kumbukumbu za tokea 2010 mpaka 1955 kwamba hizi tayari kumbukumbu zipo ni jambo zuri nani jambo ambalo linastahiki Afisi hii kupongezwa sana.

Wito wangu kwa Afisi hii kumbukumbu hizi wazitunze vyema ili kusije kukatokea mambo ya kupotea potea kumbukumbu hizi, kumbukumbu ni muhimu sana. Kuna watu wametoka katika maeneo ya mbali wazazi wao wameishi katika maeneo mengine, lakini kwa sababu ya kumbukumbu wakarudia katika vyanzo vyao vya asili na wamemiliki mali nyingi kwa sababu ya kumbukumbu ambazo waliekewa na wazazi wao.

Mhe. Spika, niseme kwamba uwekaji wa kumbukumbu ni jambo muhimu na kwa kweli niseme kwamba Ofisi imefanya jambo zuri lakini ingeundwa kamati hasa ya kushughulikia suala hili, ili likapatikana uharaka zaidi kwa sababu wana azma ya kukusanya mpaka 1963 na hapa wamekusanya mpaka 1955 kwa hivyo kuna miaka kadhaa hapo ambayo hawajazikusanya kumbukumbu hizo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 19 kifungu cha 60. Mhe. Spika, naomba ninukuu:

"Mhe. Spika, katika juhudi za kupata takwimu sahihi za misikiti na vyuo vya *Qur-an* Afisi ya Mufti imeweka utaratibu wa kugawa fomu kwa masheha kupitia kwa Wakuu wa Wilaya ili wazijaze. Jumla ya fomu 215 za misikiti na 215 za madrasa zimesambazwa na fomu 159 za misikiti na madrasa zimerejeshwa".

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba tuna misikiti mingi, tuna madrasa nyingi sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa kweli niseme kwamba fomu zilizotolewa ni kidogo sana, 215 kwa misikiti, 215 kwa madrasa hizi ni fomu kidogo sana. Lakini nimuombe Mhe. Waziri atoe yaani Wizara yake itoe taaluma tosha juu ya walimu wa madrasa pamoja na mashekhe na maimamu wa misikiti juu ya uchukuaji wa fomu hizi. Inawezekana kuna baadhi ya maeneo fomu hizi zipo, lakini walimu pamoja na maimamu wa misikiti hawaelewi chochote katika hiki ambacho kinaendelea. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. atoe taaluma ya kutosha juu ya umuhimu wa kukusanya kumbukumbu za misikiti na madrasa.

Kwa kuwa nchi yetu imekuwa na misikiti na madrasa nyingi, ni vyema Ofisi yetu kujua takwimu sahihi ya misikiti na madrasa yanapotokea matatizo au migogoro katika misikiti au vyuo inakuwa ni urahisi sana kujua kwamba chuo hiki kiko pahali fulani bila ya kuuliza maswali mengi kwa sababu fomu zake zitakuwa zipo katika masuala mazima ya Ofisi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika kifungu cha 61 na hapa naomba ninukuu.

"...aidha migogoro ya ndoa 83 imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi"

Mhe. Spika, nataka nizungumzie masuala haya yanayohusiana na ndoa na kuhusiana na suala zima la Ofisi ya Kadhi au Ofisi ya Mufti. Mhe. Spika, kunakuwa na malalamiko mengi kwa waislamu kutokana na kulalamikiwa masuala haya ya ndoa. Kuna baadhi ya mahakimu wetu katika Ofisi za Kadhi ninafikiri wanakuwa wanalalamikiwa kwamba kesi wanaziangalia kwa upande mmoja, hawaziangalii kwa upande mwengine na kutolewa fatua hasa kesi hizi za ndoa na hasa za talaka, kwamba watu wanaachwa ovyo ovyo bila ya kuangalia ushahidi wa kina.

Kwa hivyo Ofisi kama hizi kulalamikiwa na wananchi katika masuala haya inakuwa kwa kweli haipendezi hata kidogo. Kwa hivyo ninaiomba Ofisi ijitahidi, wizara kutoa taaluma kwa wale wanaoshtakiana ili inapotolewa fatwa au inapotolewa hukumu basi hukumu ile ni ya usawa, iwe ni ya uadililifu, iwe ni ya haki.

Jengine ambalo napenda nilizungumze hapa Mhe. Spika, linahusiana na suala zima la wale makadhi wastaafu. Kuna makadhi wastaafu vile vile huwa bado wanaendelea na kuozesha na kuachisha je, sheria inawaangalia vipi ya kuwapa mamlaka yale ya kuozesha na kuachisha katika suala hili la sheria.

Mhe. Spika, nataka nitoe lalamiko moja niliwahi kuikutia kesi pahali pamoja watu wanajadiliana. Kuna mwanamama mmoja alikwenda kwa kadhi, kadhi X amestaafu alikuwa na mume tayari wameshapanga kumuoa huyu mama ana walii wake ambao ni kaka zake mama mmoja baba mmoja lakini alikwenda kwa miongoni mwa makadhi wastaafu akapeleka shauri lake la kutaka kuolewa na bwana huyu kadhi yule bila ya kushauriana na walii wake alichukua fatua ya kumuozesha.

Je, Mheshimiwa suala hili likoje, niombe tu kwamba Kitengo hiki cha Kazi kinahitaji kuwa makini sana, kwa sababu masuala ya kisheria yanatakiwa yafanywe kisheria wala yasifanywe kwa kubahatisha tu ikiwa walii wa ndoa ile yupo basi kadhi anawajibika kufanya nini, ili kuiunganisha ndoa ile na wakati walii hajakataa kumuozesha mtoto wake au ndugu yake.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 20 kifungu cha 66 naomba hapa ninukuu:

"Mhe. Spika, katika kujenga uwezo Afisi imewapeleka masomoni wafanyakazi wawili kwa ngazi ya shahada na wawili katika ngazi ya stashahada kwa Unguja na Pemba. Sambamba na hilo Afisi inaendelea na uimarishaji wa maktaba ya kiislamu kwa kununua makatibu ya kuwekea vitabu na kutafuta vitabu vyengine muhimu kwa ajili ya maktaba hiyo".

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na ni jambo ambalo linafaa sana kwa sababu kuna historia kubwa ya wazanzibari kuhusiana na maktaba ya kiislamu. Maktaba ya Kiislamu kuwepo Zanzibar kwa kweli ni jambo zuri kwa sababu asilimia kubwa ya wazanzibari ni waislaamu. Kuna wageni mbali mbali wameingia katika nchi hii, kuna mashekhe wakubwa wakubwa walitangulia kuwepo kwa maktaba ya kiislamu na kuweka kumbukumbu za mambo mbali mbali ya kiislsmu kwa kweli ni jambo zuri na linafaa kwa kweli kupigiwa mfano.

Ninaiomba Wizara hii ilifanyie juhudi suala hili si kununua tu makabati bali kutafuta vitabu mbali mbali vya historia, vitabu mbali mbali ambavyo vinaelezea mambo mbali mbali ya uislamu katika nchi yetu ya Zanzibar, ili kizazi kiweze kurithi tabia njema ya waliotutangulia.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango niende katika ukurasa wa 23 Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, inaonekana hapa kwamba mwaka 2014/15 wamezaliwa watoto wengi, Mwenyezi Mungu awajaalie wawe ni watoto wenye barka na wale waliotangulia basi wakawasaidie wazazi wao huko. Lakini Afisi bado inakabiliwa na changamoto ya kuzorotesha upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa hasa niseme pale kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, bado mpaka leo watu wanasumbuka kwenda na kurudi, kwenda na kurudi kiasi anazaliwa mtoto unakaribia mwaka mmoja au na zaidi mtu anaambiwa nenda rudi, nenda rudi. Niiombe Wizara katika kitengo hiki cha Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo, viwe makini sana katika kuweka miundombinu ya kupatikana vyeti kwa wakati. Mhe. Spika, kuzorota kwa kupatikana kwa vyeti kwa kweli kunazorotesha mambo mengine ambayo yanatakuja kumfaa mtoto huyu baadae.

Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili alipe kipaumbele sana kwa sababu watu wamepata muamko watu wengi waliozaliwa katika miaka ya 1960 na huko mpaka leo kuna watu wengi hawana vyeti vya kuzaliwa. Lakini watu waliozaliwa miaka ya hapa elfu mbili wazazi wengi wamefahamu umuhimu wa kupatikana kwa vyeti vya kuzaliwa. Sasa vyeti vya kuzaliwa unapopatikana ule msongamano wa kwamba kesho, kesho kutwa, mwezi ujao tarehe fulani linawavunja moyo sana wananchi wetu. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali lengo lake kubwa kuweza kuwasajili watu wake na lianzie hapa kwa vizazi. Kwa hivyo ninaomba suala la kupatikana kwa vizazi vyeti, basi lipewe kipa umbele na wala kusiwe na nenda rudi zaidi ya miezi miwili au mitatu Mheshimiwa watu wanasumbuka, wengine wanakaa mazingira ya mbali, wanakaa mazingira ambayo nauli ya kwenda na kurudi kwa siku ni zaidi ya shilingi elfu tatu.

Kwa hivyo tuwapunguzie urasimu wa kwenda na kurudi na tunapowapangia tarehe basi maafisa wanaohusika wanapopangia tarehe ya kwamba wewe unatakiwa uje

tarehe kadhaa, basi kusiwe na mzunguko tena. Mhe. hili ni suala muhimu sana na naomba kwa kweli kwa ujumla wake Serikali ilizingatie.

Jengine katika vizazi na vifo niseme kwamba bado wananchi wetu wengi hawajahamasika kabisa kuandikisha vyeti kwa ajili ya kifo na mimi niseme kwamba hili ni tatizo kwa watu wetu, wizara ina kila haki ya kutoa elimu, kutoa taaluma ya kutosha ili watu waelewe umuhimu wa kuchukua vyeti vya kifo kama walivyojua umuhimu wa kuchukua vyeti vya kizazi.

Mhe. Spika, kwa kweli kupatikana kwa orodha ya waliofariki katika nchi ni jambo muhimu kwa sababu kuna mambo mbali mbali ambayo yataisaidia Serikali kuweka taratibu zake na takwimu zake. Kwa hivyo wizara inawajibika na inalazimika sana kutoa taaluma ya kutosha ili kuhakikisha kwamba vyeti kwa ajili ya vifo vinapatikana.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika kiambatanisho Nam. 5 (b). Mhe. Spika, hiki kinaonekana katika ukurasa wa 49, hapa niende katika ufunguaji wa kesi Mahakama za Kadhi.

Mhe. Spika, Mahakama za Kadhi, Wilaya kuna Mahakama ya Kadhi Wilaya ya Mjini zilifunguliwa kesi 586 katika kipindi cha mwaka 2014/2015, lakini kesi zilizopewa hukumu ni kesi 232. Kwa hivyo, ni nusu tu ya kesi ambazo zimetolewa uamuzi kuna kesi nyengine bado zimeganda.

Mhe. Spika, lakini nikienda katika Mahakama ya Mwera kuna kesi 60 zile zilizotolewa uamuzi 50, hapa imekwenda vizuri lakini nikiendelea na mtiririko huu ni kwamba kesi bado zinaonekana kuwa bado zinazorota sana katika Mahakama zetu. Na zinapozorota kesi za mwaka huu ni kuongezeka kwa wingi wa kesi katika mwaka ujao. Kwa hivyo, maoni yangu ni yale yale kama niliyozungumza mapema kwamba tunapaswa kabisa kabisa Mahakama zetu kufanya kama inavyowezekana kwamba kesi hizi zisirundikane kwa wingi ili kila mmoja ambaye amefunguliwa shauri ajue aende wapi katika maamuzi ya kesi hizo.

Mhe. Spika, mwisho niseme kwamba naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kusema machache katika hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kweli nimpongeze pamoja na watendaji wake wote na niseme kwamba wizara hii pia nayo ni muhimu kwa sababu ya kusema hivyo ni kwamba kwanza inasimamia suala muhimu sana la Katiba na Katiba ndio sheria mama na sheria nyengine na pia inasimamia taasisi mbali mbali ambazo pia nazo ni muhimu.

Mhe. Spika, kwa sababu hotuba hii Mhe. Waziri amesoma kwa ufanisi mzuri na vile vile Kamati ya Katiba na Sheria kwa niaba ya Mwenyekiti imesomwa na mtoto wangu hapa Mhe. Wanu Hafidh Ameir na ameisoma kwa ufanisi mzuri na yale waliyoyatoa kama nikuishauri wizara, kwa kweli mimi niko pamoja nao.

Mhe. Spika, katika pongezi zangu nina suala moja kwenye utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2014/2015 ambapo Mhe. Waziri ametwambia kwamba katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 10,244,164,000 kati ya fedha hizo shilingi bilioni sita, milioni mia tano hamsini na moja elfu, mia nne na hamsini na tano zilipangwa kulipia mishahara stahiki na stahiki mbali mbali za watumishi. Na shilingi bilioni tatu, milioni mia sita tisiini na mbili elfu, mia saba na tisa kwa matumizi mengineyo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 jumla ya shilingi bilioni sita, milioni mia tano na thamanini na tisa ambayo ni *sixty one percent* zimepatikana.

Sasa nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri ikiwa pesa hizi kwa mujibu wa hapa nataka anisahihishe kama bilioni sita zilitakiwa ni mishahara na stahiki nyenginezo, lakini hapo hapo zilizoingizwa ni hizo bilioni sita laki tano, milioni mia tano na thamanini na tisa. Sijui hata kama hiyo mishahara ilipatikana sahihi kwa ujumla kwa sababu naona kama ina-*defer*. Kwa hivyo, nilitaka nijue zaidi kwamba ni kweli pesa hizo ndizo zilizotiwa kama ni mishahara ndio hivyo hivyo labda iwe *less* ya hapo lakini naona kama kuna *difference* kidogo kwa hivyo ningetaka atapokuja aniweke sawa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, halafu niipongeze wizara pamoja na kazi zake mbali mbali, lakini idara imefanya maandalizi ya kazi za utafiti na sera kwa kuratibu utafiti wa taarifa za msingi za sekta ya sheria *(Legal Sector Baseline Study).* Amesema aidha kupitia kwa Mradi wa Mabadiliko ya sekta ya sheria idara imeratibu utoaji wa mafunzo kuhusu uhalifu wa kimtandanao, sijui kama ndio ile *cyber crime* tulipata semina kidogo kwa ufanisi huo basi ningeomba kukatungwa sheria ambayo yule atakayeingia kwenye vitendo hivyo vya *cyber crime* basi ingekuwa ni vizuri vile vile tukawa na sheria.

Mhe. Spika, kama wenzangu walivyokwishakutangulia taasisi hii ni muhimu na ina taasisi nyingi ambazo zina umuhimu vile vile kama Mahakama ambayo ni muhimili mmoja tulionao katika serikali yetu. Kwa hivyo, lazima nayo vile vile ifanye kazi yake kwa ufanisi zaidi ili suala la rushwa basi lione kwamba kwenye taasisi hii lisiwepo kwa sababu rushwa ni adui wa haki na zile stahiki zote iweze kupatiwa kwa Mahakimu wetu, kwa sababu haiwezekani mtu akafanya kazi kama ile na ndio zinazosababisha kuwepo kwa rushwa. Kwa hivyo, ili wafanye kazi vizuri basi zile stahiki ziweze kufanyiwa kwa mujibu wa kazi zao.

Vile vile kuna Ofisi ya Mwanasheria ambayo ni muhimu lakini kuna taasisi za kuwa lazima ili zile sheria zisiwe na kukinzana, ni Ofisi ya Mwanasheria basi washirikiane pamoja na ile Tume ya Kurekebisha Sheria.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kweli nayo vile vile kuna changamoto kwanza ya bajeti yake, bajeti inayopewa ni ndogo sana mimi kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* nimeona. Kwa kweli Mkurugenzi wa Mashtaka ni mtu mweledi sana na ni mtu muaminifu na muajibikaji, lakini kutokana na ile bajeti ambayo anaipata kwa kweli haikidhi hata na zile stahiki pia hazitoshi unamkuta Hakimu au Mwanasheria wa pale ukitizama na wanasheria wengine basi haziendani sawa.

Pia niwashukuru kwa hii Taasisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara nafikiria na wao vile vile nawashukuru sana.

Vile vile kuna Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, kama alivyotangulia kusema mwenzangu ni lazima elimu ya kutosha itolewe kwa sababu mtu anaona akishafiliwa na mtu wake basi imekwisha, kumbe kuna vitu vyengine ambavyo vinaendelea na moja ni ile watu wengi sasa hivi misaada inakuja kutaka kuwasaidia watoto yatima, lakini ukiambiwa upeleke kile cheti cha kifo basi kwa kweli watu wanashindwa kupeleka na wanaweza wakawakosesha haki wale watoto.

Mhe. Spika, vile vile nikienda kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana nimeona kwamba kuna mambo mbali mbali na hasa haya mambo ya wakfu, kunakuwa na wakfu za watu ambazo zinatakiwa pale zihifadhiwe ili wenyewe yawasaidie kule walikokwenda. Mhe. Spika, kuna mambo ya hapa na pale yanakuwa ni vikwazo kwanza ule ukodishaji wa yale maeneo yanakuwa, kwa kweli kuna mambo yanakuwa ni tatizo wenyewe wanajua yapo mambo mbali mbali kuhusiana na namna wanavyokodisha, wao wenyewe wapo hapo juu sitaki niseme halafu nije kuikosea. Kuna mambo ya …. kwa hivyo wajue kwamba ile mikataba wanavyojaziana, basi iwe na ufanisi ndani yake ili wale wenyewe wenye yale maeneo waliyoyaacha kama ni wakfu iwe inaleta faida kwao na kwa wale wengine waliowaacha pia.

Mhe. Spika, kwa kweli kwenye kitabu hiki sina mengi sana isipokuwa yale yale tu ninayokaa nikayasema mara nyingi kwamba kutokana na mfumo huu wa kibajeti ambao moja kwa moja sasa hivi tunaenda kwa programu na huku ndio kutaonesha ufanisi. Kwa hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Amani naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Spika, ahsante sana nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote sina budi na mimi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa katika majukumu yetu ya kila siku. Pia nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya kututayarishia bajeti yetu hii ambayo kwa muda huu tunaijadili.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti, niipongeze serikali kwa kutaka kwa mpango kazi wake ambao umekusudia kununua *machine* hii ya *DNA*. Mheshimiwa hili ni jambo zuri na ambalo ni kilio chetu cha kila mara tunaposimama hapa huwa tunasema kama serikali ijipange katika kukitafuta chombo hiki ili tuanze kuondosha ile kadhia inayowapata na kuwasumbua watoto wetu katika zile hali ambazo zinawatokea za ubakaji. Hii ingekuwa ni hatua moja tukiipata hii *machine* basi tunaweza pengine tukapiga hatua kwa kuwabaini wale ambao wanasababisha matatizo katika ubakaji wa watoto wetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika ukurasa wa 8 ambapo kuna Mahakama. Mheshimiwa pia niipongeze Idara hii ya Mahakama kwa kazi kubwa ambazo wanazozifanya lakini pia niseme wana ufinyu mkubwa wa bajeti. Mhe. Spika, nao huu ni muhimili mwengine, niiombe sana serikali ijipange katika kuuwezesha muhimili huu ili uweze kujitegemea, kwa sababu huu ni muhimili mkubwa ambao unatoa haki za wananchi wetu, lakini utakapokuwa bado unaendelea kujificha ficha hivi basi haki hizo zinaweza zikakosekana.

Kwa sababu kwanza Mahakama inakosa fedha hata huu mrundikano wa hizi kesi, basi pia unasababishwa na ukosefu wa fedha katika Mahakama. Sasa kuendelea mihimili hii tukaiweka mahala pamoja, ili hawa wakakosa nguvu yakuweza kujiendesha basi inawezekana ikawa tunazidi kuwafinya na haki za watu humu zinakosekana.

Mhe. Spika, wanashindwa hata kuwaita mashahidi kwa ajili ya kuja kutoa ushahidi katika Mahakama kwa ukosefu wa fedha katika Mahakama. Vile vile wenzangu hapa wameeleza pia kuna usumbufu wa ma-*assessors* kupata fedha zao kwa wakati na inakuwa pengine zinadundulizika, huku na pengine na wao wanashindwa kuhudhuria katika Mahakama, kwa ajili ya kukosa ile nauli ambalo posho wanalopewa katika Mahakama kuweza kufika Mahakama na kutuliza zile kesi ambazo zinaendelea pale.

Mhe. Spika, pia niiombe sana serikali iliangalie hili kwa umadhubuti kwa sababu kuna vitendea kazi kama usafiri ambao wanakosa Mahakimu wetu na wanakuwa wana usafiri ambao hauna uhakika na kutokana na zile kazi zao ambazo

zinaonekana ugumu wake. Ni vizuri tukawapatia wao fungu lao ikawa wanaweza kujitegemea wao wenyewe muhimili huu ukawa unajitegemea ili Mahakama ikaweza kufanya kazi vizuri na ikaweza kupata majengo yaliyo bora, lakini pia kupata nyumba za makaazi mazuri za Majaji wetu na Mahakimu wetu.

Mhe. Spika, niende pia katika Ofisi ya Mufti. Mimi naipongeza ofisi hii kwa kazi nzuri ya utatuzi wa migogoro katika misikiti yetu na madrasa zetu. Na pia nawapongeza kwa kuendelea kutupatia taarifa zile za mwezi unapoandama kwani huwa tunawategemea sana wao tupate taarifa kutoka kwao ili tuweze kujua kufunga na kufungua.

Mhe. Spika, mimi niiombe sana hii Ofisi ya Mufti kutokana na kukosekana hii elimu ya ndoa ambayo wenzangu pia wameigusia, niiombe basi kwa kuwa wao wanakuwa wanafanya ziara za mara kwa mara katika madrasa zetu na misikiti yetu, basi niwaombe wawaombe walimu wa madrasa kuanzisha kwa elimu hii ya ndoa katika madrasa zetu, ili wanafunzi waweze kujua elimu hii tangu wapo katika madrasa pale mpaka hatimae wanafika kuolewa au kuoa.

Kwa hiyo, elimu hii watakuwa wanaijua na mtu anakwenda kuoa ilhali akiwa anaelewa taratibu zote za ndoa katika dini yake. Mhe. Spika, niombe sana hilo ili nalo lipatikane kama yanavyopatikana masomo mengine.

Mhe. Spika, lakini pia niiombe ofisi hii kwa kweli tuna wahisani wengi ambao huwa wanakuja kutusaidia kujenga misikiti na kwa kweli *mashaallah* tunashukuru tuna misikiti mikubwa, mizuri mizuri na mingi. Lakini niiombe ofisi hii kwa kuwa wahisani wale bado tunao na wanaendelea kuja na misikiti mingi tayari tumeshajengewa na madrasa nyengine tunazo, *alhamdulillah*.

Kwa hiyo, niiombe ofisi hii sasa kuwaomba wahisani wale watusaidie sasa katika kuwasomesha walimu ili tuweze kuwa na walimu katika madrasa ambao watakwenda na mambo haya ya sasa na pia tuweze kupata Maimamu kwa sababu misikiti mingi tunayo lakini utakuta tuna uhaba wa Maimamu na walimu walio wazuri. Kwa hiyo, sasa wale wahisani tuwaombe sasa misikiti tayari tunayo sasa watusomeshee vijana wetu hawa ili tuweze kuwa na walimu wazuri na Maimamu wazuri watakaoweza kuendesha misikiti yetu ile.

Mhe. Spika, pia niombe kwa hizi Madrassa tulizonazo zinasajiliwa lakini bado kwa kiasi kikubwa usajili huu haujawa wa kutosha, bado ziko Madrassa hadi vijijini kwetu. Mimi niseme bado ziko nyingi hazijasajiliwa.

Kwa hiyo, niombe hizi fomu ziendelee kutolewa kwa wingi na hii elimu pamoja na kuwa zinapelekwa hizi fomu katika wilaya lakini pia si vibaya pia tukatangaza

katika chombo cha Habari kama hivi tunavyotoa matangazo kutoa kwa elimu nyengine. Tuwatangazie walimu wa vyuo popote walipo, ili waende katika wilaya zao wakachukuwe fomu hizo waliokuwa hawajajisali ili waweze kujisajili.

Hii itarahisisha Afisi ya Mufti kujua idadi ya vyuo vyake vyote viliopo Unguja na Pemba na hata kile ambacho wanakipata kupitia misaada wanayoipata basi itawarahisisishia wao kujua na kuweza kugawa, kwa sababu itakuwa idadi wanaijua iko kamili na hata wale wanaopata nao basi watakuwa na wao wanafurahia kwa sababu watakuwa wanajua wengine watakuwa wanalalamika kama misaada inakuja lakini sisi hatupati. Lakini kumbe hawamo katika idadi ya wale waliosajiliwa.

Pia niombe hii Afisi kuzungatia pale wanapopata misaada kama misahafu na vitabu vyengine vya dini basi waweze kuwasambazia katika vijiji hasa vijijini tunakosa sana mambo haya. Waweze kusambazia katika madrasa zetu, ili na wao waweze kufaidika na vitabu hivi na masafu waweze kusomeshea wanafunzi wetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende ukurasa wa 23 katika Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Mhe. Waziri ni kweli ulioeleza hapa kwamba vizazi vinaendelea kusajiliwa, lakini bado kuna tatizo la usajili wa vifo. Hili ni kweli na bado watu wetu hawajawa na ule muamko ambao wa kujua kama kuna umuhimu mkubwa wa kusajili vifo vinapotokea.

Shida inajitokeza pale anapokuwa mtoto yule yatima sasa anatafutiwa msaada kunatangazwa misaada watoto yatima, sasa na mzazi anataka apate lakini kumbe hajasajili kile kifo cha yule mzazi wake inabidi anakosa na inabidi urasimu mkubwa.

Sasa mimi niombe serikali kwa kuwa tayari serikali za vijiji tunazo Shehia niombe sana Masheha wetu pamoja na sisi Waheshimiwa tutaongeza elimu hii kwa wananchi wetu. Lakini kwa kuwa chombo kipo basi tuombe kwa sababu Sheha pale yuko yeye na Wajumbe wake na nadhani hakuna kifo kinachotokea nje ya Shehia, vifo vyote vinatokea ndani ya Shehia zetu. Kwa hiyo, niombe sasa Mhe. Sheha tumpe na hili jukumu la kuona kunapotokea kifo aweze kuratibu pale ili baadae aweze kumwambia yule mzazi afike katika Afisi ile na apate kile kitambulisho muhimu cha yule mzazi aliefariki. Hii itasaidia na halafu tufatilie sasa tuwapitie Masheha wetu katika vyombo vyetu, ili kujua kila mwezi vimetokea vifo vingapi katika Shehia hizo. Hapo tutaweza pia kuisaidia serikali kuweza kujua vizazi na vifo katika Shehia.

Mhe. Spika, pamoja na vizazi na vifo lakini pia kuna tatizo la ndoa na talaka. Hili nalo halina takwimu sasa kwa sababu sio mara nyingi kusajiliwa ndoa na talaka

hakupatikani usahihi mzuri. Pia kupitia Sheha tungeomba hivi ndoa zote zinafanyika katika Mashehia ni vizuri Sheha akawa anaelewa ndoa inayofungishwa japo asialikwe, lakini kuelewa kama hapa panafungishwa ndio hii ili akachukuwa ile taarifa na ikaweza kusaidia serikali.

Mhe. Spika, niendelee katika ukurasa wa 27 kwenye Wakfu na Maliamana. Niipongeze sana kwa kazi nzuri ya kuendelea kuzifanyia tafiti mali za wakfu na pia kusimamia safari za Hijja. Mhe. Spika, ni kweli wenzetu wanajitahidi sana katika kuzitafuta nyakfu mbali mbali zile ambazo zimepotea potea wenzetu wanaendelea kuzitafuta ili haki za watu ziweze kupatikana.

Mhe. Spika, nawapongeza kwa hilo lakini pia niombe taasisi hii kwa kuwa inaendelea kuwaelimisha watu basi ni vizuri kupita katika taasisi zetu za serikali au za watu binafsi, ili basi wakatoa elimu ile ya kuhamasisha wananchi jinsi ya umuhimu wa waislamu kwenda katika Hijja ila basi wakahiari kukatwa fedha zao, ili wakaweza kujiwekea akiba kidogo kidogo kutokana na uwezo wetu mpaka ikitimia ile safari ya mtu basi akaweza kusafiri.

Naamini tungeweza kupata mahujaji wengi kwa kupitia njia hiyo. Kwa hiyo, niombe sana basi waendelee kutoa elimu hii kwa wananchi, ili waislamu tuko wengi hapa na fursa hii ya Hijja inamlazimikia kila mtu. Kwa hiyo, tusije kuona kwamba hatuna uwezo lakini kumbe tukijipanga vizuri tunaweza tukaenda Hijja watu wengi.

Mhe. Spika, niende katika Afisi ya Hatimiliki na hawa nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa kazi nzuri ambayo sasa inaonekana kuwanufaisha wabunifu wetu. Tumeanza kuona faida inayopatikana wabunifu sasa haki zao zinawarejea wenyewe baada ya kuwa zinapotea na kuibiwa. Niwapongeze sana kwa hilo na niwatake waendelee na juhudi yao hiyo lakini, pia tuwafikirie na wao kuwapatia wale wataalamu ambao wanawalalamikia kila mara wana upungufu wa wafanyakazi katika yao.

Pia nitoe msisitizo wa wale ambao watabainika kukamatwa katika wizi wa kazi hizi za ubunifu basi waweze kuchukuliwa hatua za kisheria, ili mafanikio yazidi kuendelea kupatikana kwa wale wabunifu ambao wanaonekana kufanyakazi ngumu.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme nashukuru sana na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mfalme wa wafalme mwenye kutoa malipo kwa waja wake kwa anayoyafanya siri na dhahiri.

Pia namshukuru sana kwa kuniwezesha kusimama hapa na kutoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Wizara ambayo inasimamia sheria na utowaji wa haki nchini.

Mhe. Spika, naomba pia nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu huo na vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna alivyoiwasilisha hotuba yake ya bajeti kwa kweli aliiwasilisha kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu katika ukurasa wa 12 unaozungumzia Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Pia naomba uniruhusu niipongeze sana Afisi hii kwa namna inavyoteleza majukumu yake. Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri alivyotueleza katika hotuba yake na vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu aliekuwepo Mhe. Said Hassan anafanyakazi zake vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia naomba Mhe. Waziri anipelekee pongezi zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu aliepita Mhe. Othman Masoud kwa namna alivyokuwa akitekeleza kazi zake kwa kujiamini sana. Mhe. Spika, kiwango chake cha ujasiri kitakumbukwa na Wazanzibari wote kwa namna alivyosimamia kidete kwa ujasiri wa hali ya juu kutetea nchi yetu ya Zanzibar katika Bunge la Katiba Dodoma.

Mhe. Spika, kwa kweli kiwango chake cha ujasiri alichokionesha ni heshima kubwa kwake kwa familia yake na kwa nchi nzima na kwa hakika Mwenyezi Mungu atamlipa mema kwa moyo wake wa kuitetea nchi yake bila ya woga. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie ukurasa wa 23 juu ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, hapa naomba nimlaumu sana Mhe. Waziri kwa namna ya utaratibu mbovu wa uandikishaji wa vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Spika, kwa kweli hapa naomba nikemee sana uandikishaji wa vyeti vya kuzaliwa huwa unachukuwa muda mrefu havipatikani na hatujui hasa tatizo ni nini. Mhe. Spika, lakini tatizo lililopo ni kwa wale waandikishaji wanaomba vyeti vya kuzaliwa wakiwa ni watu wazima. Pamoja na kuwa watu hao huwa wameshajiandikisha na wameshalipia lakini vyeti hivyo huchelewa zaidi ya miezi minne mpaka sita.

Mhe. Spika, bado vyeti vya kuzaliwa vinaganda na havitoki, sasa nadhani Mhe. Waziri na watu wake hawatoi vyeti hivi vya kuzaliwa, kwa khofu kwamba wakivipata watu wataweza kupata vyeti vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, hili ni jambo baya ambalo naomba Mhe. Waziri anipe maelezo vyenginevyo nitazuia fungu la Programu hii.

Mhe. Spika, hii ni Afisi tunayotegema itoe haki lakini leo ikiwa Wazanzibari wanakwenda pale kutaka vyeti vya kuzaliwa wanazuiwa, kwa muda mkubwa kwa kuhofiwa watapata vitambulisho vya Uzanzibari kwa kweli hili ni tatizo na namuomba Mhe. Waziri atueleze.

Eneo jengine Mhe. Spika, ambalo naomba kidogo nilizugumzie ni Afisi ya shughuli za usajili wa Biashara na Mali. Mhe. Spika, hii ni Afisi muhimu sana ambayo uendeshaji wake wa kazi ni muhimu sana katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, hivi karibuni kulitokea jambo ambalo mimi limenishitua sana. Jambo lenyewe kuna Kampuni inaitwa *Transworld*. Mhe. Spika kampuni hii imesajiliwa kwa watu wawili tafauti lakini kwa jina moja. Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo linahitaji maelezo kwa nini jina moja la Kampuni likasajiliwa kwa watu wawili.

Mhe. Spika, hivi kweli Afisi ya Msajili haina kumbukumbu za usajili wake na ikiwa ni hivyo si hatari hiyo Mhe. Spika, ninaomba Mhe. Waziri anipe maelezo hali hii imetokeaje ni uzembe ni makusudi au ni kwa dhamira imekusudiwa. Mhe. Spika, kwa kweli mimi naunga mkono hotuba hii lakini nasubiri Mhe. Waziri anipe jibu. Naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Kuna dakika kumi na Mhe. Bikame Yussuf Hamad ulinambia kwamba nikuite jioni. Lakini ningekuomba ukachangia sasa kwa sababu jioni unaweza ukachelewa kidogo.(*Makofi*)

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kutaka nimalizie hizi dakika kumi zilizopo kwa sababu nilileta ombi langu lakini haikuwezekana kwa jioni.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo sana kwa sababu kwanza ni Mjumbe wa Kamati.

Awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia tukafika katika Baraza hili kwa siku ya leo ya Ijumaa tukiwa katika hali ya utulivu na amani. Lakini tukiwa na hali ya afya njema. Kwa hilo hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, jengine nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao walitupa wakati wa miaka miwili hii na nusu ya kwenye kamati walionesha umahiri wao wa hali ya juu na kutujali. Kwa hiyo, hatuna budi kuwashukuru na tuwapongeze na kama kuna pahali tuliwakwaza basi watusamehe kwani ndio hali ya binaadamu.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara muhimu sana kwa jamii zetu hasa tukizingatia ni wizara ambayo inatoa haki za wananchi. Lakini ni wizara ambayo kuwa mambo ya sheria yamo katika wizara hii. Ni wizara muhimu sana na tunaiomba serikali basi waangalie kwa jicho la huruma sana katika kuwapangia bajeti zao, ili wananchi waweze pale watakapokuwa na matatizo yao.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika Mahkama ambayo kwa Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki ukurasa wa 10 ameeleza kuwa Mahakama ya Watoto ilianza mwaka wa Fedha 2014/15 ikiwa na idadi ya mashauri 23 yalisalia kutoka miaka ya nyuma na kupokea mashauri mapya 28 na hivyo kufanya idadi ya mashauri kufikia 51 katika kipindi cha Julai 2014/Machi 2015. Mahakama ya watoto imetoa maamuzi ya mashauri 9 uchache huo unatokana na kukosekana kwa ushahidi.

Mhe. Spika, hili suala linaelezwa siku zote kutokana na jamii kukosa kutoa ushirikiano wa pale yanapotokea matatizo haya hasa kuhusu kesi za watoto. Mhe. Spika, hilo limekuwa tatizo kubwa la udhalilishaji wa watoto kijinsia na mambo mengine na tatizo la changamoto hii kukosekana kwa ushahidi limekuwa, pia ni tatizo sugu na Mhe. Spika, matatizo haya ya kesi hizi za watoto zimekuwa zikiendelea siku hadi siku juu ya kuanzishwa hii Mahakama ya Watoto. Lakini bado ukosekanaji maamuzi yaliyo sahihi basi inashindikana na imekuwa ni tatizo kubwa na tatizo sugu.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, sijui hasa tufanye dawa gani kwa kusema kweli kwa sababu watoto wanaendelea kuzalilishwa lakini tukitizama bado uamuzi sahihi umeshindikana kupatikana.

Mhe. Spika, kutoka kesi 51 na kusikilizwa kutolewa uamuzi mashauri haya 9 na hatujui hizi kesi pengine ni za mwaka gani kama ni za juzi na jana au ni za lini. Lakini mpaka leo hii kwenye Mawio haya masuala yanaendelea na taarifa za mawio asubuhi kuna mtoto karibuni amedhalilishwa na watu wasiopungua 3 mtoto mmoja wa miaka 14. Sasa leo kila tukiendelea kunaku kukosekana kwa ushahidi inakuwa ni tatizo sugu.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi niiombe jamii na siku zote tunaomba kupitia vyombo hivi tuiombe jamii kushirikiana na serikali kwa ujumla ili tuweze kuliondoa tatizo

hili. Mhe. Spika, serikali peke yake haiwezi kuonda tatizo hili. Lazima tushikamaneni na jamii kwa ujumla na sisi wenyewe tuwe watu mahiri kuweza kutoa ushahidi. Lakini pia Mhe. Spika, suala hili lina usiri wa ushahidi kwa sababu huyu anaedhamiria kufanya mambo haya hafanyi ndani ya hadhara.

Kwa hiyo, serikali pia nayo tunaiomba waridhike na ushahidi wa yule mtoto ambaye kuwa pengine ni mtoto anaweza kusema, kwa sababu anaekifanya kitendo hiki hafanyi kwenye watu au kwenye jamii anafanya wa kujificha. Sasa leo wewe serikali ikitaka lazima itoe ushahidi wao bado yuko hali gani ndani ya sehemu zake za siri bado ana matatizo gani.

Hii itakuwa haipatikani ushahidi. Kwa hiyo, niombe serikali nayo kama mtoto anaweza kusema na ana akili timamu hata huyo aliekuwa hana akili timamu mtu yoyote anaefanyiwa kitendo kama hichi anaweza kutoa ushahidi wake mwenyewe. Kwa hiyo, wakubaliane na haya wasingoje ushahidi wanautaka wao wa vipimo. Mhe. Spika, hilo ni moja nililosema niligusie.

Lakini niipongeze Kamisheni hii ya Wakfu .......

**Mhe. Spika:** Hali inatulazimisha kwamba tutoke humu ndani na katika mchango wa Bikame nilikuwa napenda na nina wasi wasi ili asije akasema mambo hayo nafanya kwa kificho. Lakini nashukuru hakusema hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki kwa kweli kimsingi umekwisha na hitilafu ya umeme iliyopo haitupi raha kuweza kuendelea hata tungeomba muda uongezwe. Kwa hiyo, tukubaliane kwamba turudi tena jioni ambapo baada ya kuona Waheshimiwa Wajumbe wanashughulika shughulika jioni nitakuwa na wachangiaji wafuatao:-

Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Mwanasheria Mkuu, atafuata naye mwishoni lakini na yeye ana nafasi yake.
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Hawa niliowataja pamoja na wengine wote naomba tufike mapema ili tuweze kuchangia kabla sijamwita Mhe. Waziri ili aje afanya majumuisho.

Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe sasa turudi tukapate kusali ili jioni tuwahi mapema.

*(Saa 6:02 Mchana kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Haya majadiliano yanaendelea. Ninajua Mhe. Mwanasheria Mkuu utaifanya hiyo kazi ni kawaida yako unapiga ngoma huku na huku, basi majadiliano yanaendelea.

Basi nimkaribishe Mhe. Rufai Said Rufai.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati jioni hii Mwenyezi Mungu akatujaalia hali ya afya na uzima, tukaweza kukutana katika suala zima hili la kupitia na kutoa maelezo yetu katika hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, mimi nianze katika kutoa pongezi zangu za dhati katika Ofisi ya Mhe. Mufti. Hii Ofisi ni Ofisi moja nyeti, ni Ofisi inayomuhusu kila Muislamu aliye katika nchi hii. Kwa hivyo, katika ufanyakazi wake inaonekana kwamba hii Ofisi inajitahidi katika kufuatilia mambo mbali mbali yanayohusu Dini ya Kiislamu na Waislamu wenyewe.

Mhe. Spika, niipongeze hii Ofisi kwa ufuatiliaji na juhudi za makusudi za kupata takwimu sahihi za Misikiti na Vyuo vya Kuruani. Imefanya kazi moja kubwa na ni kazi moja adhimu ambayo kwa Zanzibar hakuna kijiji au kitongoji kilichokuwa ima hakina Msikiti au Madrassa. Kwa hivyo ni jambo moja kubwa na ni jambo ambalo linahitaji ufuatiliaji wa hali ya juu ili kuweza kuzipata hizi takwimu na ili kuondosha nong'onong'o, kuondosha mivutano baina ya Msikiti kwa Msikiti au Madrassa kwa Madrassa.

Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri hapa ameonesha kwamba walifanya ziara na wakagawa fomu karibu mia mbili na kumi na tano za Msikiti na mia mbili na kumi na tano za Madrassa. Lakini hivi karibuni Misikiti mia moja na kumi na nane na Madrassa mia moja na tisini na saba zimetambuliwa kuwepo kwake. Ni jitihada moja nzuri na ninaiomba hii Ofisi iendelee na masuala haya ya ugawaji fomu ili kila kinachowahusu Waislamu na Misikiti na Vyuo vyao basi viwe vimesajiliwa katika Ofisi hii Mufti.

Pia nimtake Mufti kwamba mara nyingi Zanzibar hasa hapa tulipo, leo Mhe. Spika, tupo mwezi wa Shaaban, kesho tunaingia Ramadhani. Kwa hivyo, mara nyingi hupata taswira baina ya kuwa mwezi umeonekana au mwezi haukuonekana.

Mhe. Spika, ningekuomba sana Mhe. Mufti, suala hili lisimamiwe linavyopaswa ili kuondosha lawama lawama, ili wananchi wapate kupata taarifa za mwezi kwa wakati. Mhe. Spika, ikifika saa nne na nusu za usiku Zanzibar hii hatujapata taarifa kutoka eneo lolote, hii kidogo inakuwa inaumiza, hii inakuwa inauma na pia na mwaka huu ninashauri tena, tukitaka tusitake Mhe. Spika, Zanzibar tuna miezi miwili ya miandamo ima ya Kimataifa au huu wa Kitaifa unaoandama hapa Tanzania.

Kwa hivyo, kama mwezi wa Kimataifa umeonekana basi waambiwe tu waliofunga Kimataifa kwamba kesho ni mwezi mosi kwa wale wanaofuata muandamo wa Kimataifa na wale ambao wanafuata kwa muandamo wa Tanzania, basi bado wao wataendelea na kula au na kufuturu kutokana na muandamo, ili kila mmoja aweze kuridhika na kile ambacho anachokifanya. Kwa sababu kila mmoja atalipwa kwa kila anachokifanya.

Kwa hivyo hili litatusaidia sana kwa wale ambao wanafuata muandamo wa hapa Tanzania au *East Africa* basi itawasaidia na wale ambao wanafuata popote mwezi utakapoandama, basi na wao itawasaidia kwamba leo ni siku yao ya kuanza kufunga. Kwa hivyo hiyo Mhe. Spika, inaweza kuwaweka wananchi wetu vizuri bila ya kuanza kujua nani leo anahitaji kufunga au nani ambao bado hawajastahiki kufunga.

Mhe. Spika, niipongeze tena Ofisi hii kwamba imejaribu jumla ya masuala karibuni mia moja na hamsini na mbili yanayohusiana na mambo ya ndoa na talaka, pamoja na mirathi yamejibiwa katika vipindi sabini na mbili ya maswali na majibu na vimerushwa kupitia *ZBC* redio pamoja na vipindi hivyo, wamejaribu kupitia katika vyombo hivyo vya habari. Ni suala moja zuri sana na wale ambao wanasikiliza redio basi ninadhani kwamba walifarajika ndani ya masuala haya na majibu ninadhani na wengine wamepata taaluma hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, talaka zimekithiri. Sasa talaka hivi sasa imekuwa kama maji ya kunywa, watu wanafanya ndoa kwa sherehe na urembo. Karibuni Madrassa kumi au kumi na tano, karibuni Dufu kila eneo pengine harusi moja inapigwa Dufu karibuni sita au wiki nzima harusi hiyo inapigiwa Dufu tu. Lakini ikimaliza Dufu ya mwisho na talaka imetoka. (*Makofi*)

Sasa sijui faida gani inayopatikana Mhe. Spika. Kwa hivyo ningeiomba sana hii Ofisi ikajaribu kutoa taaluma. Mhe. Panya Ali Abdalla asubuhi hapa amesema, katika hizi Madrassa zitoe elimu za ndoa, kabla ya vijana wetu hawajaingia katika ndoa, iwe kila wanachotaka kwenda kukifanya tayari kinajulikana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na hivi ndivyo mambo yalivyo, huwezi kuwa dereva kama hujajifundisha udereva, huwezi kuwa rubani wa ndege kama hujifundisha ndege. Kwa hivyo, kila kitu lazima kwanza upate mafunzo. Hivyo Ofisi ijaribu kutoa taaluma, kuwafanya walimu wa Madrassa ni kichocheo na kutoa elimu hii ili wanafunzi wao. Kwa sababu Mhe. Spika, baadhi ya wachumba wanapatikana kwenye Madrassa hii na Madrassa au Madrassa hiyo hiyo inazalisha ndoa katika Madrassa.

Kwa hivyo kama walimu hii taaluma wataitoa na kuhimizwa na kufanywa kwamba waiendeleze, basi mambo haya ya talaka ninadhani kwamba huenda yakapungua sana na vijana wetu wanaweza wakaishi kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hivi sasa ni wakati wa ndoa kwa sababu Ramadhani ipo karibu. Maeneo mengi ikikaribia Ramadhani ndipo watu wanapoowa, lakini haimalizi Ramadhani na ndoa nazo tayari zinaendelea kuachwa. Kwa hivyo huu si utaratibu wala si Uislamu, sijui ni mwendo gani niseme, pengine ni mwendo wa Kishetani. Lakini ni vyema wale waliokusudia kufunga ndoa wazidumishe ndoa zao ili ziweze kupata rehma kwa sababu ndani ya ndoa kuna rehma moja kubwa sana. Kwa hivyo ni vyema wana ndoa wadumishe hizi ndoa zao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika hizi Madrassa walimu wa Madrassa ni watu kama wametupwa, hawajaliwi. Ningeliiomba hii Ofisi, tunaamini kwamba Madrassa ni nyingi kuzilipa zote haiwezekani. Lakini angalau zitafutiwe wafadhili angalau kila mwisho mwezi au miezi miwili au miezi mitatu angalau wapatiwe posho dogo la kuweza kukimu kwenye baadhi tu ya maisha yao ya kawaida. (*Makofi*)

Kwa kumuacha tu mwalimu wa Madrassa anasomesha tu, chuo hicho aliyerithi kwa babu zake, baba yake mpaka yupo yeye, hakuna lolote linaloendelea na hali za wananchi wetu kama tunavyozijua. Mtoto anakwenda Madrassa na hasa Madrassa za shamba, mtoto anaweza kusoma mwaka mzima hata shilingi mbili hamchukulii mwalimu. Kwa kweli hali zao ni hali moja ngumu sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kutafutiwa ufadhili zinaweza zikasaidiwa hizi Madrassa. Kwa hivyo Mhe. Spika, tukitaka tusitake hapa Zanzibar wapo Waislamu wengi tena wenye uwezo. Lakini watu wamesahau kwamba wana wajibu wa kutengeneza Akhera zao. Kwa hivyo Ofisi iendelee kutoa semina mbali mbali za Waislamu wenye uwezo ili kuzisaidia hizi Madrassa, kwa sababu isije ikafika mtu pale ndiyo roho yake inatoka akamwambie Mwenyezi Mungu, eeh! Mwenyezi Mungu niahirishe kidogo angalau nikatoe sadaka. Pale nafasi itakuwa haipatikani tena. Mwenyezi Mungu kishasema hatoiahirisha nafsi yoyote hata sekunde itakapofika muda wake. (*Makofi*)

Sasa na muda wa kuyafanya haya ni hivi sasa huu wakati ninaiuzungumza na hapo tunapoendelea. Ndiyo wakati pekee wa kutoa ili kuzisaidia Madrassa zetu ili iwe ni akiba ya kesho Akhera tunakokwenda. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo kuna kila hali Waislamu kuacha mwenendo wa kusaidia tafrija mbali mbali wakasahau hizi Madrassa ambao ni muongozo unaofanya mtu mpaka kufikia hapo alipo. Kwa hivyo ni vyema sana Mhe. Mufti akazidi kuwafanyisha semina hawa watu wenye uwezo wao na kuzijali hizi Madrassa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika Ofisi ya Mrajis, Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, nimeona hapa kwenye Ofisi hii imetoa takwimu kidogo. Takwimu zinatuonesha kwamba mwaka 2014/2015, Ofisi hii Mrajis, Vizazi na Vifo imesajili vizazi visivyopungua 43,501, siyo ongezeko dogo, ni ongezeko kubwa. Kati ya hawa wanawake ni 21,418 na wanaume ni 22,083.

Mhe. Spika, ukiangalia hapa utaona kwamba kizazi hiki kinachokuja wanaume wameongezeka mara mbili kuliko wanawake; karibuni ni watu 665 wameongezeka kulikoni wanawake. Kwa hivyo, mwaka huu 2014/2015, kwa hesabu hii wanaume wamekuwa ni wengi zaidi.

Mhe. Spika, kwa hivyo pia hesabu hii imetuonesha kwamba kuna vifo vilivyojitokeza wakiwemo wanaume 1,327 na wanawake 1,098. Kutokana na takwimu hizo ni wazi kwamba uandikishwaji wa vifo bado haujawa mzuri. Juu ya hivyo imeoneshea kwamba wanaume tunakufa wengi zaidi kuliko wanawake. Mwaka huo tumezaliwa wengi lakini hata kufa wanaume tunakufa wengi zaidi kulikoni wanawake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nikubaliane na mawazo ya wenzangu asubuhi hapa kwamba ni vyema Masheha wafanye kazi ya ziada. Kwa sababu hakuna kijiji kilichokuwa siyo Shehia au Sheha hawezi akafariki mtu ima mtoto au mtu mzima, Sheha wa Shehia hiyo akakosa kupata taarifa. Kwa hivyo Masheha ni nafasi peke yake ambayo inaweza kusaidia kutoa taarifa hizi za kizazi na kifo.

Mhe. Spika, na hasa kwetu vijijini itokezee mtu kuna ajira, anatakiwa kama baba yake kishakufa apeleke kile cheti cha kuthibitisha kama mzazi kishakufa, hapo ndiyo mtu atakaposhughulika kutafuta cheti kile cha kifo cha mzazi yake ambaye tayari kishafariki. Lakini si aghalabu wananchi wetu kulifanya hili kwamba kwao ni la umuhimu kutafuta hivi vyeti vya kifo, si rahisi kwa hilo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ni vyema tukaona ili takwimu hii ya kizazi na kifo, hasa kwa wale waliofariki inakwenda vizuri kama inavyopatikana katika hivi vizazi.

Inaweza ikaisaidia Serikali na Serikali ikaweza kujua kwamba kila mwaka watu wanaofariki ni wangapi na kila mwaka watu wanaozaliwa ni wangapi, ili hesabu ya Serikali ikawepo vizuri sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije Wakfu na Mali Amana. Mhe. Spika, hii ni Idara moja nzuri na shughuli zake ni nyeti sana. Ukiangalia Mhe. Spika, watu wengi wameeka Wakfu ima mashamba yao, majumba yao, ardhi zao na mambo mengine mbali mbali. Lakini Mhe. Spika, ukiangalia majumba mengi yaliyowekwa Wakfu sasa hivi hali yake ni mbaya sana, yanahatarisha hata wale watu wanaoishi katika majumba yale.

Hivyo wenzetu Mhe. Spika, walifanya jambo la kheri, wao na kwetu sisi kwa sababu sisi tunapata faida vile kuwaendeleza watu kuweza kuishi. Lakini katika kuishi huko na pia inazalisha kwa sababu watu wanaishi, kwa hivyo Serikali nayo inafaidika. Lakini kutokana na majumba jinsi ya hali yake yalivyo, hii hali imekuwa ni dhaifu sana na maeneo ambayo yanahatarisha maisha ya wananchi wetu.

Kwa hivyo bado niiombe Serikali ifanye inavyoweza angalau kukarabati baadhi ya haya majumba ili yawe katika hali anayoweza kuishi mwanadamu. Kwa sababu thamani ya mwanadamu ikipotea, hakuna mwenye uwezo wa kuirejesha na thamani kubwa ya mwanadamu basi ni roho ya Mungu aliyenayo. Kwa sababu ikitoka roho ninalobakia ni boksi tu, hapana mwengine yeyote atakayesema ngoja tufanye maarifa *body* hii tuifanye tuirejeshee hii roho, si rahisi hakuna hilo Kwa hivyo, kusema kwetu kuringa kwetu kufanya mambo yetu ni kutokana na hii roho ambayo Mwenyezi Mungu aliyetupa ili tuweze kuishi na *alhamdulillahi* lakini ndiyo ikitoka ndiyo imetoka.

Kwa hivyo katika maeneo yale baadhi ya watu wanaoishi katika majumba haya ya Wakfu, kwa kweli roho zao zimo katika hali mbaya sana katika kuishi majumba yale. Hivyo, ningeliomba sana Wizara ilione hili na yale ambayo kwamba hayawezi kuweza watu kuishi tena, basi isione muhali kuwahamisha watu wale na Serikali ikaanza kufanya ukarabati ili yaweze kwenda na wakati tulionao.

Mhe. Spika, lakini pia niseme katika Ofisi hii ya Wakfu na Mali Amana, nilikuwa na wazo la muda mrefu lakini Mhe. Panya Ali Abdalla asubuhi hapa pia na yeye amelisema, kwa hivyo na mimi nimepata faraja nikasema nikipata nafasi basi na mimi nilitilie mkazo.

Mhe. Spika, ni suala zima la Hijja. Hijja bado hapa Zanzibar hatujaipa umuhimu wake, bado ni suala linalofanywa kwamba aah! ni atakayekuwa na uwezo tu ndiye atakayekwenda kuhiji, *Manistatwaa Ilayhi sabiila.*

Mhe. Spika, uwezo wa watu kwenda Hijja upo mkubwa tu, na watu wanajipangilia katika maisha yao, kufanya mambo yao ya kidunia mbali mbali na yote yanakwenda katika vile alivyoyapanga. Kwa nini ukosekane uwezo wa kwenda kuhiji, mimi bado nasema uwezekano huo upo, ni taasisi tu husika ikajipanga na kuweka mfuko wa kumfanya kila mfanyakazi wa nchi hii na kila mfanyabiashara ambaye ataona na yeye ajiunga na mfuko huu, basi uwezekano wa kuzalisha Mahujaji upo mkubwa sana na kuwasaidia wale wengine ambao hawana uwezo kabisa. Hili jambo tumeliweka nyuma kwa muda mrefu, lakini hakuna sababu mfanyakazi wa serikali wa nchi hii, akakosa kwenda Hijja kwa kupitia njia hii ya mfuko, hakuna sababu Mhe. Spika.

Kwa hivyo, pesa zipo na mimi naamini kama huu mfuko utaanza mwaka huu 2015/2016, basi mwakani watu wataanza kwenda Hijji kwa kupitia mfuko huu, lakini ni jambo ambalo hatujalipa uzito. Kila mara hapa Tanzania tunaambiwa karibuni watu 2000 wanatakiwa waende wakahiji Makka, lakini hatujafika takwimu hiyo, nafasi tunazo lakini bado zinazoendewa hatujazifikia. Lakini mimi naamini Mhe. Spika, kama serikali itaamua kweli kuanzisha huu mfuko wa Hijja, basi ni hatua moja wapo ambayo tutafika lile lengo tunalotakiwa twende na tutatafuta na ziada.

Kwa sababu jambo lolote linahitaji kuhamasishwa, mimi naamini kama hawa wafanyakazi wetu watahamasishwa vizuri, basi uwezekano wa kuchangia mfuko huu na watu wakenda kuhiji na hatimayake wakasaidia na wengine, basi uwezekano huo utakuwa upo kwa hapa kwetu Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri, hili wazo

**Mhe. Spika:** Unamalizia kwa dakika tano.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Ahsante. Hili wazo alifanyie kazi ili tufike malengo ya kufikia katika hatua hiyo. Mhe. Spika, mimi nakushukuru sana, kwa hivyo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kusema machache sana, katika hoja ya Mhe. Waziri iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kabla ya kuingia katika hoja hii, kwanza natumia fursa hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uhai na hatimae kutujaalia neema ya uzima, afya na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu mpaka katika hili jengo, haya ni mapenzi makubwa ya *Allah* kwetu na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na timu yake ya ufundi, kwa kuweza kututayarishia kitabu hiki cha hotuba na yeye kuisoma kwa umakini mkubwa, kwa kutumia saa moja na zaidi katika kuiwasilisha hapa, tena kwa utaalamu mkubwa, kwa hivyo nampongeza sana.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo fupi, naomba sasa niende moja kwa moja katika hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 18 wa kitabu cha Mhe. Waziri ameelezea kuhusu Ofisi ya Mufti. Ofisi ya Mufti ni ofisi muhimu sana kwa mazingira ya Zanzibar, basi Ofisi ya Mufti ni ofisi muhimu sana, kwa sababu karibu asilimia 100 ya Wazanzibari ni Waislamu na ofisi hii kwa sababu miongoni mwa kazi zake ni pamoja na kusimamia shughuli za Misikiti pamoja na Madrasa.

Huu ndio utamaduni na silka za Kiislam chem chem zake ziliko katika Miskiti na Madrasa. Miskiti na Madrasa ya Zanzibar inapatikana katika maeneo ya miji pamoja na vitongoji, vijiji pamoja na vitongoji. Sasa ndio kusema kwamba Ofisi ya Mufti ina kazi ya kupenya kila kipembe cha nchi hii, ili kuona kwamba Miskiti pamoja na Madrasa zimo katika mazingira mazuri pamoja na kuendelezwa.

Mhe. Spika, mimi nilidhani kwamba ofisi hii ingekuwa na programu maalum, ndani ya programu kubwa kungekuwa na programu ndogo ya kuweza kuimarisha Miskiti na Madrasa kwa msingi wa kujenga mila na silka za Kizanzibari. Lakini inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba Ofisi hii ya Mufti Mhe. Waziri kaifumbia macho sana. Mhe. Spika, nataka upate siku wewe ukatembelee kisiwa cha Pemba, uende katika Ofisi ya Mufti pale Pemba uone jinsi ya lile jengo lake lilivyokuwa halina viwango, ile ofisi yao ilivyokuwa haina viwango.

Halikadhalika Mhe. Spika, baada ya kufanya utafiti wa kina sana na upembuzi yakinifu, nimeona Ofisi ya Mufti Pemba hata usafiri haina, huku kukiwa na Misikiti mingi Bogoa, kukiwa na Misikiti mingi Nanguji, kukiwa na Misitiki mingi Kiwani, kukiwa na Misikiti mingi sana sehemu za Mwambe, kukiwa na Misikiti mingi sana Konde, kukiwa na Misikiti mingi sana Ungi Msuka, kukiwa na Misikiti mingi sana Chake Chake pale. Inatakiwa itembelewe ili kuona kwamba Misikiti ile inakuwa mizuri, pamoja na Madrasa, shughuli za Madrasa zinakwendaje.

Mhe. Spika, kama hayatoshi hayo njoo kisiwani hapa Unguja uone, sehemu za Mtende kule kuna Madrasa nyingi sana na Makunduchi zinataka zitembelewe na Ofisi hii ya Mufti, lakini ukiangalia hawana usafiri. Kule Pemba wana kigari cha Naibu Mufti nacho ni kibovu, Pemba nzima ni kigari cha Naibu Mufti na ndio kibovu, sasa watafikaje Bogoa, watafikaje Makunduchi na sehemu nyengine kwa kigari kile.

Inasikitisha sana na inaonekana kwamba Mhe. Waziri ofisi hii hataki ilinde mila na silka pamoja na maadili ya Kiislamu kwa kuweza kuimarisha Madrasa na Misikiti. Kwa sababu hata bajeti ya kununua gari humu kule Pemba wala bajeti ya kununua gari hapa Unguja hatujaiona humu ndani, ana siri gani na ofisi hii Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, hayo tisa tu, njoo zako katika *OC*. Pemba walipangiwa kupatiwa *OC* shilingi milioni 80 katika kipindi hiki, mpaka mwezi huu wamepatiwa shilingi 25 milioni, kwa habari nilizonazo za haraka haraka, ni asilimia sijui 20 ya fedha ambazo walikuwa waingiziwe kwa ajili ya kufanya mambo hayo, unatakiwa kutoa fatwa Makoongwe.

Ofisi ya Mufti kuna ugomvi kule chungu nzima, katika kisiwa cha Makoongwe sehemu za Uvinje huko na sehemu nyengine, wanatakiwa Ofisi ya Mufti waende kwa kutumia mashua, iende kwa kutumia boti, alimradi ni tatizo. Wanategemea hizo *OC* Mufti aweze kwenda kukodia mashua kuelekea sehemu za Tumbatu kwenda kutoa fatwa, atumie *OC* hii hii kwenda kutoa fatwa sehemu za Bogoa, kule sehemu za Chokocho, Bogoa aende akatowe fatwa, *OC* mpaka sasa ni asilimia 25 hawana hata lolote pale ofisini za kuweza kutilia mafuta. Mhe. Waziri hiyo si dharau ofisi kubwa kama hii?

Mhe. Spika, mimi nadhani ofisi hii ni lazima tuiangalie sana, ofisi hii katika kisiwa kama hiki chenye Waislamu wengi na dini nyengine zipo, lakini Waislamu ni wengi. Ilikuwa angalau wawe na ofisi nzuri tu ya kuweza kuwakaribisha wageni mbali mbali, hususan zile nchi za Ghuba wanakuja hapa, wakija Pemba pale ile ofisi yao ilikuwa ikivuja, ukienda pana michirizi inavuja vuja mule ndani.

Hivi karibuni alikuja Mufti wa Oman, sijui hata walimkaribisha wapi, nilimuona kachukuliwa na jamaa zake humo pembezoni, wakati alikuwa afikie katika ofisi pale akasaini. Sasa hiyo sio kuitia aibu ofisi tu, lakini mpaka serikali yetu wanaitia aibu, kwa sababu kuja mgeni wakamkaribisha katika kivuru, maana kile ni kivuru Mhe. Spika. Ile kule Pemba ni kivuru. Waliokuwa hawajui neno kivuru ni kibanda cha mgongo ambacho kinakandikwa kwa udongo na kuezekwa kwa makuti ndio kivuru hicho.

Sasa Mhe. Spika, hakitofautiani na ile Ofisi ya Mufti iliopo pale Pemba. Sasa yule Sheikh Harith mimi niliuliza kakaribishwa wapi siku ile, kumbe walimchukua jamaa zake pembeni, ni aibu Mhe. Waziri. Hebu tueleze Mhe. Waziri utakapokuja.

Je, una mpango gani wa kuimarisha Ofisi ya Mufti kwa kuweza kuwapatia ofisi iliyokuwa ya kisasa kabisa, *computerised*, ambapo wakija wageni kutoka Sharja, wakija wageni kutoka Oman, wakija wageni kutoka nchi kadhaa za Kiislamu kuja

kuitembelea ile ofisi na wao watajisikia wamekuja katika nchi ambayo nayo ina Waislamu wengi.

Mhe. Spika, sasa niende katika Mahakama. Mhe. Spika, kama kuna chombo ambacho ni moyo, sio kwa kutoa haki tu. Lakini katika kusimamisha utawala bora katika nchi, basi ni hii mahakama. Mahakama Mhe. Spika, ni chombo muhimu sana na kwa bahati sisi Zanzibar hapa chombo cha Mahakama kipo, tuna Bunge hili na tuna hawa *executive*. Sasa vyombo hivi vilitakiwa viwe makini sana katika suala zima la kuleta utawala bora katika nchi.

Inasikitisha Mhe. Spika, katika Mahakama ya Zanzibar kuna tatizo kidogo. Mhe. Spika, dhamana ni haki ya kila mshtakiwa, ni haki ya kila mshtakiwa ku-*bail*, lakini kuna wakati Hakimu anashindwa kutoa *bail* kwa sababu ya kuona mazingira hayaruhusu kutoa dhamana. Mimi Mhe. Spika, sio mwanasheria, sijui mara hii, lakini mara nyingi huwa nakamatwa napelekwa Mahakamani, ninao uzoefu katika hizi Mahakama zetu za Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nina uzoefu kidogo, mara nyingi kesi zinapoonekana zina tatizo kwa ajili ya mambo ya kutaka kuhatarisha amani na utulivu, basi Hakimu anafunga *bail* kwa mshtakiwa yule. Mimi imeshanitokezea mara kadhaa, japokuwa nabambikiziwa makosa ambayo naambiwa nahatarisha amani na siku nyengine hujikuta sipati *bail* wiki tatu au mwezi. Hata nikipelekwa huko Mahakamani naambiwa nashtakiwa kwa uzembe na uzururaji, lakini huku kesi niliyofunguliwa awali nahatarisha amani ya nchi nanyimwa dhamana.

Hivi karibuni tu Mhe. Spika, Hakimu mmoja pale Pemba juzi tu tarehe 27, sijui kama ni tarehe 26 au 27, lakini alizuwia dhamana kwa watu wafuatao. Khamis Masoud Hamad, huyu ni Afisa Uchaguzi Msaidizi wa Wilaya ya Micheweni, halafu akazuwia dhamana kwa Mbwana Shaame Afisa Elimu Wilaya Micheweni huyu, halafu bwana Bakar Khamis Juma ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Shumba Mjini. Leo kama ni siku ya tatu tangu azuwie ile *bail* kwa sababu ya kuhofia uvunjifu wa amani.

La kusikitisha sana Mhe. Spika, ni kwamba hawa watu walikwenda na zogo kubwa sana nyumbani kwa bwana mmoja pale Kwale na mapamba. Sasa Hakimu akaona busara tu kwamba hawa watu niwazuwie kusudi watu wa Kwale wasije wakahatarisha amani. La kusikitisha Mhe. Waziri litakalotokea pale Kwale wewe utakuwa mas-ul. Hakimu amezuwia *bail*, lakini leo wale watu wametolewa Rumande na wakapita na mabeni katika eneo lile la pale Kwale na kuanza kuwafanyia ishtizai yule bwana mwenye nyumba, jambo ambalo vurumai wakati wowote linaweza likasababishwa tena pale.

Sasa waziri ambaye naona tabu kumuambia sana ni mzee wangu hapa Mhe. Abubakar Khamis, nataka unipe maelezo ya kina. Kwa nini Mahakama imeweza kumpa dhamana wakati ile kesi ni nyeti namna ile na yeye mwenyewe alikwisha izuwia, kuna nguvu gani iliyotumika pale mpaka ikapatikana dhamana ile na ishtizai zikaendelea kufanyika Kwale, jambo ambalo wakati wowote linaweza likahatarisha amani na utulivu pale. Naomba maelezo Mhe. Abubakar Khamis.

Mimi nasikitika sana Mhe. Spika, ikiwa utaratibu wa kuingilia mashtaka Mahakama upo, basi sisi tumeonesha uzembe mkubwa sisi Waislamu wa Zanzibar, kwamba watu wamezuiwa siku mbili tu na Hakimu na zikenda nguvu na Hakimu akashindwa na akatoa dhamana. Leo kuna Masheikh wale wanadhalilika rumande, hadi leo hii hatujafanya lolote.

Sasa kama kuna nguvu basi Waislamu tujikusanyeni tukawatowe Masheikh wetu kule jela, katika utaratibu huu huu waliotolewa watu wa Kwale. Hapa nawaomba sana Waislamu tushikamane na sisi kama utaraibu uliotumika Kwale ni mzuri na sisi tukautumie utaratibu ule ule kuwatoa Masheikh wetu walioko katika kizuwizi kule.

Mhe. Spika, twende katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni ofisi muhimu sana. Lakini inasikitisha vitendea kazi hawana hawa wenzetu. Ukiangalia gari walizokuwa nazo pale ni mbili, moja ni mbovu kabisa wanatumia zaidi gari moja, kwa ajili ya kwenda Micheweni, Wete, Mkoani. Sasa ninachoomba Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hususan kule Pemba, waangaliwe kwa jicho la huruma, ili wapatiwe vitendea kazi na waweze kuzisimamia kesi.

Kesi zinakwama kwama kwa sababu ofisi haina vitendea kazi, napenda niwasifu sana kwamba kutokana na kigari kile kile wanajitahidi. Lakini jitihada yao humalizia wakati mwengine kesi kuwazidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri ofisi yake itupie macho Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Halafu Mhe. Spika, nilikuwa naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa uje unifafanulie kidogo katika mambo ya maslahi hapa, ukiangalia wafanyakazi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kimaslahi yaani kitaaluma na mahakimu hawakutofautiana, lakini kimaslahi ni tofauti sana, hebu ukija tueleze kwa nini mtu mwenye *first Degree* akiwa ni Hakimu wa Wilaya kimaslahi anakuwa mbele zaidi kuliko hata mtu mwenye *Masters Degree* ambaye yeye yupo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Sasa naomba uje utupe ufafanuzi inasikitisha kwamba hawa watu wana taaluma ya aina moja kiwango sawa sawa cha elimu lakini maslahi wako chini wanatukimbia sana hawa.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa na kwa kuwa mimi si msemaji sana katika mambo haya ya sheria naomba sitaki niunge mkono kwanza mpaka utakapokuja kunieleza hili tatizo la Kwale na dhamana iliyotolewa. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji wapatao wanne na nilikuwa nataka nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu ikifika kunako saa 12.30 au pengine na robo aanze kumsaidia Mhe. Waziri na hatimae tumwite Mhe. Waziri, hivyo naomba tutumie dakika kama kumi kumi ili kuweza kufika pahala tunapohitaji nataka niitumie hii nafasi ya akidi kiasi iliyopo na wengine wanakuja wako njiani tuweze kumaliza maana mahudhurio yetu kwa kweli sio mazuri. Sasa unapoona kidogo tumekusanyika kusanyika basi uitumie hiyo nafasi hapo hapo ili tuweze kumaliza mambo yetu vizuri.

Naomba basi sasa kwa kutumia dakika kumi kumi nianze kumkaribisha Mheshimiwa Hamza Hassan Juma baadae afuate Mhe. Hija Hassan Hija. Mhe. Hamza.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi kwa upande wangu nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nijitahidi dakika kumi niweze kuzitumia vizuri, kwa kuanzia kwa kuokoa muda nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote katika Afisi yake pamoja na zile taasisi zilizo chini yake.

Mhe. Spika, nataka kutoa shukurani zangu za dhati kama kawaida yangu mimi Mhe. Waziri namkubali sana na namkubali kwa sababu unapojenga hoja ikiwa ya msingi basi kwa kweli anaifanyia kazi, nashukuru sasa hivi angalau suala la *scheme* kwa majaji wetu pamoja na Mahakimu wa zile Mahakama za mwanzo angalau kidogo zimekuwa na afueni.

Kwa hivyo nakupongeza sana Mhe. Waziri na uendelee na moyo huo huo wa kutusikiliza na kile kilio chetu kinapokuwa cha msingi basi uweze kukifanyia kazi. Halikadhalika pamoja na yale malipo ya wale ma- *assessor* ambao kwa muda mrefu sana walikuwa wakilalamika huko mitaani.

Mhe. Spika, na mimi nataka niungane alipoachia swahibu yangu, mkwe wangu maalim Salehe hasa alipozungumzia Mhe. Spika, ninaposema Mkwe wangu mkwe wa kweli kweli huyu sio wa juu juu, kuhusu suala la Ofisi ya Mufti katika Ofisi sasa hivi tunatakiwa Serikali tuikazie sana kuingizia fedha ni Ofisi ya Mufti. Mhe. Spika, sasa hivi ukiangalia maadili kila siku zikienda maadili yanamong'onyoka humjui mkubwa humjui mdogo, sasa kwa kweli Mashekhe lazima watusaidie sana sasa hivi washuke mitaani kama alivyosema maalim Salehe, bila ya nyenzo hawawezi kutufikia ili waje kutoa taaluma angalau kurejesha maadili katika nchi yetu.

Chengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka niseme kwamba Ofisi hii ya Mufti ina kazi kubwa sana na moja katika kazi yao kuhakikisha kwamba Miskiti yetu na madrasa zetu zinakuwa katika hali nzuri, lakini vile vile kuondoa au kusimamia migogoro mbali mbali inayojitokeza katika misikiti katika kipindi hichi cha sasa hivi, sio migogoro mingi ambayo inakuwa inajitokeza kw hivyo tunawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Sasa nilikuwa naomba jambo moja sasa hivi dunia imeharibika na baya zaidi sasa hivi kila ukiwa muislam basi duniani unakuwa unaangaliwa katika macho matatu, maana yake baada ya yale mawili basi kuna na jengine linakumurika. Sasa tumekuwa na utamaduni mashehe wetu waalimu wetu huwa wanatoka wanakwenda nchi mbali mbali na wao vile vile huwa wanatembelewa katika maeneo yetu, sasa Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana Ofisi hii ya Mufti iwe inajaribu kuratibu sana shughuli zote za mashekhe wetu hawa au wanavyuoni wanaotoka kwenda katika zile fisabilillahi kuweza kurekodi.

Vile vile wanapotembelewa waweze kuwa wanarikodi ili pasije pakaanza kuingia mikono mikono Mhe. Spika. Hivi karibuni nilianza kuletewa malalamiko kwa mashekhe wangu fulani walikuwa na wasi wasi kwamba huenda labda wakazuiliwa wale wageni wao wasije hasa baada ya kutokezea matukio matukio katika maeneo ya Mombasa.

Sasa mimi nilikuwa naomba si busara kuweza kuwazuia hawa Mashekhe wetu kutembeleana kwa sababu hata Serikali, vile vile wanatembeleana wanakwenda katika mikutano huko ya kimataifa wanarudi na wageni wanakuja wanafanya mikutano yao, na wao si busara kuweza kuwazuia lakini iwe katika utaratibu maalum wa uangalizi wa hali ya juu. Kwa kweli tunawatakia mema Mashehe wetu ili waweze kufanya kazi zao kwa vizuri.

Chengine Mhe. Spika, nilikuwa naomba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, wana rasilimali ambazo walizoachiwa na watu tofauti tofauti aidha wakfu mtu alioandika au wakfu wa urithi wa femilia, sasa mimi nilikuwa naomba kuna majumba au maeneo ambayo waliachiwa Kamisheni ya Wakfu nilikuwa naomba sana sasa hivi wasiwe rahisi sana kuyaruhusu maeneo yale kuyatoa tu hasa katika bei nafuu.

Mimi nadhani sasa hivi wakati umefika Kamisheni ya Wakfu basi wajaribu kuangalia na kuzungumza na hizi taasisi za kifedha kuweza sasa baada ya majumba yale kuendelea kuyakodisha katika hali dhaifu, basi wanaweza wakazungumza na taasisi za fedha hasa yale majengo yaliyokuweko mjini

wakayajenga upya yakawa bora zaidi na wakaweza kukodisha katika kiwango kikubwa.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana kwa sababu ukiangalia Kamisheni ya Wakfu imekuwa wao wanarithi halafu na wao wanakodisha lakini katika hali ambayo iko dhaifu sana, kwa hivyo naomba basi wajaribu kutafuta wachumi waangalie zile rasilimali zao walizokuwa nazo waangalie watayaboresha vipi, ili waweze kuingiza fedha zaidi kwa kuweza kusaidia yale malengo yaliyokusudiwa.

Chengine Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuangalia katika kitabu huu ukurasa wa 10 Mhe. Spika, samani ni ukurasa wa nane Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia hapa katika kipindi hicho ambacho kilichotajwa hapa kipindi cha Julai hadi Machi 2014 kuna mdorongo wa kesi ambazo zilipelekwa Mahakamani, hapa naambiwa mashauri mapya Mei, 1 ni 63 lakini vile vile ukijumuisha mashauri 116 yamekuwa jumla ya mashauri 279, mashauri manne yametolewa uamuzi, katika Divisheni ya Mahakama ya Kazi yamepokelewa mashauri 11 na kuifanya Divisheni hiyo iwe na mashauri 18 kujumisha na masharti saba yaliyosajiliwa kabla. Hakuna mashauri yoyote yaliyotolewa maamuzi katika Mahakama hiyo.

Sasa Mhe. Spika, kwa kweli hili jambo bado halipendezi sana inaonesha bado kuna uchereweshaji wa hizi kesi sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Spika, tumsaidie Waziri, ili kuondoa kadhia hii tuangalie *performance* ya Majaji wetu. Mimi nafikiri lazima kuwe na *assessment* ya kuwafanyia Majaji, je Jaji fulani katika muda fulani amepokea kesi ngapi na kesi ngapi ameweza kuzimaliza. Mhe. Spika, kesi hizi zinapochukua muda mrefu kwa kweli nachukua ule msemo ambao Mhe. Waziri kipindi hicho alipokuwa kama mimi huku niliko *backbencher* alikuwa anazungumza sana, kwamba *Justice delay justice deny*. Mheshimiwa basi msemo ule sasa hivi hebu tunaomba uvalie njuga ili uweze kuondoka, ili ile haki iweze kutendeka.

Mhe. Spika, nikiendelea nilikuwa najaribu kuangalia kwenye usajili wa wakala wa biashara….

**Mhe. Spika:** Bado dakika tatu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, hapa kidogo kuna tatizo katika suala la usajili wa wakala wa biashara, huku bado kuna tatizo sasa hivi hapo ukiangalia Mrajis bado *vote* yake iko chini ya Katibu Mkuu kwa hivyo utakuta hapa fedha kunakuwa hakuna, wakati mwengine na hii wakala wa usajili wa biashara Mhe. Spika, kuna ma - *investors* wanakuja kuin-*vest* biashara kubwa. Kwa hivyo wakati mwengine wanakwenda pale unaambiwa *printer* haina wino sasa mimi nilikuwa naomba kwamba huyu Mrajis hasa katika hii Taasisi hii ya Usajili wa Mahakama

basi *at least* wawe na *account* yao maalum ambayo itakuwa *independent* ambayo itaweza ku-*operate* muda wote, wafanyabiashara Mheshimiwa si watu wanaotaka njoo kesho njoo halafu, kwa hivyo nilikuwa naomba hili kwa kweli liweze kushughulikiwa.

Jengine Mhe. Spika, kwa haraka haraka Mahakama ya Ardhi Mheshimiwa, Mahakama ya Ardhi sasa hivi tunashukuru wanashusha mpaka katika Wilaya lakini bado katika ile sheria tulivyopitisha kulikuwa kuna kanuni Mhe. Spika, kesi za Mahakama ya Ardhi nyingi zinacherewa kwa sababu ile sheria ukiangalia ina ugumu wake, kwa hivyo tunamuomba sana Mhe. Waziri hizi kanuni aweze kuziharakisha ili kuweza kuwapa wepesi wale Mahakimu wa kuweza kufanya maamuzi kwa haraka.

Mhe. Spika, Mahakama ya biashara hili moja katika jambo ambalo linarejesha nyuma sana wafanya biashara Mahakama ya biashara, na hii Mahakama ya Biashara sijui kama imeshaanza kazi, lakini sheria ilishakuja tulikwisha kuiptisha lakini mpaka leo sijui kuna tatizo gani.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, kabla hujaniambia nikae kuna hii taasisi yetu ya wanasheria wa kujitegemea mpaka leo ukiangalia taasisi ile iko kama *NGOs* na wenzetu wote tumejaribu kuangalia katika Nchi za Afrika ya Mashariki Mhe. Spika, ndani ya sheria imeelezewa sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, basi na kwa bahati nzuri kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba na sisi kidogo tunajisomesha somesha sheria, tunapoona tunakwama tunapitia kidogo tunatoroka lakini bado tunahudhuria.

Sasa tunamuomba sana Mhe. Waziri kama ingelikuwa Baraza hili tutakuwa tuna miezi mingine mitatu tutakuja hapa ningelimuomba Mheshimiwa akaleta Mswada akasoma kwa mara ya kwanza mswada ambao utaifanya ile taasisi ambayo sasa hivi inahisabika kama ni NGOs iwe ndani ya sheria, ili na wale mawakili... Mheshimiwa sasa hivi Mawakili hawana mwamvuli, wapo wapo tu kila mmoja anafanya kivyake. Kwa hivyo hata ile nidhamu ya mawakili wetu Mhe. Spika, hakuna *umbrella* ambayo ipo kisheria inayotaka kuwa-*guide* na ikitokezea wale inataka kuwa- *guide* wanasema aa, nyinyi mko kama nini hamko katika sheria, nyinyi kama NGOs na ukiangalia ni kweli.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri nafikiri nimejaribu kusema haraka haraka lakini kwa kweli Mwanasheria naamini atajua nimekusudia kitu gani, na kama atakuwa hakunifahamu vizuri basi katika zile programu zile kidogo nitakuja kuzuia zuia lakini zaidi kwa kupata ufafanuzi.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba nitoe taarifa kabisa kwamba siungi mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, na siungi mkono kwa sababu ya maeneo manne kila ambapo lipo fungu la Afisi ya Mufti siungi mkono, kila ambapo lipo fungu la Mahakama siungi mkono, kila ambapo lipo fungu la Mrajis wa Vizazi na Vifo siungi mkono, na kila ambapo kuna Ofisi ya Wakala wa Usajili wa biashara na mali siungi mkono.

Kwa hivyo maeneo haya manne Mhe. Spika, naomba niseme kabisa kwamba sitopitisha bajeti hii mpaka pale Mhe. Waziri atakaponipa maelezo ya kutosha kwa maeneo haya manne.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wangu huo nataka niseme kwamba ukurasa wa 20 Ofisi ya Mufti *paragraph* 65 naomba ninukuu;

"Mhe. Spika, Mashirikiano mema na taasisi nyengine za kidini ndani na nje ya nchi hukuza udugu kwa waumini, afisa wa Mufti kwa ushirikiano na Kamati ya Amani na Utulivu pamoja na Taasisi ya *Friends of Zanzibar* imefanya mikutano miwili Unguja na mmoja Pemba; mikutano hiyo ililenga kusisitiza kuwepo kwa umoja, mashirikiano, amani na utulivu katika nchi yetu".

Mhe. Spika, nimefahamu kwamba ofisi ya Mufti kumbe mbali ya kazi zake nyengine za kidini lakini pia inafanya kazi ya kujenga misingi ya amani, sasa amani Mhe. Spika, ina viashiria vyake kwa mtazamo wangu Mhe. Spika, Ofisi hii bado haijafanya kazi ipasavyo wanajaribu kujenga ukuta lakini wanashindwa kuziba ufa, sasa hatuwezi kusubiri kujenga ukuta kwa kuacha kuziba nyufa mbali mbali.

Kwa mtazamano wangu Mhe. Spika, nimesema tokea juzi na leo nasema kwa nchi inavyokwenda bila ya kuchukuliwa tahadhari za msingi Ofisi ya Mufti na Serikali nzima na Wazanzibari wote wanakabiliwa na changamoto ya tishio la amani. Ofisi hii ya Mufti kwa mtazamo wangu ingezungumza na wanasiasa na ninaposema wanasiasa maana yake zaidi ni wale viongozi wa CUF na CCM wawakumbushe wajibu wao kujenga misingi ya amani, viashiria vinaonesha kwamba huko mbele kama hatukuwa makini basi Zanzibar watajenga ukuta badala ya kuziba ufa. Badala ya kutoa mawaidha msikitini kuwaambia wale wa msikitini kwamba njoni mswali, nadhani washuke chini kwa viongozi na wanasiasa wajenge misingi ya amani kusudi malengo ya Afisi hii yafikie kipeo ambacho wamekusudia.

Hoja yangu ya pili kwa Ofisi hii zipo taarifa kwamba yako baadhi ya maskuli binafsi wamekuwa na utaratibu wa kulazimisha mapishi mwezi wa Ramadhani, miezi yote hii 11 hawapiki, lakini unapoandama mwezi wa Ramadhani wamiliki wa skuli zile wanalazimisha kupika na wanafunzi kula na walimu kula. Ofisi ipo na maelezo hayo yanajulikana, hakuna hatua inayochukuliwa. Hii ndio sababu ambayo naomba Mhe. Waziri anieleze vyenginevyo fungu lile la Ofisi ya Mufti, nitalizuia kwa nguvu zangu zote.

Mhe. Spika, hoja yangu ya tatu, niende Ofisi ya Mahakama na niungane mkono na ile hoja ya Mhe. Saleh Nassor Juma, kwamba mara nyingi tumekuwa tukilaumu Mahakama na mimi silaumu Mahakama *in such*. Mahakama zinaongoza kisheria, nalaumu viongozi wa kisiasa kulazimisha nguvu Mahakamani. Naamini kwamba Mahakama zina uledi mkubwa na Mahakimu wetu na Majaji wetu wana uwezo mkubwa wa kutumia haki. Lakini Mahakama zetu zimekuwa si huru kwa sababu viongozi wa kisiasa wamekuwa wakiingilia.

Mfano wa Mhe. Saleh Nassor, aliyoutoa wa Kesi ya juzi Micheweni, mfano ule umekwenda kwa nguvu ya viongozi wa kisiasa. Hakimu aliamua maamuzi halali kwa mtazamo wake, lakini ushahidi umeonyesha kwamba viongozi wa kisiasa wameondoka hapa kwenda Pemba wameshindikiza Hakimu abadilishe maamuzi. Huu sio utawala bora, huu sio uongozi bora na huu sio uwadilifu.

Kwa hivyo, mkiwa mnao uwezo wa kutoa maamuzi kwa Mahakimu kwa kesi A, kwa nini mshindwe kutoa uwamuzi wa Mahakimu kwa kesi B. Ndiyo maana tukalalamika kwa nini mashehe watiwe ndani karibu mwaka mmoja serikali hamjachukua hatua? Kwa msingi huo mnawafanya Mahakimu wetu sasa waonekane kwamba wanapendelea kumbe mnawalazimisha kisiasa. Mhe. Spika, kwa msingi huo siungi mkono fungu hili la pili.

Mhe. Spika, fungu la tatu, Ofisi ya Msajili wa Vifo na Vizazi siungi mkono kwa sababu mambo yote makubwa ya dini ya Kiislamu, funga, zaka, Hija na swala yanaratibiwa na Ofisi ya Mhe. Waziri na hayo ndio mambo ya dini. Lakini wameshindwa kutoa haki ya vyeti vya kuzaliwa kwa Wazanzibari. Wanahubiri dini, lakini haki ya msingi ya kuzaliwa wanainyima.

Kwa hivyo, mimi siungi mkono fungu hili kwa sababu ni dhahiri kwamba wanapendelea upande mmoja. Kwa nini unahubiri amani lakini mkononi una panga, haiwezekani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili siungi mkono kwa misingi hiyo, kwamba inaonekana kwamba mnafanya *bias.* Mnazungumza amani upande mmoja lakini mnazungumza mambo yenu kwa upande mwengine hatimae Wazanzibari wanakosa haki na wanaposa haki Mhe. Spika, maana yake unasababisha viashirio vya kuvunjika kwa amani katika nchi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa siungi mkono fungu la Mrajisi wa Makampuni na ni kwa sababu moja tu, nipate maelezo ya usajili wa *transworld*. Bado kuna malalamiko kwamba Kampuni ya *Transword* Zanzibar imesajiliwa kinyemela. Nipate maelezo ya fungu hili ndio hapo tupitishe bajeti hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo na hadi pale Mhe. Waziri, atakaponipa majibu sahihi, siungi mkono hotuba hii. Nakushukuru.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, na mimi nashukuru tena nashukuru sana kwa kupata nafasi hii adhimu ya kuzungumza machache tu katika hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2015/16 ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, mimi leo sitokuwa na mengi na kwa sababu hiyo moja kwa moja naanza kuhusu vyeti vya kuzaliwa. Mhe. Spika, hali ilivyo hivi sasa ni kwa vyeti vya kuzaliwa vina umuhimu wa aina yake na bila ya vyeti hivi vya kuzaliwa kwa wale ambao wanahitaji kupiga kura hawawezi wakapata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na bila ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi huwezi kuwa na kitambulisho cha kupigia kura. Hii ni sawa na kwenda kinyume na kifungu cha Katiba kinachoeleza kuwa kila Mzanzibari mwenye kutimia umri wa miaka 18 na mwenye kukamilisha masharti anayo haki ya kupiga kura.

Mhe. Spika, kulitokea mabadiliko hapa katikati ya kuwa hawezi kuwa mtu mpiga kura kwa uchaguzi huu wa Zanzibar mpaka awe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kitambuliso ambacho kimo katika sheria Nam. 7 ya mwaka 2005, katika sheria hii ukiangalia kifungu cha 6 kinasema kuwa;

"Kazi za mkurugenzi anayehusika na vitambulisho kwa mujibu wa sheria hiyo atafanya kazi kwa sheria hiyo na vile vile kwa kufuata maelekezo yatakayotolewa na Waziri husika."

Kwa vyovyote vile wananchi ambao zamani walikuwa ni wapiga kura kundi kubwa pia lilibidi likose haki yake kwa sababu yakutokuwa na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa bahati mbaya walikuwa ni wazee na wao walikuwa hawana vyeti vya kuzaliwa kutokana na utamaduni wao ulivyowapitia. Kiutaratibu katika Wizara hii ni kuwa wale watu ambao hawana vyeti vya kuzaliwa na umri wao ni mkubwa sana hulazimika kujaza fomu na baada ya kujaza fomu kula kiapo na baada ya hapo huipeleka fomu ile katika sehemu inayohusika ili wapatiwe vyeti hivyo vya kuzaliwa. Lakini gharama yake baada ya kazi hiyo anayoifanya ni jumla ya Sh. 32,000/=, hii ni pesa nyingi sana na tulimlalamikia Mhe. Waziri, kuhusu hili na yeye mwenyewe akazungumza kuwa atalifanyia kazi. Alitwambia kwamba ameshatoa agizo na wameshakubalia kuwa bei ipunguwe, lakini mpaka hivi sasa bado tunakwenda na Sh. 32,000/=.

Swali langu ni kuwa je, Mhe. Waziri, alipotupa maelekezo yale ilikuwa uwamuzi haujakamilika kutolewa? Kwa hivyo, naomba nipate jibu na wakati huo huo nakumbusha kuwa Sh.32,000/= ni nyingi, Mhe. Waziri, anahitaji kutuonea huruma.

Jambo jengine Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria. Hii Tume inakazi muhimu sana na hii tume ni Tume ya kitaalamu. Katika sheria tunazotumia nyengine ni sheria ziliomo katika Katiba yetu na hasa sheria zilizokuwa zinahusiana na uchaguzi. Ukiziangalia tu katika kutoa haki ni lazima ziandikwe vyengine ambavyo ndiyo marekebisho ili haki iweze kutendeka. Sheria hizi zipo kwa miaka mingi sana. Tumeona sheria ambazo zimerekebishwa lakini tumeona kuna sheria muhimu sana zimeachwa.

Kwa hivyo, mimi nauliza hii Tume ya Kurekebisha Sheria wana mamlaka yao wenye za kupitia sheria zote na kuona kuwa sheria hii ina hitaji kurekebishwa au ni lazima wapelekewe na serikali ili watafute utaratibu wa kuzirekebisha. Kwa mfano Mheshimiwa, ukitizama kifungu 119 (12), (13) na (14), vifungu hivi vinaeleza namna ya Tume ya Uchaguzi inavyofanya kazi zake. Ukiangalia kifungu cha 119 (13), kinasema kuwa; "Hakuna Mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote litakalotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii."

Sasa waliofanya kazi hii ni binaadamu, na binaadamu wanapitikiwa, lakini kumbe hakuna Mahakama yoyote inayoweza kufanya chochote katika kufanya kazi yao, wanafanya tu wanavyofanya na matokeo tunayaona, mara nyingi tunapofanya chaguzi huwa zinakuwa na matatizo kwa sababu ya Tume. Ukiangalia kifungu hicho cha 119 (12), kinaeleza kuwa;

> "Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya Chama cha siasa."

Mhe. Spika, ina maana inafanya kazi zake itakavyo. Haiwi Rais wetu ambaye ndiyo kiongozi wetu Mkuu anakuwa na washauri wake.

Mhe. Spika, hata katika dini yetu mtu yeyote ambaye hakubali ushauri tunasema huyo si mtu na sio Muislamu kabisa. Kushauriana ni jambo muhimu sana na hii ni Tume imewekwa kwa sababu ya kutenda haki. Sasa ikiwa vifungu vyenyewe ndio kama hivi na wanafanya wanavyotaka. Tumeshuhudia siku za nyuma matokeo kiongozi fulani anayakataa kabla ya kutangazwa kwa kujua tu yanakwenda upande huu, lakini baada ya kutangaza anasema Tume imeamua. Sasa sheria kama hizi ambazo ni kandamizi, kwa nini Tume hii ya kurekebisha sheria hawazioni, wakazirekebisha na kuzidi kuiweka nchi hii katika amani na utulivu.

Mhe. Spika, mfano mwengine Kifungu cha 34 (7), kinasema hivi hii inahusiana na uchaguzi wa Mhe. Rais, inasema;

> "Iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa kifungu hichi, basi hakuna Mahakama yoyote itakayokuwa na Mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake."

Mimi kwa fikra zangu naona hivi ni baadhi ya vifungu ambavyo vingehitaji kufanyiwa marekebisho kwa maslahi ya nchi hii ambayo ni nchi ya amani, utulivu na mshikamano mkubwa.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati, naomba nimalizie Ofisi ya Mufti. Moja katika kazi yake ni kutangaza kuhusu mwazi kuandama ama kwa kufunga au wa Skukuu na kuratibu mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, dini ya Kiislamu ni dini moja. Mwenyezi Mungu ni huyo mmoja, maelekezo ya Mwenyezi yamo katika *Qur-an* ambacho ni kitabu hicho kimoja na hadithi za Mtume (*S.A.W*) ambazo ni nyingi tu na zina-*base* kwenye *Qur-an* ni hizo hizo na Mwenyezi Mungu katwambia hivi; *"Wa3taswimuu Bihablillahi Jamiia walaa tafarraquu."* Yaani tushikamane katika kamba hii ya Mwenyezi Mungu sote kwa pamoja wala tusifarikiyane.

Mhe. Spika, inasikitisha katika hii nchi moja; kuna watu wengine wanafunga na kuna wengine hawafungi siku ile na kinyume chake. Wakati mwezi ni mmoja, tarehe ni hiyo hiyo moja na tumeambiwa tusifarikiane na hii ndio Ofisi inayohusiana na Utangazaji kuhusu mwezi kufunga au kufungua. Na ikitangaza ni lazima tufuate, sasa je, kwa vile kunamtafaruku huu wa dini moja katika nchi hii na chombo hichi kimewekwa kwa makusudi pamoja na kuondoa migogoro.

Je, Mhe. Waziri, atatuelekeza nini katika mambo haya mazito ambayo tungeliona katika nchi moja, pengine katika nyumba moja tofauti hizi zisingekuwa ni vizuri kutokea. Mheshimiwa, nashukuru.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi jioni hii nikaweza kuchangia kidogo hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kitabu chake hichi ambacho amekipanga kushindwa hata kila moja kuweza kuja kupiga buti, nimpongeze Mhe. Waziri.

Lakini pia nije katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, kwanza niseme kidogo Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu la kuifanyia mapitia Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake. Lakini pia niseme Mhe.

Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na kuifanyia mapitio haitoshi Tume hii, kwani Tume hii ni kongwe na imeshapitwa na wakati, kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, Tume hii ikabadilishwa na kufanyiwa marekebisho zaidi.

Mhe. Spika, kuna tatizo la mishahara, serikali iangalie suala la mishahara kwa watumishi wake kwa *OC* wanazozipata ni kidogo sana, hili liangaliwe sana na zaidi limekuja katika kitabu hiki katika ukurasa wa 15 kinaosema kwamba;

"Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 498 milioni kati ya fedha hizo ni Shilingi 138 milioni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 340 kwa matumizi mengineyo. Lakini vile vile, hadi kufikia Machi 2015 shilingi mia mbili hamsini, arubaini na nne mia nane na hamsini hizi zilipatikana zikiwemo shilingi mia moja ishiri na tatu, elfu moja thamanini na nne mia nane na hamsini sawa na asilimia 78."

Mhe. Spika, niseme kwamba vile vile mishahara na stahiki za watumishi ni shilingi mia moja na ishirini na sita mia nane na sitini sawa na asilimia 37 kwa matumizi mengineyo.

Sasa Mhe. Spika, niseme kwamba kutokana ugumu wa kazi zao wa hii Tume wanashindwa kufanya kazi hasa pale kutokana na hizi fedha ambazo hazikutimizwa. Kwa hivyo, niiombe serikali wanapokuwa wanatia mishahara yao katika Mawizara iyangalie kama kiwango hichi kinatosha, kuliko watu kuwa tayari Wizara kutegemea na hatimaye fedha zile zinakuwa hazikamiliki.

Lakini pia Tume ifanyiwe utafiti, inahitajika kufanya utafiti na utafiti huo uwe nje ya nchi sio hapa Zanzibar. Ili kuongeza ufanisi zaidi kwa hii tume.

Mhe. Spika, nikija katika Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka, ninukuu kipande hichi kidogo;

"Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka ina jukumu la usimamizi wa mashtaka ya jinai Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Afisi inaendelea kusimamia kesi za jinai na kutoa ushauri wa kisheria kwa jeshi la polisi na taasisi mbali mbali za serikali pamoja na raia."

Mhe. Spika, ofisi hii ina kazi kubwa sana, kushuhulikia na kusimamia kesi za jinai na kutosha ushauri. Mheshimiwa, hii ni kazi kubwa sana, lakini niseme kwamba tukiangalia Ofisi hii inawafanyakazi ambao wameanza kazi tokea 2003, lakini wafanyakazi hawa Mhe. Spika, mishahara yao ni midogo, wanashindwa na mfanyakazi ambaye kaingia kazini miaka ya karibuni. Mtu huyu ukimuangalia ana *Master* au *Degree*, lakini mshahara wake ni mdogo tofauti na aliyeiingia hivi sasa.

Hili Mheshimiwa, naomba lirekebishwe kwa sababu tunawapoteza wafanyakazi wetu na ndio maana wafanyakazi hawa wanatukimbia kwa sababu ya kuwa levya levya.

Naomba Mhe. Spika, liangaliwe ili tuwe nao kwa makini, hawa ni wasomi wetu ambao ndio wa kuwategemea. Lakini leo ikiwa tutawaachia ambao kuwa na mishahara yao haitimii na kiwango tunachowapa hakilingani Mhe. Spika naona kama itakuwa tunakimbiwa na wafanyakazi wetu.

Lakini pia Mhe. Spika, nije katika Mahakama. Mahakama katika Kifungu cha 8 kinasema kwamba;

> "Mahakama ina jukumu la kusimamia utoaji wa haki."

Mhe. Spika, ni kweli Mahakama ina jukumu la kusimamia, lakini pia niseme kwamba Mahakama ni chombo kikuu cha kusikiliza kesi mbali mbali Mhe. Spika, za madai na jinai na Mahakama pia husema kwamba hupokea kesi mbali mbali za jinai na za rufaa, pamoja na utekelezaji wao mzuri Mhe. Spika, kuna haja ya kuwapa elimu au kuwapatia elimu zaidi wafanyakazi wetu hapa ili kuweza kuendeleza kazi zao. Lakini Mhe. Spika, Mahakama tutaiacha bado haina jitihada za elimu itakuwa wanakwenda wanavyotaka na hii itakuwa ni tatizo kwa kesi zinapotokea.

Pia, Mhe. Spika, nije katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Hii ina jukumu kubwa sana. Katika kamisheni hii kuna watu hawajui mali ya amana ni nini na wakfu ni nini, kwa sababu sasa hivi Mhe. Spika, kuna mashamba ambayo yanavamiwa na watu na haya mashamba watu wao tayari wameshakufa na bado pana watoto ambao wanahitaji kujua mali zao. Hili nimuombe Mhe. Waziri, aliangalie kwa kina na kulifuatilia zaidi ili watoto hawa wanapokuwa wanafikia umri wa kutaka haki zao watoto hawa wazipate.

Pia, Mhe. Spika, nije katika Ofisi ya Mufti, tumeshakaribibiwa na mwezi Mtukufu wa Ramadhani na mwezi huu maisha yote huwa na utata; aidha kwa wananchi na hata kwa Serikali vile vile. Unapofika mwezi Mtukufu wa Ramadhani kila mmoja hajui kama leo ni mwezi ngapi na yule atasema leo mwezi ngapi, sijui kwamba Ramadhan mtu inamuuma asipate kufunga au vipi. Lakini namuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie kwa kina kuhusu suala la mwezi wa Ramadhani tuepukane na huu utata unaotokea wakati wa mwezi huu mtukufu.

Lakini la mwisho niseme Mhe. Waziri, niiombe Serikali pamoja na wizara ndio Serikali kupiga vita wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuacha matusi ya ovyo, tuache kuvaa nguo fupi, tuvae nguo ambazo zinastahiki kwa mwanaadamu.

Vile vile, Mhe. Spika, tuache kula ovyo ovyo mabarabarani, hili ni tatizo itatuvunjia Ramadhani yetu na saumu yetu kuwa ni njema.

Baada ya hapo Mhe. Spika, niseme ahsante.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante Mhe. Spika, kwa jioni ya leo na mimi kunipa fursa ya kuchangia mawili matatu katika bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo tukaendelea kuwa pamoja hapa na hatimaye kuendelea na taratibu ambazo ilikuwa tumejipangia.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia haya, lakini tatu nimshukuru Mhe. Waziri na niwapongeze pamoja na timu yake inayoongozwa na Katibu Mkuu ndugu yangu Asaa ambaye yuko pale na timu yake juu kwa siku ya leo.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo sasa niende katika hili buku kubwa ambalo ni G04 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Nikiangalia kitabu ambacho tumekabidhiwa kwa siku ya leo ambacho kina hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria, hapa kuna fedha ambazo zimeombwa, lakini nimepata utata kidogo nikitaka nisaidiwe sasa sijui hesabu sahihi ni ipi; iliyokuwemo katika buku kubwa au iliyokuwemo katika kitabu hiki kidogo. Kitabu kidogo hiki katika Kiambatanisho namba 2, Makadirio na Matumizi kwa mwaka 2015/2016 katika eneo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka tumeombwa tujaalie milioni elfu moja mia tano na sitini na saba na mia tatu. Lakini hili buku kubwa hili tuna moja sita ishirini na saba na mia moja, sasa sijui kama ni *typing error* tu au ni kitu gani, nitamuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie hasa wapi tutakapo-*base;* ni kwenye kitabu kidogo hiki au hili buku kubwa na tatizo liko wapi katika hizi hesabati.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo, nakwenda katika eneo la Hati Miliki. Mhe.Spika, zamani tulizoea kuona vipindi vya kina bwana Mashaka, profesa gogo na mambo mengine mengine. Vipindi vile kwa ghafla moja tu vikasita, lakini tulipowatafuta wenzetu ili watusaidie walisema kwamba ile kazi ya kufanya ule utayarishaji wa vipindi vina-*cost* muda mkubwa sana na wakati mwengine wanapoteza mpaka fedha kwa kiwango fulani na wanapotoka kwenda kuwaomba wahisani mara nyingi wanakuwa wana matatizo ya kuwasaidia kuwapa hicho kitu ambacho kinaweza kikasaidia.

Lakini masikitiko yao makubwa yanakuja katika suala zima la kuona zile filamu zao ambazo wao wanakuwa wao wanazi-*act* kwa ajili ya kusaidia kufurahisha watu watu maemeno yetu, filamu zile zinauzwa kwa fedha nyigi sana na watu wanakodishana lakini wao hawanufaiki na michezo ile. Na hatimaye hata ndugu

yangu Makombora akaacha utaratibu ule wa ku-*act* michezo na watu wengine wengine kwa sababu ilikuwa haziwapatii tija.

Kuja kwa Taasisi hii ya Hati Miliki tuliona kwamba kuna muelekeo na hisia zetu kwamba hapa sasa asaa kheri kutakuwa watu wanapo-*act* michezo yao itakuwa inahifadhiwa, inamilikiwa na wale wanao-*act* michezo yao watakuwa wanapata faida fulani fulani. Lakini bado katika sekta hii wale watu wanahitaji taaluma, ningelimba sana Mhe. Waziri, kupitia katika taasisi zake au awasaidie wale watu wakae pamoja na waweze kujua sasa ni namna gani wataweza kuneemeka kwa ile michezo ambayo watakuwa wana-*act* na hatimaye ikaweza kuwapatia kitu kidogo na wao wakanufaika kama ambavyo wale watu wanachukua zile *films* zao wakenda kuzipeleka nje wakaneemeka wao pasina wao kupata faida yoyote.

Mhe. Spika, ukiacha hapa kuna eneo ambalo lina vijana wetu wanaitwa "Kizazi kipya" kwa sasa na wao vile vile wanajitahidi sana, ajira zenyewe katika Serikali mtihani, lakini wanakwenda kujiajiri wenyewe kwa ajili ya kurekodi nyimbo zao na mambo mengine mengine. Ningeliomba taasisi hii pale ambapo wanakuwa wanafanya yale mambo yao na wakapata zile nyimbo zao, naomba zitunzwe na zitumike sasa kwa faida yao wao pamoja na wale wengine ambao wanafata zile taratibu ili waweze kuona matunda ya kazi kubwa na nzito ambayo wanatumia mabongo yao kutayarisha na hatimaye zile nyimbo zao zikapigwa ovyo ovyo tu nje bila ya wao kunufaika na yale mambo ambayo wanakuwa wanayafanya.

Mhe. Spika, nimesema leo mchango wangu ni mdogo sana, nikiondoka hapo, nakwenda katika suala zima la *DNA*. Chombo hiki kimekuwa kina kitendawili katika Baraza lako hili tukufu. Sasa leo hii ninashukuru kwamba tumepata pahala ambapo tulisikia tetesi kwamba huenda hapa pakawa ndio pahala pake. Sasa leo tunamuomba Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba atakapokuja hapa atupe mustakbali wa suala la kuweza kupatikana kwa chombo cha *DNA* kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa zamani ninasikitika sana na huwa wakati mwengine hasa sasa hivi ninakuwa ninahuzunika ninaposikia kuna taasisi zinawasifu sana ndugu zetu akina mama, lakini nikawa sisikii namna gani akina baba wanasifiwa. Lakini baada nikaweza kujiona kwamba sisi kina baba tuna matatizo ambayo yanakera katika jamii.

Mhe.Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona udhalilishaji umekua kwa hatua kubwa sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, ni jambo la kusikitisha. Wawakilishi wako humu ndani wamekuwa na utaratibu wa kuendelea kuchangia kila inapotokezea mwaka na bajeti mbali, hususan katika Wizara ya Afya kwa ajili ya kukiomba chombo hiki. Lakini matokezeo yake sasa imekuwa kunapigwa dane dane kila siku; tunaambiwa Wizara hii, kesho Wizara hii, keshokutwa wizara hii.

Sasa leo tumefahamu kwamba chombo hiki kumbe ninasimamiwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Tunamtaka Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atuelezee, je, Serikali ina utaratibu gani wa kuweza kupatikana chombo hichi ili watoto wetu wanusurike na matatizo haya ambayo yanawakabili.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, kwa kumalizia ninakuja katika suala la Katiba inayopendekezwa. Jana tulipomalizia kuchangia katika Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, miongoni mwetu tulichangia kuweza kuona na wengine wakahitaji kutaka kujua baadhi ya ufafanuzi katika suala zima la Katiba inayopendekezwa. Kwa ufahamu wangu Mhe. Spika, Wizara hii ya Katiba na Sheria ndio pahala hasa panapohusiana na suala lile la Katiba inayopendekezwa kwa sababu hii ni Wizara ya Katiba na Sheria katika nchi yetu.

Nikiangalia Mhe. Spika, naweza mtu akaja akazungumza kwama Katiba ile haikuhusu upande huu wa Zanzibar, lakini Baraza lako Tukufu hili Mhe. Spika, lilipitisha hoja hapa ya kukubaliana na suala zima la upitishwaji wa kura za maoni katika taasisi yetu. Kwa uzoefu wetu katika Wizara zetu tunazokwenda nazo katika nchi yetu inapokuwa kuna jambo huwa Wizara inayohusika kuligusia au kuzungumzia jambo lile. Sasa katika taasisi hii ya Wizara ya Sheria na Katiba suala la Katiba inayopendekezwa sikuona hata dalili zake, je, kulikoni Mhe. Spika? Tunaomba tupate maelekezo juu ya suala la Katiba inayopendekezwa, kwa nini hatujapata taarifa zake katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Baada ya maelekezo hayo Mhe.Spika, na kwa kujali muda wako ninaomba kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni nipate maelezo lakini nipate na majibu ya masuala ambayo nimeyaomba hapa nijibiwe ili mwanzo nachangia kwa asilimia 80 bajeti hii na nitakapopata jawabu kwa asilimia 20 nyengine ya mambo niliyoyaomba nitamalizia kwa asilimia 20. Nitakuwa makini kuangalia buku leo nisije nikapotea ili Waziri wa Fedha asije akanikosoa tena. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ambayo ndani ya Wizara hii pia kuna taasisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ambazo ametujaalia hadi leo hii kuwa tuko salama na kuweza kuichangia hoja hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, nimewasikia wajumbe wengi Mhe. Spika, na wamechangia kwenye maeneo mengi kama ilivyo ada inapokuwa kuna bajeti ya Wizara hii maeneo muhimu lazima yanaguswa. Mahkama, vizazi na vifo, Ofisi ya *DPP*, Ofisi ya *Attorney General* na nyingi nyenginezo na ni taasisi ambazo zinagusa jamii moja kwa moja.

Mhe. Spika, wakati tunamaliza kipindi hiki cha miaka 5 cha ungonzi huu wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzim Dr. Ali Mohammed Shein, ni wajibu wetu sisi kama Wizara, sisi kama Wakuu wa Taasisi kufanya tathmini ya pale ambapo tulikuwepo kabla ya uongozi wake na sasa ambapo tupo wakati tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, miongoni mwa wizara ambazo zimepata neema kubwa katika uongozi huu ni Wizara ya Katiba na Sheria. Wengi tunakumbuka Mhe. Spika, wakati wa mwanzo tu wa uteuzi wa Mhe. Rais jambo la mwanzo ambalo alifanya ni kuteua majaji wa Mahkama Kuu, mbali ya hayo uajiri wa mahakimu umekuwa ni mkubwa katika kiipindi hiki cha miaka 5 tofauti na vipindi vyengine vyote ambavyo vilopita. *(Makofi)*

Mishahara ya watendaji Mhe. Spika, pamoja na hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe, lakini mishahara hii ya mwaka 2010 kabla ya uongozi wa Mhe. Rais na leo ukiipima basi imeongezeka karibu mara tatu. *Of course,* bado tunatambua sote kama kima kile bado wengi wetu tunalia kwa Serikali, lakini kiujumla nyongeza kubwa imefanywa.

Mhe. Spika, jengine ni uajiri wa Wanasheria wa Serikali na Wanasheria kwenye Taasisi mbali mbali za wizara, zimefanywa kwa kiwango kikubwa kwenye kipindi hiki cha miaka 5. Mfano Mhe. Spika, ukitizama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hadi mwaka 2010 kulikuwa kuna wanasheria 9 ukijumlisha na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Leo mwaka 2015 tuna wanasheria zaidi ya 25, hao wote ni kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini kuna wanasheria wengine karibu 12 tumewapa *status* ya kuwa wanasheria wa Serikali kwenye Taasisi zetu mbali mbali za mawizara. Ukipiga jumla yake Mhe. Spika, unapata karibu wanasheria wa Serikali 36, tokea wanasheria 9 mpaka wanasheria 36, nalo hilo ni jambo kubwa na inabidi tushukuru lililofanywa.

Jengine Mhe. Spika, ni majengo, leo tunajinasibu Mhe. Waziri, anajinasibu na jengo lake la kisasa, lakini Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia na yeye anajinasibu kwa jengo la kisasa zaidi ambalo tayari limeshajengwa. Haya yote Mhe. Spika, yametokea kwenye kipindi hiki kwa miaka 5 na majengo haya yote ni kwa fedha zilizotoka hapa kwa kaka yangu Mhe. Waziri wa Fedha. Kwa hivyo, wakati tunachangia haya ni vyema pia Waheshimiwa Wajumbe wakumbuke na haya pia. Kama Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa kipindi hiki tumepewa neema kubwa na Mhe. Rais, haya yaliyobaki mengine sasa ni ya kwetu sisi ya kiutendaji, ndio haya sasa ambayo wengi Waheshimiwa Wajumbe, wameyazungumza, wameyajadili na wameyatolea maoni, haya ni yetu sasa ya utendaji, lakini mengi ambayo yalistahiki kufanywa na Mhe. Rais, nadhani ametimiza wajibu wake.

Sasa kwa kupitia chombo hiki Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Rais kwamba sisi ambao ametupa dhamana na majukumu ya kuongoza hizi taasisi kwa neema hizi ambazo ametoa kwenye Wizara hii ya Katiba na Sheria tutatimiza na sisi majukumu yetu kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa taratibu na kuhakikisha kwamba Taasisi hizi zote zinatenda haki na zinatoa fursa na haki kwa wananchi wote ili sasa Waheshimiwa Wajumbe baadhi ya hizi hoja ambazo wamekuwa wakizitoa ziwe zinapungua kila mwaka ambao tutakuwa tunakutana hapa.

Baada ya hayo Mhe. Spika, sasa naomba nimsaidie Mhe. Waziri kwenye baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza na wameyatolea hoja.

Mhe. Spika, nikianza na Mhe. Wanu, ambaye ametoa hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, *of course,* kwa umahiri wa Mhe. Wanu, ambaye amekuwa kwenye kamati hii kwa kipindi chote cha miaka mitano ameweza kutambua haya maeneo mengi na *gaps* ambazo zipo na ameweza kutushauri.

Mhe. Spika, moja hili ambalo amelizungumza ni la rushwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza rushwa ndani ya Mahakama na ndani ya taasisi zetu mbali mbali.

Mhe. Spkika, kazi kubwa inayofanywa Mahakamani kabla hata ya kutoa hukumu ni kusikiliza na baadae kuandika, hakuna *Hansard* kule kama hapa Barazani. Kwa hiyo, kazi kubwa wanayofanya ni kusikiliza. Sasa naamini hoja nyingi hizi za Waheshimiwa Wajumbe zilizozungumzwa kwenye rushwa wamezisikia, na mimi Mhe. Spika na Mhe. Waziri, tunawaahidi Waheshimiwa Wajumbe kama tutachukua dhamana ya kwenda pia kuzungumza na Mhe. Jaji Mkuu, hatwendi kumpangia kazi, wala hatuwezi kumfahamisha majukumu yake, kwa sababu yeye ni muhimili na anajitegemea.

Lakini tutakwenda kumpa salamu ambazo zimetoka kwenye chombo hiki cha muhimili kama wake yeye na hizi ndio salamu ambazo tunampelekea. Lakini kwa kiasi kikubwa Mhe. Spika, mambo haya yamepungua na rushwa sio tu anayopokea lakini hata pia anayetoa, maana yeye ndiye *source;* yule anayetoa ndiye anaye-*solicit* mpaka yule mwengine sasa akamshawishi apokee.

Sasa lina pande zake zote mbili. Hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, wasilitizame upande mmoja, tunapojadili kadhia hii tulitizame kwa pande zote mbili na sisi wajibu wetu kuhakikisha kwamba hayo hayatokei na ndio maana imepitishwa hapa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ambayo imeshaanza kazi zake, kuna Mkurugenzi wake Mkuu na kazi zake zimeanza uzuri. Kwa hiyo, hilo tumelisikia na naamini Waheshimiwa hawa nao pia wamelisikia.

Mhe. Spika, jengine ni hili la uhaba wa fedha kwenye taasisi ya Mwanasheria Mkuu, kukosa ushirikiano ndani ya taasisi za serikali na alitaka Mwenyekiti wa Kamati kutoa toleo kwa serikali. Mimi niseme hili la toleo nadhani halina haja, kwa sababu moja ya jambo ambalo serikali imefanya ni kutukubalia kuwapa *status* wale Maafisa wa Sheria waliokuwa mawizarani kuwa Wanasheria wa Serikali. Maana yake sasa wao ndio watakuwa kiungo baina ya wizara zao na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sasa yale yote ya kisheria ambayo yanatoka ndani ya wizara zao lengo letu ni kwamba wao kama Wanasheria wa Serikali waanze kuyashughulikia kwanza kule wizara kabla hayajaja kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa hiyo, nadhani hili serikali imetusikia kilio chetu cha muda mrefu na imetukubalia kufanya hayo na tutaendelea kuwapa *status* ya uanasheria wa serikali kila pale haja itapohitajika kufanya hivyo. Kwa sababu mtu unapompa cheo cha Mwanasheria wa Serikali kinakwenda pia na maslahi, inabidi nae awe na maslahi kama ya Mwanasheria wa Serikali aliyekuwepo Ofisi ya *AG* au Ofisi ya *DPP*. Kwa hiyo, nayo pia inakwenda na hivyo, lakini tunaishukuru serikali kwa kutukubalia ombi hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Mshimba, kama desturi yake amechambua vifungu vingi na akazungumzia suala hili la *Transworld* ambalo Waheshimiwa wengi nalo wamelizungumzia. Lakini Mhe. Mshimba, yeye alizungumzia kwenye mikataba, nadhani tatizo lilokuwepo ni la usajili kama kampuni hii jina hili la *Transworld* limesajiliwa mara mbili. Sasa hili naamini Mhe. Waziri wa Katiba atakuja kulitolea ufafanuzi zaidi, lakini utaratibu wa kisheria upo hairuhusiwi kusajili jina la kampuni moja mara mbili. Sasa utaratibu wa kisheria upo na inapotokea bahati mbaya kama hii sheria zinaelekeza nini kifanyike.

Kwa hiyo, hili *details* zake zaidi Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria atakuja kulielezea. Lakini utaratibu wa kisheria upo na wala sijambo ambalo lakuwafanya Waheshimiwa Wajumbe waingie hofu kwa kuona kwamba limetokea hili, hili linaweza kutokea ni jambo la kawaida na hawa ambao wanafanya huku kazi pia nao binadamu na sisi mpaka sasa hatuna *data base*, sina hakika ambayo imesajili majina yote. Sasa kwenda kupekua pekua majina haya yote nayo pia inahitaji muda. Kwa hiyo, haya hutokea, lakini yanapotokea kama hivi na tukipata taarifa basi sheria imetoa muongozo wake na naamini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria atakuja kulitolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Mshimba, amechangine kuhusu *AG* kusimamia sheria. Mimi nadhani hiyo ndio kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndani ya Baraza hili na ndivyo ambavyo Wanasheria Wakuu wote wamekuwa wanafanya, maana chombo hiki tunakiita Baraza la Wawakilishi, lakini ukisoma Katiba kinaitwa ni

chombo cha kutunga sheria. Kwa hiyo, kazi zetu humu ni kutunga sheria, hiyo ndio kazi yetu ya msingi Nam.1 na kazi yetu nyengine ya msingi Nam.2 ni kuisimamia serikali na kazi yetu ya msingi Nam.3 ni hii ambayo tunaifanya kupitisha bajeti ya serikali. Hizo ndio kazi kubwa za msingi ambazo zinatakiwa zifanywe na chombo hiki.

Kwa hiyo, kutunga sheria na katika sheria hizi nyingi ambazo tumezitunga karibu elfu na zaidi zinakaribia ambazo nyingi huwa zinaletwa na serikali, pamoja na kwamba Kanuni inaruhusu mjumbe kuleta Mswada binafsi na tumeona hilo kipindi hiki kwa Mhe. Hamza, amejaribu kuleta mswada wake binafsi. Lakini ni miswada mingi ambayo inaletwa na kupitishwa Barazani huletwa na serikali, sasa kwa kuwa miswada hii kabla haikufikishwa hapa inabidi ifanyiwe *drafting* na mwandishi wa miswada hii ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali inabidi awemo humu ndani atoe ufafanuzi wa kisheria kwenye yale maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe mara nyingi huwa wanataka ufafanuzi. Kwa hiyo, namuhakikishia Mhe. Mshimba, ambaye *AG* hiyo ndio kazi yake na wala hana haja ya kuingia kwenye kazi ya siasa, na ndio maana haendi jimboni. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine ni hili la *DNA,* wajumbe wengi wameliuliza na sio tu kwenye *session* hii, lakini kwenye vikao vingi ambavyo vimepita. Mimi sitaki nimuondolee utamu wake Mhe. Waziri, lakini kuna ahadi ambayo imeshatolewa kutoka kwa wenzetu wa *European Union,* wametuahidi kama watatununulia mashine hii. Na mimi nimemsikia yule Balozi wa *European Union* mara mbili na mara ya mwisho ilikuwa ni juzi wakati tunazindua rasmi mkakati ule wa *Legal Sector Reform* na ule mkakati wa udhalilishaji dhidi ya watoto na yeye alikuwepo na pia aliahidi kama chombo hiki atakinunua.

Sasa kitakuwepo wapi, kitatizamwa na nani, mimi nadhani kitapokuja huo utaratibu utatengenezwa kwa sababu nacho kile chombo kinataka utaalamu, chombo kile ni ghali, chombo kile ni cha kisasa, sasa kinataka pia utaalamu wake wa kukishughulikia. Sasa nimuhakikishie Mhe. Mahamoud, kitapokuja hicho chombo kitatafutwa pahala muafaka pakuwekwa ili sasa kianze kufanya ile kazi ambayo Waheshimiwa Wajumbe, wengi wamekuwa wakiipigia kelele nayo ni kuhakikisha kama zile *samples* za wale ambao wanafanya vitendo hivi viovu vya ubakaji inawezwa ikenda ikatizamwa na ikatolewa maamuzi mara moja. Kwa hiyo, hilo jawabu lake nadhani Mhe. Mahamoud ni hilo.

Mhe. Spika, jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumza ni hili la maamuzi, kwamba maamuzi mengi ya Mahakama yanachelewa kupatikana, na Mhe. Hamza, hapa ametusomea *phrase* muhimu (*Justice Delayed is Justice Denied),*yaani haki inayochelewa kutolewa ni sawa sawa na haki ambayo imenyimwa kupatikana. Nadhani kwa tafsiri ya haraka haraka.

Mhe. Spika, lakini hili pia kwanza nikubali kwamba katika eneo hili hakuna muongozo wa kisheria ambao upo, pale ambapo Hakimu au Jaji anapopewa dhamana ya kushughulikia kesi fulani, hapewi muda wa kuambiwa inapofika tarehe fulani uwe umeshamaliza kusikiliza kesi hii. Na hakuna muda ambao umewekwa wa kisheria wa kuambiwa yeye baada ya kusikiliza sasa achukue muda gani kutoa ile hukumu au maamuzi. Sasa hili moja ni eneo ambalo inabidi pia tukae na tulitafakari na tujue tunaweza tukalishughulikia kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, lakini pia maamuzi haya wakati mwengine kesi hizi zinachelewa kusikilizwa, kwa sababu kesi hizi ni za pande mbili. Upande wa mdai, upande wa mdaiwa au upande wa mshitaki, anayeshitakiwa na upande wa Jamhuri ambao ni *DPP*. Sasa zinakuwa zina pande mbili mara zote, na wakati mwingi Mhe. Spika, kesi hizi ambazo zinakuwa na pande mbili, sio tu ucheleweshwaji wake unakuwa wa Kimahakama, lakini hata sisi ambao tunakwenda Mahakamani; leo umekwenda wewe, mwenzio hakuja, utapokwenda wewe wakili mwengine anakwambia niko *High Court* huko chini siwezi kuja kwanza.

Sasa kuna sababu nyingi ambazo zinapelekea maamuzi haya au kesi hizi zishindwe kutolewa kwa wakati. Lakini hili ni jambo la msingi ambalo Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumza na niwaahidi kupitia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tutatizama namna bora sasa yakuweza kuangalia angalau hawa ambao wanapewa hizi dhamana basi hawachelewi na hawachukui muda mrefu kuzishughulikia na kutoa maamuzi. *Of course,* sasa hivi moja ya jambo ambalo limefanywa kwenye sheria hii ya makosa haya ya jinai, kama ikipita miezi minne kesi hiyo haikuanza kusikilizwa basi Hakimu au Jaji amepewa mamlaka ya kuiondosha kesi hiyo.

Mhe. Spika, lakini pia kwenye kesi hizi za madai kwenye *civil procedure* ukiisoma kuna kifungu pia kinaelezea kama upande mmoja wa kesi ukiacha kuhudhuria kipindi mfululizo, pia Hakimu au Jaji nae amepewa fursa ya kuweza kuiondoa kesi hiyo. Lakini haya yanahitaji yafanyiwe maamuzi ya umakini kwa sababu yanabeba maslahi ya watu pia. Sasa hawa ambao wamepewa dhamana hii wanapofanya maamuzi hayo inabida pia wayatafakari hayo yote kwa upana wake.

Mhe. Spika, jengine ambalo Wajumbe wengi wamelizungumza labda ni hili la Mhe. Hija. Mhe. Hija, yeye amesema kuna maeneo haungi mkono, hiyo ni haki yake lakini haungi mkono wakati huo huo akatoa kazi ambazo zinatakiwa zifanywe na taasisi hizi. Sasa kwa mfano Mhe. Spika, ukisema huungi mkono bajeti ya Mhe. Mufti, lakini unamwambia Mhe. Mufti huyu aanze kazi ya kwenda kuzungumza na wanasiasa, sasa atahitaji hizi fedha ambazo ameziomba hapa ili aweze akafanye kazi hiyo.

Sasa utapomzuilia Mhe. Mufti huyu, hii kazi Mhe. Spika, nadhani hatoweza kuifanya, sasa nimsihi sana Mhe. Hija, alitafakari hili vizuri, kwa sababu hii kazi ambayo ameitoa kwa Mhe. Mufti ni kazi ya msingi na ni kazi ambayo sisi sote humu ndani inatakiwa tuishughulikie. Sasa nimuombe kwamba Mhe. Mufti huyu amtizame kwa makini na asimchezee huyu mzee.

Mhe. Spika, hili jengine la vizazi na vifo ambayo pia wengi Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumza na kwamba vyeti hivi havitoki. Mhe. Spika, hili nalo pia inabidi tulitizame kwa umakini, kwa sababu hapa kwenye Baraza ambalo tulimaliza kikao kabla ya hiki wengi Waheshimiwa Wajumbe wako walikuja na marundo ya vyeti vya kuzaliwa. Hiyo ni ishara ya kwamba vyeti hivi vinatolewa, lakini labda havitolewi kwenye kile kiwango ambacho Waheshimiwa Wajumbe wengi wanataka, nayo pia ina sababu yake. Moja ya malalamiko ambayo chombo hiki kina ilalamikia sana serikali ni kukosa fedha za kununulia zana za kuweza kufanyia kazi. Mara ya mwisho waliomba nadhani milioni 60 ili waweze kwenda kununua karatasi za kuchapisha hivi vyeti.

Sasa kazi hii inafanywa, lakini inawezekana na changamoto hizi ambazo tunazo za fedha haifanyi kwa kile kiwango ambacho wengi wetu tunataka kifanywe, mtu akienda na akisajiliwa basi baada ya siku mbili apate cheti chake, na *of course*, sote sisi tungependa iwe hivyo, lakini kuna sababu nyingi ambazo hizi zinafanya sasa ishindikane kufanywa ile kazi. Lakini naamini wanasajiliwa, ila kazi ambayo sasa inakosekana kutolewa haraka haraka ni hivi vyeti, lakini na hili pia naamini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, atakuja pia kulitolea ufafanuzi wake.

Mhe. Spika, hili la maslahi kwenye…

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa, zingatia muda ili Mhe. Waziri, aje akamilishe.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, hili la maslahi hili nadhani nimelizungumza la Wanasheria hawa wa Ofisi ya *DPP*, Wanasheria wa Serikali nimelizungumza na kama ambavyo nimesema bado wengi wetu kuna kilio, na sisi ambao tunaongoza hizi taasisi tunayafahamu hayo. Lakini kama ambavyo nimesema Mhe. Spika, tulipotoka sio hapa ambapo tulipo. Sasa mara nyengine inahitaji tu subra na serikali nayo kupitia wizara husika nayo pia inashughulikia.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kwa heshima na taadhima niunge mkono hoja hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kufanya majumuisho katika mjadala ambalo ulikuwepo tokea jana.

Lakini kabla sijafanya hivyo Mhe. Spika, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kutufikisha hapa katika kuendeleza shughuli zetu hizi.

Mhe. Spika, pili, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, wote ambao wamechangia na wale waliokuwa hawakuchangia, lakini zaidi Kamati ya Katiba na Sheria ambayo ilitoa maoni yake na hasa maoni yao ambayo kwa kweli kwa upande wetu sisi itakuwa kama ni dira na chachu ya kufanya shughuli zetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba niwatambue wachangiaji wa hoja hii ambao kwanza ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Mohammed Haji Khalid
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Hija Hassan Juma
Mhe. Salum Abdalla Hamad
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa; na
Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe.Spika, wote hao nawashukuru sana kwa michango pamoja na maoni yao ambayo wametupa ili tuweze kuyafanyia kazi katika wizara yetu.

Mhe.Spika, michango mingi iligawika sehemu sita na mimi nitaomba nizungumzie sehemu hizo sita ambazo naamini kila sehemu itawagusa wale ambao wamechangia.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la Mahakama, kulikuwa kuna suala la Usajili wa vizazi na vifo, kulikuwa na suala la Mufti na usajili wa misikiti, suala la *Transworld* kubadilishwa mara mbili, suala la Afisi ya *DPP*, kesi ya Kwale na jengine lilikuwa ni suala la Wakfu na Maliamana.

Mhe. Spika, Mahakama kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu ni kwamba tumejitahidi katika suala la mafao na nafurahi kusema kwamba kwa hivi sasa matatizo mengi ambayo tulikuwa nayo yamepunguka na namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, aliyasema hayo kwa sababu yeye alikuwa mstari wa mbele katika kuwatetea wafanyakazi hawa. Lakini tuna tatizo kubwa Mhe. Spika, ambalo lilizungumzwa hapa la suala la *assessors* . Ni kweli kwamba *assessors* wanadai.

Lakini suala la *assessors* naomba nilizungumze katika misingi inayofuata; walikuwa wandai fedha nyingi na tulijitahidi kuomba fedha hizo walipwe na tunaishukuru serikali walijitihadi sana kutupa fedha hizo. Lakini ukiwalipa leo kwa sababu kila siki kesi zinaendelewa wale *assessors* wanakuja katika kesi Mahakama Kuu. Kwa hivyo, wana kama mzunguko, kama umeshawalipa leo kesho wana kesi pengine *assessors* 12 watakuwepo katika kesi zitakazokuwepo katika Mahakama.

Kwa hivyo, bado lile deni linaendelea kulimbikizwa hata kama utawalipa na fedha zetu ambazo tunazipata tunazijua. Kwa hivyo, suala hili limekuwa likitupa mashaka kwa misingi hiyo, lakini hata hivyo deni lilikuwa kubwa sana na hivi sasa limeshapungua sana kabisa, lakini kama nilivyosema litaendelea kuwepo kwa sababu ya misingi hiyo.

Hata hivyo, baada ya kuona matataizo haya wizara tumekaa na tumejaribu kutafuta njia nyengine ya namna gani kupunguza *assessors* katika kesi hizi. Kwa hivyo, tunafikiria kwamba kuwe na kesi nyengine ambazo si lazima kuwa na *assessors*. Lakini hii bado tunaifikiria namna gani tutafanya na namna gani tunaweza tukafanya hivyo kisheria ili tuweze kuendesha kesi bila ya *assessors* na kwamba mana hiyo kupunguza yale madeni ya kesi za *assessors*.

Mhe. Spika, kuna suala la kesi la ubakaji ambalo limezungumzwa sana kesi za ubakaji nazo zinamashaka. Lakini hapa kwa kweli napenda niseme kwamba jamii nayo haitusaidii hata kidogo. Jamii haitusaidii kwa sababu kuna kesi nyingi ambazo zimekamatwa, lakini unapotaka kwenda Mahakamani mama wa mtoto alobakwa anakuja anasema hataki kesi, baba wa mtoto aliekamatwa au alibakwa au mjomba wake au mtu mwengine anakuja anasema kuwa hataki kesi au utaona kwamba kesi unaipelekea Mahakamani utasikia kwamba wameshaozana huko mitaani.

Kwa hivyo, tatizo ya ushahidi ndio gumu hapa, ingelikuwa jamii inatoa ushahidi inakubali kuleta ushahidi, kwa kweli suala hili lingelikuwa kidogo tungeliweza

kulidhibiti sana. Kwa hivyo, wito wangu Mhe. Spika, ni kwamba wazee na jamii ili tukitaka suala hili tulipunguze kwa asilimia kubwa sana, basi lazima wazee pamoja na jamii tuwe mstari wa mbele katika kutoa ushahidi ambao unahitajiwa na ushahidi wenyewe hauko mgumu sana kama ule ushahidi wa kawaida. Lakini sasa wazee hawataki, jamii haitaki na nyinyi mnatwambia kwamba ikiwa hakuna ushahidi basi kesi tuifute kwa sababu itakuwa kama unamuonea mtu bure.

Kwa hiyo, ndio maana kesi hizi zinazorota sana siku nyingi zinakaa katika Mahakama hazisikilizwi kwa sababu mashahidi hawaji. Kwa hivyo, ombi langu kwa jamii na kwa wananchi ni kwamba jamani tunapopata kesi hizi na mashahidi ambao mara nyingi huwa ni wazee au huwa ni jamaa basi waweze kutoa ushahidi ili tuweze kufanikisha suala hili.

Lakini lilizungumzwa Mhe. Spika, suala la *DNA*, naomba nilizungemze kabisa. Hapo nyuma *DNA* ilikuwa kama inapigwa mpira, mara ni suala la Wizara ya Afya, mara suala la Wizara ya Katiba na Sheria mara Wizara ya Wanawake na Watoto. Lakini mtakumbuka kwamba hivi juzi tulizindua mradi wa *Legal Sector Reform* na wadau wetu pale au watu ambao wanasaidia katika mradi huu ni watu wa *EU* pamoja na *United National.* Nafurahi kusema kwamba *European Union* wamekubali kutoa chombo hichi na hivi sasa watu wameshanza kufanya utafiti kwa namna gani tuweze kukipata chombo hichi kwa ajili ya kukileta na kukitumia.

Sasa suala ni kwamba je, kitakapofika tutakiweka pahala gani na nani watakuwa ni *responsible*? Suala hili bado tunalifanyika kazi na baadae tutajua wapi tukiweke chombo hichi ili tuweze kufanya uchunguzi huo ambao unahitajiwa. Kwa hivyo, suala hili la *DNA* nafikiri ni suala ambalo tunamshukuru Mwenyezi Mungu tumeshakubaliana na wenzetu hawa watatusaidia na karibuni sana chombo hichi tunaweza tukakipata. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa katika Mahakama, ni suala la Mahakama ya Kazi. Kweli katika Mahakama ya Kazi tulisema kwamba bado kesi zote zile hazijasikilizwa na si kwa sababu Mahakimu au Majaji walikuwa hawafanyi kazi ni kwa sababu yule Hakimu au Jaji aliekuwa anahusika na Mahakama ya Kazi alikuwa bado hatajeuliwa. Kwa bahati hivi sasa ameshateuliwa na kazi imeshaanza na ameshaanza kusikiliza kesi zinazohusiana na suala la kazi.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo lilizungumzwa kuna *percentage* ya zile kesi ya zile kesi. Nashukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumza vizuri na

kwamba kesi tulizotoa ile *percentage* yenyewe ni zile kesi ambazo tulizipata kwa mwaka huu. Lakini kuna kitu kimoja ambacho pia lazima Mhe. Spika, tukitizame ni kwamba unapofungua kesi Mahakamani ile kesi haitokwenda tu ina mambo yake mengi ambayo lazima yatimilie.

Kwa mfano ushahidi, kuna *procedure* nyengine na kuna utaratibu mwengine ambao lazima ufuatwe. Sasa unaweza kwenda Mahakamani ikawa Wakili mmoja anayeshughulika na kesi ile yuko katika Mahakama nyengine na kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria ikiwa Wakili yule yuko Mahakama Kuu kwa mfano na kesi iko katika Mahakama ya Mkoa, kwa hiyo, Mahakama Kuu inachukuwa *precedence* ndio kubwa ile. Kwa hivyo, hawezi yule Wakili kuja katika Mahakama ya Mkoa.

Kwa hivyo, utaona Hakimu yule kama ana kesi mbili siku ile lazima atakwenda moja katika ile Mahakama kubwa. kwa hiyo, kesi ya Mahakama ndogo ya Mkoa kwa mfano au ya Wilaya itabidi ighairike. Kwa hivyo, kutokana na matatizo hayo na kutokana na matatizo ya ushahidi watu wengine hawaji na wengine wana dharura; huku ana dharufra hii, huku ana dharura hii, kwa hivyo, kesi zinaendelea kukaa na kurudikana. Lakini kama tulivyosema kwamba kuna ile Kamati ya kusukuma mwenendo wa kesi hizi ambayo kamati hiyo inajitahidi na ndio maana tukaweza angalau kupunguza kwa kiasi kikubwa sana ule umlindikano wa Mahakama.

Mhe. Spika, lazima tujue katika Mahakama hizi kuna utaratibu wake vile vile, inapofika miezi minne kama kesi haijasikilizwa Hakimu ana uwezo wa kuifuta au miezi tisa Hakimu ana uwezo wa kuifuta. Kwa hivyo, ikiwa kuna matatizo hayo ya ushahidi wa Mawakili au wengineo ndio maana utaona mara nyingi kesi hizi mara zinaaghirika au zinafutwa kwa misingi hiyo. Liliulizwa swali la Mahakama ya Biashara ni kweli tumepitisha sheria ya Mahakama ya Biashara, tulikuwa hatujaianza kwa sababu tulikuwa lazima tukamilishe baadhi ya vifaa na baadhi ya mambo, ninafuraha kusema wiki mbili zilizopita tumeshazindua rasmi na hivi sasa inaanza kazi.

Na pia lilizungumza suala la utaratibu ule wa Mawakilishi. Pia, ninafuraha kusema kwamba kuna sheria ambayo hivi sasa tumeshaifanyia kazi ya *Legal Practitioners Act* ambayo hivi sasa iko tayari. Hii itadhibiti ule mwenendo wa Mawakili kama ilivyozungumzwa. Hii iko tayari na nafikiri karibu mtaiona katika Baraza.

Mhe. Spika, kuna suala la Mufti ambalo lilizungumzwa sana, kwanza napenda niseme tu kwamba katika zile fomu iliulizwa sana fomu mia mbili na kumi na tano, kwa nini misikiti elfu moja na kumi na nane. Napenda ijulikane tu kwamba kwanza kuna *registration* nyengine ambayo tumeshaifanya ya misikiti na madrasa. Lakini fomu tunavyozipeleka kwa mfano fomu mmoja hii tunaipeleka kwa Sheha ya Shehia fulani. Sasa tunamwambia ajaze misikiti yake yote ile iliopo, kwa hivyo, fomu mmoja inaweza kuwa na misikiti mitano, kumi, sita, inategemea idadi ya misikiti iliyopa katika eneo lake na ndio maana ikiwa zile fomu ni kidogo, lakini idadi ya misikiti au idadi ya madrasa ni kibwa.

Lakini hiyo haina maana ndio *registration*. Yeye anatuletea, akeshatuletea, sasa sisi tunaweka moja moja kwa mujibu wa utaratibu wetu. Kwa hivyo, huo ni utaratibu tu wa kumpa sheha kazi ili aweze kutufanyia.

Mhe. Spika, kuna suala la taaluma ambalo lilizungumzwa sana. Mimi nafikiri taaluma ambayo inatakiwa itolewe na Mufti na Afisi yake nakubaliana nayo, lakini tujue tu Mufti hawezi kutoa taaluma kwa Unguja na Pemba yote, watu wenyewe ni kidogo na sasa tukisema kama wao tu ndio watakwenda, mimi nafikiri hiyo sio sahihi. Nakubali taaluma iwepo kwa misingi gani, kwa misingi ya kwamba na wazee wetu, jamii nayo isaidie kutoa taaluma. Lilizungumzwa sana hapa suala la ndoa kwamba ndoa zinavunjika.

Ni kweli wala siwezi kumlaumu Mufti au Afisi ya Mufti. Lakini kuvunjika kwa ndoa mimi nitalaumu jamii na wazee kwa sababu kijana ambaye anakwenda kuoa leo hajenda msikitini isipokuwa ile siku ya Akdi ndio atakwenda msikitini na pale Shekhe akishakufanya Akdi ndio atatoa hotuba ndogo ya kwamba ukae na mke wako, mkigombana uwende kwa wazee na nini. Sasa elimu hiyo ya mara moja haiwezi kufanya kitu, lakini jaminii sisi tunatakiwa hawa vijana wetu tuwalazimishe na wao wahudhuria madrasa, wahudhuria katika mambo kama hayo. Sasa ukisema Mufti ndie afanye hivyo, haiwezekani na ndio maana ni kweli kwamba jamii yetu siku hizi imeharibika kutokana kwamba sisi wazee ambao lazima tubebe lawama hatuwasaidii vijana wetu katika misingi hiyo.

Kwa hivyo, mimi naomba sana kwamba jamii tujitahidini katika kuwaelimisha wazee, katika kuwaelimisha watoto na vijana wetu misingi mizuri, utaratibu mzuri wa dini yetu kwa mambo kama hayo ya ndoa na mambo mengine. Mimi nafikiri hapo tukishirikiana na Afisi ya Mufti tunaweza tukafanyakazi nzuri sana.

Lakini napenda niseme tu kwamba katika misingi hiyo hiyo tuliona kwamba tuna mapungufu kidogo hasa ya Maimamu wetu katika kukhutubu na mambo kama hayo. Nafuraha kusema kwamba tunakubaliana na wezetu wa Uturuki ambao watakuja hapa karibuni kuanzisha masomo maalum kuwapa wale walimu wetu kuwapa maimamu wetu na watu kama hao katika misingi ya dini na katika misingi hiyo ya malezi na mambo kama hayo. Hii tumekubaliana hivi karibuni na *Inshaallah* nafikiri baada ya muda mfupi watu hawa watakuja ili waweze kutusaidia na shughuli hii itakuwa kwa manufaa ya sisi Wazanzibari.

Lakini pia kulizungumzwa suala la Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mimi Mhe. Spika, nisingependa niseme sana kuhusu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa sababu sote tunajua na tunaelewa kidogo kwamba tunaambiwa kuwa tufunge tunapoona mwezi. Nafikiri hiyo ndiyo amri ambayo tunayo, sasa kama wewe hujaona mwezi unafunga, ni shauri yako wewe na Mungu wako, ndio kitu ambacho nahisi ni cha msingi, sheria ipo vizuri imewekwa, fanyeni hivi msifanye hivi, sasa wewe mwezi hujauona unafata watu wengine, basi ni shauri yako na halafu sisi hatuwezi kuingilia mambo kama hayo kwa sababu hata kwa mujibu wa Katiba. kifungu cha 19 Katiba kinasema;

"Mtu muache aamini dini anayotaka."

Sasa kama yeye anaamini dini nyengine haitaki ile kwamba funga ukiona mwezi wa Ramadhani, mwache yeye si atakutana na Mungu wake, ya nini kufanya hivi. Mimi nafikiri ni kwamba sisi wajibu wetu na ndio tunavyofanya, tunapouona mwezi, tuna Kamati maalum ya mwezi tarehe 29 ile tunakaa mpaka saa sita za usiku tunatizama kila pahala, hakuna mwezi, hakuna au tumeona pahala fulani tunatangaza, ndio utaratibu na hivi ndio tunavyofata.

Lakini siku hizi kumeingiliwa Mhe. Spika, na hili limeshatokea mara mbili lakini tumeshawajua wale watu. Wanakaa huko anapiga simu anasema mwezi ameuona pahala kadhaa, kumbe wale ndio hao tunaowaita "Vikanzu Uchwara". Sasa wale wanasema mwezi wameuona kitu ambacho si kweli, wanafata pahala pengine, sisi hatukubali hivyo, hatukubali hata siku moja. Sisi tunafuata misingi yetu ya dini ambayo kuna kamati maalum ikiongozwa na Kadhi Mkuu na Mashekhe kama hao. Sasa huu ndio utaratibu ambao tunaufuata na tutaendelea kuufuata huo, hatutokubali hata siku moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa kuhusu kupata sabuni kwa walimu wetu wa madrasa kwamba jamani angalau tuwagaie sabuni. Mimi nafikiri na hili tulitizameni kwa misingi mirefu, hivi sasa tuna madrasa ambazo zinafika kwa kiasi elfu moja naa na tukishakuzisajili zote zinaweza zikafika elfu mbili na madrasa moja inaweza kuwa na walimu watatu, wanne au watano, ni madrasa chache ambazo zitakuwa na mwalimu mmoja.

Sasa ukisema serikali tutoe kila mwalimu sabuni, ni mzigo mkubwa sana kwa serikali na serikali hatuuwezi. Lakini mimi najua kwamba hao waanzishaji wa madrasa wanajitolea wao wenyewe, yaani wanajitolea wao kwa imani yao na kuwasadia ndugu zao, ni kitu kizuri na ndio maana tukazifanyia *registration* ili tunapopata misaada ambayo tunahisi kwamba madrasa ile tuisaidie hilo tunafanya na tumeshafanya kwa madrasa nyingi Unguja na Pemba. Kwa hivyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba sisi tutasaidia madrasa kwa misingi hiyo, lakini sitotoa kauli hapa ya kusema kwamba Serikali itawapa walimu wa madrasa sabuni, itakuwa hivyo si kweli. Kwa hivyo, sisi tutawasaidia pale ambapo tunapata misaada, tunatizama madrassa gani ambayo inahitaji kusaidiwa na tunasaidia kwa misingi hiyo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa katika Ofisi ya Mufti ni suala zima la Ofisi yenyewe ya Mufti. Ofisi kweli na hasa Pemba, Unguja ingawa tunayo Ofisi nzuri lakini Pemba Ofisi si nzuri, tunajua. Lakini hata Wizara ya Katiba na Sheria Pemba si nzuri. Hata hivi juzi katika mvua hizi kwa kweli lile jengo lilikuwa katika hali mbaya.

Lakini ninachopenda kusema sisi tulikwenda kulitizama, kiwanja tunacho Mkoroshoni tumeshakipata na matayarisho ya kujenga Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria ambayo itai-*accommodate* hata Mufti na wenzake, hiyo ipo mbioni. Lakini hivi sasa kuna mpango tunautizama wa kuhama katika jengo lile ili tuweze kuhamia katika Ofisi nyengine, kwa sababu ya hali ya jengo ambalo liliopo hivi sasa. Kwa hivyo, hiyo tunanua kwamba Ofisi si nzuri na inahatarisha maisha lakini na hatua tumeshaanza kuzichukua.

Mhe. Spika, lilizungumzwa suala la Wakfu na Mali Amana. Ni kweli kwamba nyumba zipo katika hali mbaya na nyumba hizi zipo katika hali mbaya kwa misingi miwili. Kwanza walipaji kodi hawalipi na pili kodi yenyewe ni ndogo sana. Kodi ni shilingi elfu thalathini, ukimuongezea mtu shilingi elfu kumi, ukimwambia shilingi arobaini tu anapiga makelele. Hata kama atakubali shilingi elfu arobaini atakaa mwaka mzima halipi na huku jumba ni bovu. Kwa hivyo, hali hiyo tunaipata na ipo kubwa sana. Tunachukua jitihada za kupambana na matatizo

kama haya, lakini zaidi ni kwamba pale ambapo kuna mtu ambaye anataka kujenga nyumba kama tulivyoshauriwa hapa. Tunakubali na nimeshaanza kufanya hivyo kwamba kuna kiwanja au kuna nyumba ambayo ni mbovu, akija mtu ambaye ana uwezo tunakubaliana kwa misingi ile ile ya *BOT* au misingi mengine yoyote ambayo tunakubaliana. Hapo tutaimarisha majumba yetu, tutaimarisha nyakfu za watu na tutapiga hatua katika misingi hiyo.

Lakini Mhe. Spika, suala la Hijja nalo pia ni suala gumu, lakini huu ni ushauri ambao tumepewa hapa tumeshaanza kuufanyia kazi na kuna baadhi ya Taasisi za Hijja ambazo hivi sasa zinakusanya fedha kidogo kidogo kwa mtu ambaye anayetaka. Kwa hivyo, ombi langu kwa jamii au kwa wananchi ni kwamba yeyote anataka kujilimbikizia mkusanyo ili baadae awe na uwezo wa kwenda Hijja, basi Taasisi zetu za Hijja zimeshaanza kazi hiyo na tunawakaribisha nyote. Na hiyo unalipa wewe mwenyewe kidogo kidogo kwa utaratibu maalum, unalipa mpaka ikifika *time* unaambiwa sasa kutokana na malimbikizo yako unaweza sasa kwenda kufanya safari ya Hijja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, ninawaombeni jamii yetu na wananchi wote kwamba tuukubali utaratibu huu ili watu wengi waweze kwenda kuhiji kama wenzetu wanavyofanya Indonesia na Uturuki wote wanafanya katika misingi hiyo. Kwa hivyo, tujaribuni kufanya haya yanaweza yakasaidia sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa ni suala la vizazi na vifo. Suala la vizazi kuhusiana na vyeti vya vizazi ni aina mbili na ninaomba hapa tuelewane; Kuna mtu anayezaliwa leo, kesho na keshokutwa. Sasa huyu ukenda kutaka cheti za kuzaliwa haina maana kwamba unataka kwenda kupata cheti cha *ID* ya Mzanzibari. Ni wajibu wako kama umezaliwa leo kwenda na kupata cheti cha kuzaliwa.

Matatizo yaliopo katika vyeti hivi ni kweli unaweza ukakaa mwaka mmoja mpaka ndugu yako akazaliwa hujapata. Tunajua hivi karibuni tulikuwa na matatizo ya vyeti vile wanaita "magamba", ilikuwa hakuna fedha, magamba hamna, tulipopata fedha kukawa na matatizo *press* kwamba zile namba haziandikwi kwenye magamba yale. Kwa hivyo, huwezi ukatoa cheti bila ya namba zile. Kwa hivyo, matatizo haya ndiyo yaliyofanya kuwe na upungufu wa vyeti. Lakini hivi sasa *Alhamdulillahi* tunakwenda hivyo hivyo kidogo kidogo vyeti hivyo tunavyo.

Lakini kwa kuona hali ya watu ambavyo wanavyosumbuka, tumejaribu kufanya *pilot project* ya Wilaya ya Magharibi katika suala la kutoa vyeti kwa njia ya *electronics* na tumepata ile, tumefanya ile *pilot project*, tumeona matatizo gani tuyarekebishe. Sasa hayo tunayarekebisha baada ya kukamilika na kupata fedha, vyeti sasa vitakuwa kwa njia hiyo ambapo vinaweza vikatolewa siku ile ile ukenda na utapata cheti chako siku ile ile au siku ya pili unaweza ukapata siku ya pili.

Kwa hivyo, utaratibu huo tunao na tunaufanya, lakini sasa vyeti vyengine ambavyo tunaita *late registration. Late regitration* ni vyeti ambavyo pengine wewe ulizaliwa miaka sitini nyuma, lakini sasa huna cheti. Sasa unapokwenda pale hatuwezi tu kukupa cheti, kuna utaratibu wake, ujaze fomu, tujue ilikuwaje kwa nini ukachelewa, kwa nini hujachukua vyeti au cheti kile hujachukua. Sasa kuna masuala mengi lazima ujaze; kama unasema ulikuwa unasoma skuli, wende skuli na mwalimu mkuu athibitishe kwamba huyu alikuwepo. Sasa utaratibu ule kidogo ni mrefu na huwezi tu kutoa cheti kabla hujatimiza utaratibu ule. Sasa haya ndiyo yanayowafanya watu wengine hawajazi au anajaza anavyotaka wakirudishwa itakuwa hawana furaha. Lakini lazima tufuate utaratibu.

Sasa mimi naomba niseme tu kwamba *late registration*, mtu anapokuja kuchukua fomu zile za *late registration* basi tunaomba azijaze kwa mujibu wa utaratibu ulivyo uliomo katika fomu ile na akimaliza hakuna matatizo yoyote. Kama kuna matatizo wanakuja Ofisi kwetu tunawasaidia na wengi wameshakuja tunawasaidia. Kwa hivyo, ninaomba tufuate utaratibu ili tuweze kupata vyeti hivyo.

Na vile vyeti vya kawaida vya mtu anayezaliwa leo na kesho, kuna utaratibu mwengine ambao sasa umewekwa kwa kila Wilaya anapelekewa Mkuu wa Wilaya. Sasa na kule kuna matatizo ambayo yalikuwepo tumeshayaona na tumejaribu kuyarekebisha, kwa sababu unapokwenda Wilayani vyeti vimerundikana, anayepiga vyeti kule hayupo, pengine ni mtu mmoja tu, lakini sekretarieti yule yule ana suala hili, ana suala hili. Kwa hivyo, anaweza akakaa wiki nzima bado hajajaza vyeti vile. Kwa hivyo, haya yote ni matatizo ambayo kweli ninakubali kuwa kuna matatizo na matatizo hayo tumeyaona na tunayachukulia hatua ipasavyo.

Mhe. Spika, nije katika suala jengine ambalo lilizungumzwa la *transworld*. Kwa nini kampuni hii ikawa *registered* mara mbili. Baada ya kulipata suala hilo tulifanya uchunguzi wa ghafla na tulichofanya hatukuwaambia watu wa *registration* kule isipokuwa tuliwaambia tu walete fomu za aina mbili; walete *registration document* ya 2012 na walete *registration document* ya 2014. Kwa bahati zililetwa hizi. Hii moja ya 2012 na hii moja ni ya 2014. Mhe. Spika, ya 2012 *Tansworld Aviation Limited* imekuwa *registered* kwa namba L.2752/2012 na hii ya 2014 imekuwa *registered* kwa L.7095/2014.(*Makofi*)

Kwa hivyo, ni kweli kwamba kampuni hii imekuwa *registered* mara mbili. Sasa Mhe. Spika, *registrations* zetu tunazijua ni *manual*, yaani za mkono. Kuna buku linafika hivi ukichukua lile buku la *registration*. Sasa hii inapokuwa *registered* na zimekuwa *registered* kwa mkono, si kwa *electronics*. Ingekuwa ni kwa *electronics,* Mhe. Spika, sasa hivi wafanyakazi hawa ningeliwafukuza kazi, kwa sababu

*electronics* ukiweka pale inaonesha, ukiweka *transworld* tu inakuja zote zile. Lakini kwa mkono huwezi, unaweza ukapitia mara sita hapa ikawa hujui au hujaiona bahati mbaya.

Sasa kilichotendeka ni kwamba baada ya *search* hawa akaona kwamba hamna *transworld* na wakati huo mwaka 2012 alikuwa anayefanya *registration* alikuwa na mtu mwengine na hivi sasa ni mtu mwengine. Kwa hivyo, pia ingelikuwa ni mtu yule yule pengine angalau angelikuwa anakumbuka kwamba mbona kitu kama hichi kinanipitia katika akili yangu. Lakini akapitia akaona hamna kitu. Kwa hivyo, akasema hamna *registration*. Kwa hivyo, akafanya *registration*.

Sasa imekuja kugundulika kwamba *registration* ni mbili na kama *registration* ni mbili, siyo tatizo Mhe. Spika. Kwa sababu kisheria chini ya *Company Decree* Sura ya 155, Kifungu cha 19 kinasema kwamba ikiwa kutatokea matatizo ya ku-*register* mara mbili, basi yule aliyekuja mwisho atatakiwa afute jina lile kwa kuona kwamba lile la mwanzo limeshakuwa *registered* na hiyo imefanywa makusudi. Kwa sababu na hawa walioandika sheria wanajua kwamba matatizo haya yanaweza yakatokea. Hivyo ndivyo ilivyokuwa na kwa misingi hiyo Mhe. Spika, mimi ninamuomba sana huyu aliye-*registered* mara ya pili, basi tutumie Kifungu cha 19 cha kumtaka na ninafikiri ameshaambiwa kwamba afute jina lake ili liweze kuwa *registered* kwa njia nyengine.

Mhe. Spika, kutokana na haya na ndiyo maana hata bajeti yetu tulisema kwamba tunaomba fedha ili mambo haya sasa tuyafanye kwa *electronics*. Ndiyo matatizo kama haya ambayo yanatokea mara kwa mara. Mhe. Spika, hilo ndiyo suala la *transworld.* Lakini sasa nije katika suala la kesi ya Micheweni.

Mhe. Spika, kulizungumzwa kesi ya Micheweni ambayo kuna huyu mfanyakazi wa Tume ya Uchaguzi, sijui na mwalimu na mtu mwengine. Hawa kama ilivyozungumzwa juzi ni kwamba walikwenda wakataka kupachua bendera ya CUF katika nyumba ya mtu ya wale mabalozi na nini. Baadae kukamka rabrasha rabrasha, Polisi wakachukua hatua ya kuwachukua hawa kuwapeleka Mahakamani. Na Mahakama ikawaweka ndani kwa wiki mbili, ninafikiri ile kesi yao iende.

Na nafikiri suala hili lilikuwa jana au juzi. Sasa kinachosema ni kwamba kuna watu wa kisiasa walikwenda na kuwalazimisha Mahakama ninafikiria ku-*revise* ile kesi na wale wakatolewa nje kwa dhamana. Sasa mimi ninasema hivi Mhe. Spika, kwamba kwanza dhamana ni haki ya kila mtu, lakini ina utaratibu wake. Sasa waliowekwa ndani kwa wiki mbili na Hakimu, sijui kama ni Hakimu wa Wilaya, ninafikiri atakuwa Hakimu wa Wilaya.

Sasa sheria inaweza kumtaka Hakimu wa juu kufanya *revision*, yaani mapitio ya ile kesi ikiwa kuna jambo la haraka. Sina uhakika kwa sababu nimesikia hivi sasa hapa, sina uhakika kwamba utaratibu wa kufanya *revision* kwa Hakimu aliyezidi ile ngazi imechukuliwa au haikuchukuliwa. Lakini ikiwa haikuchukuliwa itakuwa hilo ni kosa. Mimi ninahakikisha na ninaahidi kwamba ikiwa limechukuliwa halikufanywa kwa misingi hiyo ya kisheria, basi na mimi binafsi nitahakikisha kwamba Hakimu huyu amekiuka *ethics* za Mahakama na atachukuliwa hatua.

Lakini ikiwa kenda kwa kisheria, wamefanya *revision* kwa mujibu wa sheria inavyotakiwa wakasikilizwa kwa mujibu wa utaratibu unavyotakiwa, halafu wakaachiliwa. Mimi ninafikiri hiyo itakuwa ni suala la kisheria na limefuata mkondo wake na itakuwa hatuna tatizo.

Kwa hivyo, ninachoweza kusema hapa Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Saleh Nassor Juma, ni kwamba suala hili mimi nitalifuatilia ili nijue, utaratibu gani uliofuatwa; wamefuata kisheria, hatuna matatizo, lakini kama hawakufuata kisheria, hapo tutakuwa na matatizo na hatua tutazichukua. Kwa hivyo, Mhe. Hija, kwa taarifa hiyo ninaomba sana ukubaliane na mimi kwamba nitachukua hatua za kufuatilia na kutizama hapo ambapo imefikia kesi hii.

Ninashukuru sana Mhe. Hija, kwa hilo, lakini la pili alilosema, alizungumzia suala la skuli ambazo zinapika chakula mwezi wa Ramadhani. Mhe. Hija, mimi ninafuatilia sana mambo haya na ni kweli. Ninakubaliana na wewe kwamba kuna skuli ambazo zilikuwa zinapika chakula mwezi wa Ramadhani, lakini siyo leo ni siku nyingi na ninafikiri tukijaaliwa Ramadhani hii itakuwa hakuna.

Kwa sababu taarifa hiyo tuliipata na tukaifanyia kazi sana na hizi ni skuli za Wakorea. Skuli za Wakorea ambazo zipo Tomondo, Mitondooni, Chakani, Wakorea ni Wakristo, kuna watoto wa Kiislamu wanakwenda kule, sasa wakifika wanaambiwa aah! kusoma kwa sababu Ramadhani hiyo usifunge, kwa sababu itakuwa hupati elimu haikai vizuri, almuradi mambo kama hayo. Hivyo, wale watoto *in one way or another* wanalazimishwa kula. Lakini tulipopata habari hii tukaingilia kati na ninafikiri hili suala limemalizika na kama litatokea basi tutawaondoa tu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hii naomba uwe na uhakika kwamba tumelifuatilia kwa kirefu na mambo mengine ambayo yanafanywa pale. Ninafuraha kusema kwamba tatizo hili kwa kiasi kikubwa limeondoka lakini kama lipo, naomba muniambie, ikiwa bado lipo linaendelea, lakini Ramadhani haijafika, hatuwezi kusema linaendelea. Lakini yale mambo mengine bado tunaya....

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, muda unakaribia sana kwisha...

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Ninashukuru sasa hivi nitamaliza.

**Mhe. Spika:** Na tuna tatizo kubwa sana la msingi kwamba kwa kawaida kipindi hichi *quorum* inakuwa ni ngumu sana. Na *quorum* inatimia vizuri kama Waheshimiwa Wajumbe itakuwa tumehudhuria vikao vyetu kwa wakati. Kwa kweli tunashindwa kuhudhuria kwa wakati. Sasa muda uliobaki ni dakika kama nane tu kufikia muda wa kawaida kuondoka.

Kwa ninavyoelewa na sote humu ndani tupo mashahidi wa hilo. Tukiachia *quorum* hii ambayo sasa hivi ipo, kwa hivyo, Jumatatu tukae, hatutaki. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, ninaomba sana ili twende kwa mtiririko mzuri na kwa maelezo hayo ambayo nimeyatoa kwa heshima zote kwenu nimuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, atowe hoja tuongeze muda tumalize hii kazi, ili Jumatatu tuje tukiwa *fresh*. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliokuwa mbele yetu ni mdogo ukilinganisha kwa mujibu wa Kanuni, na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria bado hajamaliza kufanya majumuisho ya wizara yake. Hivyo, niliombe Baraza lako tukufu tuweke Kanuni ya muda kando, ili kumuwezesha Mhe. Waziri, kufanya majumuisho. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, basi kwa unyenyekevu mkubwa sana, naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.*(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, endelea, usichukuwe muda mkubwa zaidi tupitishe mafungu haya ukafanye kazi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nitachukua dakika mbili tu kumalizia masuala mawili tu ambayo yamebakia. La kwanza ni suala la Haki Miliki ambalo lilizungumzwa. Mimi naomba kwa sababu mwanzo nyuma walikuwa watu hawafahamu, lakini hivi sasa vile vikundi tunashukuru vinafahamu na tunawaomba sana wajiorodheshe ili tuwa-*register* ili haki yao tuweze kuilinda kisheria.

La pili, ambalo alilizungumza Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, ni kuhusu Katiba inayopendekezwa. Kweli sikutia na wizara yangu haikutia, Wizara ya Katiba na Sheria ya Bara haitotia, kwa sababu sio suala letu. Hili ni suala ambalo

lilitoka katika *Constituent Assembly* na linatoka huko, linakwenda kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba. Kwa hivyo, sisi ni *run way* wizara yangu na wizara ya Bara inayohusiana na Katiba na Sheria hatuhusiki.

Lakini la mwisho, ni lile suala la fedha zile ambazo alizizungumza, je, alisema ni bilioni 1,627,100,000/-, au ni bilioni 1,567,300,000/-. Katika kitabu cha wizara inaonesha bilioni 1,500,000,000/- na katika kitabu kikubwa ni bilioni 1,600,000,000/-. Ni kweli hiki kitabu kidogo kimekosea kwa sababu, ukifungua kile kitabu kikubwa katika ukurasa wa 434 kuna bilioni 1,567,000,000/-. Lakini katika ukurasa wa 436 kuna ruzuku ambayo inapewa *DPP*, katika ile shule ambayo tunafundishia, kule kuna ruzuku ya 59 milioni. Sasa ukizijumlisha hizi bilioni 1,567,000,000/- na 59,000,000/-, inakuja katika bilioni 1,627,000,000/-.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba tena niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yao na yote nawahakikishia tutaifanyia kazi, ili tuweze kujenga wizara yetu kwa misingi ya katiba na sheria.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:**Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa mwaka 2015/2016 wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

## KAMATI YA MATUMIZI

### FUNGU G01 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 01 | Wakala wa Usajili ya Biashara na Mali | Sh.201,011,596/= |
| Kifungu 09 | Ofisi ya Mrajisi Vizazi na Vifo | Sh.374,052,404/= |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.575,064,000/=** |

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA USAJILI NA USIMAMIZI WA MASUALA YA DINI**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Usajili wa matukio ya kijamii | Sh.421,191,000/= |
| Programu Ndogo S02 | Usajili wa biashara na mali | |

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, nilipohoji usajili wa *transworld*, nimemfahamu nakubaliana na hoja yake. Lakini wakati kampuni hii tayari imesajiliwa tayari ziko taarifa kwamba kampuni hii imeshinda *tender* na Mhe. Waziri, amekiri kwamba kampuni hii iliingia kimakosa, hiyo *manual* yake, ingawa mimi siwezi kuamini kwamba *manual* imepotea, lakini tuseme ndio *manual* imesababisha hayo.

Lakini je, kwa sababu kampuni imeshinda *tender*, utaratibu wa *tender* utakuwaje wakati tayari imehalalishwa kufanyakazi ya *tender* ya pesa nyingi. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nijuwe ni kampuni ipi sasa, maana yake kuna *transworld* mbili, ipi iliyoshinda *tender*; ya kwanza iliyosajiliwa mwaka 2012 au ya pili iliyosajiliwa 2014.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, *transworld Zanzibar Aviation* ambayo ni ya 2012 haina tatizo. Hii ya mwaka 2014 ndio iliyoshinda *tender*. Sasa kama imeshinda *tender*, hiyo ya *handling* ya Uwanja wa Ndege na huku kampuni yenyewe imekuwa ni *fake* kiasi hicho. Ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa?

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, katika sheria na katika utaratibu wa mikataba, unapodanganya basi mambo yako yote yale uliofanya huwa sio halali. Sasa mimi siwezi kusema hapa, ninachoweza kusema ni kwamba hao waliotoa *tender* na wakatizama *tender*, ikiwa watapata taarifa ya kwamba ni *fake* kampuni ile, basi uwamuzi ni wao.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, sio uwamuzi ni wao, kampuni hii imetiliana saini na serikali, mkataba wa *tender* hiyo umetiwa saini Dubai na serikalini chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa ikiwa kampuni sio halali, maana yake serikali ndio iliyotia saini, sasa asiwasukumie hao waliohusha, aiangalie serikali kwa nini imeburururwa mpaka imekubali kutia saini na kampuni isiyo sahihi. Kwa hivyo, asiwasukumie hao waliohushi, waliohushi wanatafuta biashara, wewe ni serikali sasa ndio ambaye umetia hasara serikali kwenda kutia saini mkataba ambao kuwa kampuni sio halali. Naomba maelezo zaidi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni taarifa ambayo tunaipata hivi sasa, kwamba ni mkataba ambao umetiwa saini na serikali. Kwa hivyo, huwezi kutoa maamuzi hapa kisheria, ni lazima tuyatizame, tukishayatizama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ipo, tutakaa tutatizama utaratibu uliofikiwa katika kutia saini hiyo, baadae serikali itaamua. Lakini huwezi kusema hapa kwa sababu ni lazima tupite katika *procedures,* na *procedure* moja ni kupeleka kwa Mwanasheria Mkuu tukaitizame. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ipo na shughuli hiyo itazingatiwa.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja yake. Lakini labda aniambie ni lini watafanya hivyo ili watupe jibu. Kwa sababu hili jambo ni la serikali na huko mbele kuna kuja wizara husika ambao kuwa ndio imeingia mkataba. Sasa atuambie ni lini atamaliza hili suala tujuwe, ili huko mbele wizara husika inayohusika na hili jambo tuweze kuizuwia au kuiruhusu. Sasa labda atuambie ni lini mtakaa kitako.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema lini, kwa sababu hata kuuona sijauona huo mkataba. Kwa hivyo, ni lazima niupate na niutizame, halafu nikisharidhika nipeleke katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, kwanza niupate, nikishakuupata, nikauona na kuutizama basi nitataka ushauri kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, ndio utaratibu ulivyo. Kwa hivyo, lini siwezi kusema, lakini tukiupata tutafanya haraka iwezekanavyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tunakushukuru Mhe. Hija Hassan, umetuambia tuendelee. *(Makofi)*

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S02 | Usajili wa biashara na mali | Sh. 1,290,605,000/= |
| Programu Ndogo S03 | Usimamizi wa haki miliki | Sh. 240,000,000/= |
| Programu Ndogo S04 | Usimamizi wa masuala ya dini | Sh. 945,412,000/= |
| **Jumla ya Programu P01** | | **Sh. 2,897,208,000/=** |

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA MIPANGO NA UENDESHAJI WA SEKTA YA SHERIA**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Uongozi na uendeshaji katika sekta ya sheria | Sh. 825,316,000/= |
| Programu Ndogo S02 | Mipango, sera na utafiti katika sekta ya sheria | Sh.1,622,872,000/= |
| Programu Ndogo S03 | Uratibu na uendeshaji wa wizara Pemba | Sh. 563,904,000/= |
| **Jumla ya Programu P02** | | **Sh.3,012,092,000/=** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.5,909,300,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU G02 - MAHAKAMA KUU**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 01 | Utawala Unguja | Sh.120,000,000/= |
| Kifungu 02 | Ofisi Kuu Pemba | Sh. 30,000,000/= |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.150,000,000/=** |

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU KUU USIMAMIZI WA UPATIKANAJI WA HAKI**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Usimamizi wa upatikanaji wa haki | Sh.2,921,593,000/= |
| **Jumla ya Programu P01** | | **Sh.2,921,593,000/=** |

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU KUU USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UENDESHAJI NA UTAWALA WA MAHAKAMA**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Uendeshaji na utawala wa Mahakama Unguja | Sh. 626,988,000 |
| Programu Ndogo S02 | Uendeshaji wa shughuli za Mahakama Pemba | Sh.1,594,519,000 |
| **Jumla ya Programu P02** | | **Sh.2,221,507,000** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.5,143,100,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU G03 - MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR**

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU KUU YA MAGEUZI YA UTOAJI HUDUMA ZA KISHERIA**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Mageuzi ya utoaji wa huduma za kisheria | Sh.544,064,000/= |
| **Jumla ya Programu P01** | | **Sh.544,064,000/=** |

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Utawala na uendeshaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | Sh. 466,136,000/= |
| **Jumla ya Programu P02** | | **Sh. 466,136,000/=** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.1,010,200,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU G04 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA KESI ZA JINAI**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Uendeshaji wa kesi za jinai | Sh.146,037,000/= |
| Programu Ndogo S02 | Usimamizi wa kesi za jinai | Sh.100,555,000/= |
| **Jumla ya Programu P01** | | **Sh.246,587,000/=** |

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UENDESHAJI KATIKA OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Mipango na uendeshaji | Sh.1,086,513,000/= |
| Programu Ndogo S02 | Uratibu wa shughuli za mashtaka Pemba | Sh. 294,000,000/= |
| **Jumla ya Programu P02** | | **Sh.1,380,513,000/=** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.1,627,100,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU G05 - TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU KUU YA MAPITIO YA SHERIA**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Mapitio ya sheria | Sh.251,280,000/= |
| **Jumla ya Programu P01** | | **Sh.251,280,000/=** |

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UWENDESHAJI**

| | | |
|---|---|---|
| Programu Ndogo S01 | Utawala na uendeshaji | Sh.275,720,000/= |
| **Jumla ya Programu P02** | | **Sh.275,720,000/=** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.527,000,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana na makadirio wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa ya kumaliza shughuli hii kwa mafanikio makubwa. Sasa bila ya kukawia basi nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hiki mpaka tarehe 01 Juni, 2015, saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 2:08 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 01/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*